# Nipashe

Ijumaa Februari 14, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • Na. 0580154

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US

## Tanzania yapatiwa mkopo wa tril. 3.3/- ujenzi reli ya kisasa

UKURASA 3




UKURASA 13

# Rugemalira aibua mengine kortini

• **Adai** kumwandikia Gavana BoT awataje walio-pokea fedha za Escrow... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**TAHADHARI MVUA KUBWA ZA MASIKA**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa tahadhari ya kuwapo kwa mvua kubwa (juu ya...

UKURASA WA 8

**MAAMBUKIZI HOMA YA INI SASA TISHIO**

ASILIMIA 40 ya watu 2,000 waliofanyiwa utafiti wa kubaini iwapo wameathirika na maambukizi ya...

## Watoto 5 wafariki wakitoka shuleni

UKURASA 3



Mabaki ya bidhaa, baada ya vibanda zaidi ya 60 vya wafanyabiashara wadogo maarufu Machinga wa eneo la Makoroboi, jijini Mwanza kuteketea kwa moto juzi usiku. **PICHA: ROSE JACOB**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


## Madaktari kumwona JPM kuhusu ukosefu wa ajira

UKURASA 2

**MICHEZO** EYMAEL AGAWA KAZI NCHIMBI, MOLINGA UK.32 | **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Rugemalira aibua mengine kortini

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA, James Rugemalira anayekabiliwa na wenzake wawili katika kesi ya uhujumu uchumi, amedai mahakamani kuwa amemwandikia barua Gavana wa Benki Kuu (BoT), akimtaka ataje watu wote waliopokea fedha kutoka kwenye akaunti ya Tegeta Escrow ili ajisafishe.

Kadhalika, alidai kuwa ameziandikia notisi taasisi tisa za serikali akiwamo Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Biswalo Mganga, Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa (TISS), Diwani Athuman, Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), akiomba mahakama hiyo imwondoe katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili, endapo DPP hatafanya hivyo.

Taasisi nyingine zilizoandikiwa notisi hiyo ni, Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robert Boaz, Gavana wa BoT, Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kamishna wa Magereza, Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Clement Mashamba na Msajili wa Mahakama Tanzania.

Rugemalira alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, wakati kesi hiyo ilipokuja kwa ajili ya kutajwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upepelezi bado haujakamilika.

Hata hivyo, Rugemalira alinyoosha mkono na alipopewa kibali cha kuongea, alidai kuwa aliandika barua kwenda Benki Kuu ya Tanzania akieleza kwamba hajapatiwa hata senti moja kutoka kwenye akaunti ya Escrow na kwamba fedha alizopewa yeye ni zile zilizotolewa kwa amri ya mahakama kwa Kampuni ya Power African Power (T) Limited (PAP).

"Mheshimiwa hakimu nimemwandikia Gavana kumwomba aniorodheshee watu wote waliopokea fedha kutoka akaunti ya Escrow ili nijisafishe kwa sababu sikupokea hata senti moja. Majibu ya Gavana aliniambia hawezi kutoa orodha hiyo mpaka pale atakapopata amri halali ya mahakama ya kufanya hivyo," alidai Rugemalira.

Awali, Rugemalira alidai alipeleka maombi mahakamani hapo kwamba aliandika barua kwenda kwa Kamishna wa TRA, akieleza namna Benki ya Standard Chartered ya Hong Kong, walivyokua wakikwepa kodi na ushuru wa forodha

INAENDELEA UK. 8




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (kushoto), na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Standard Chartered nchini, Sanjay Rughani, wakibadilishana makabrasha, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kusaini makubaliano ya mkopo wa Sh. trilioni 3.3 kwa Serikali ya Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapanga kumwona JPM madaktari kukosa ajira

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Madaktari (MAT), kinatarajia kukutana na Rais John Magufuli, wiki ijayo, kuzungumzia masuala mbalimbali ikiwamo ukosefu wa ajira, udhalilishaji na motisha za watumishi.

Rais wa MAT, Dk. Elisha Osati, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano huo ambao utashirikisha watumishi zaidi ya 1,000, na kueleza kuwa wanatarajia mkutano huo kufanyika Alhamisi.

"Tumekuwa tukifanya juhudi za kutaka kuonana na kukaa pamoja na Rais Magufuli ili kufanya mazungumzo ya masuala mbalimbali yanayohusu watumishi wa sekta ya afya, ikiwamo pongezi zetu kwa kazi kubwa iliyofanywa na serikali kuboresha huduma," alisema na kuongeza:

"Leo tunayo furaha kuwataarifu kuwa amekubali ombi letu na yupo tayari kukutana nasi Februari 20, mwaka huu."

Alisema awali walitarajia kukutana naye Machi 3, mwaka huu, katika Mkutano Mkuu wa MAT, lakini aliomba kurudisha nyuma siku za kukutana.

Alisema mbali na kuelezea mafanikio yanayotokana na juhudi kubwa zilizofanywa na serikali, wanatarajia kueleza kuhusu tatizo la ajira nchini linalotokana na idadi kubwa ya wahitimu wanaozalishwa kutoka vyuoni kila mwaka.

"Kila mwaka wahitimu 1,500 wa taaluma ya udaktari wanaingia mtaani na hakuna ajira, lakini taarifa ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inaeleza kuwa wana upungufu wa madaktari kwa asilimia 51," alisema Dk. Osati.

Alibainisha zaidi kuwa serikali imejenga hospitali mpya 69 za wilaya na zilizokuwapo ni 70, lakini bado hawajaajiri madaktari.

Alisema ili kuondokana na adha hiyo, wanaishauri serikali kushirikiana na sekta binafsi kuanzisha vituo vya afya nchini ili kusaidia kutoa ajira na huduma bora na za uhakika.

"Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), daktari mmoja anapaswa kutibu wagonjwa 10,000 kwa mwaka, lakini nchini daktari mmoja anatibu wagonjwa 25,000 kwa mwaka, na ukiangalia kweli serikali haina uwezo wa kuajiri wahitimu wote," alisema Dk. Osati.

Alisema athari nyingine ambayo ilikuwapo, lakini inaendelea kupungua ni wanasiasa kuingia majukumu ya watumishi wa afya kwa ajili ya kujipatia umaarufu.

Kwa mujibu wa Dk. Osati, wanatarajia kuzungumzia suala la motisha na maslahi ya watumishi wa sekta ya afya nchini katika kuendelea kusaidia kuboresha sekta ya afya.

## Tahadhari mvua kubwa kunyesha

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa tahadhari ya kuwapo kwa mvua kubwa (juu ya wastani) baadhi ya mikoa ya Tanzania na Visiwani.

Mikoa hiyo imetajwa kuwa ni Dar es Salaam, Pwani, visiwa vya Pemba na Unguja na baadhi ya maeneo katika mikoa ya Geita, Mwanza, Simiyu, Shinyanga na Mara huku mvua za wastani mpaka chini ya wastani (mvua ndogo) zikitarajiwa katika mikoa ya Kagera na Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma (Wilaya za Kakonko na Kibondo).

Kwa mujibu wa utabiri wa mvua za masika zilizotolewa jana na mamlaka hiyo kupitia kwa Mkurugenzi Dk. Agnes Kijazi, mvua hizo katika maeneo tajwa zinatarajia kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi na kuisha katika kipindi cha wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Mei.

Akizungumza wakati wa kutoa utabiri huo, Dk. Kijazi alisema mvua hizo kubwa zitasambaa mpaka katika maeneo ya Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro. Dk. Kijazi, alisema mvua hizo hususani za juu ya wastani zinatarajiwa kuleta athari katika maeneo tofauti na kuzitaka mamlaka husika kuchukua tahadhari kukabiliana nazo.

"Yale maeneo ambayo yatapata mvua za wastani mpaka juu ya wastani tunategemea athari za kuharibika kwa miundombinu kutokea, pia usalama wa majisafi utaathirika kutokana na mvua zinazotarajiwa, hivyo Mamlaka za Miji zichukue tahadhari," alisema Dk. Kijazi. Alisema kwa upande wa sekta ya afya, wachukue tahadhari ya kutokea kwa magonjwa ya mlipuko na malaria kwenye maeneo yatakayopata mvua za wastani mpaka juu ya wastani. Aliitaka menejimenti ya maafa pia ichukue tahadhari kwa kuwa kuna uwezekano wa kutokea mafuriko kwa baadhi ya maeneo yatakayopata mvua kubwa na hivyo kusababisha upotevu wa maisha, uharibifu wa miundombinu na mali nyingine.

"Mamlaka inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, wasafirishaji na Mamlaka za Maji kuendelea kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika," alisema Dk. Kijazi.

Alivita vyombo vya habari nchini kufuatilia mara kwa mara na kusambaza taarifa sahihi za mienendo ya hali ya hewa na mirejeo pamoja na tahadhari na ushauri unaotolewa na TMA.

# Tanzania yapigwa jeki ujenzi wa reli ya kisasa

**Na Enock Charles**

BENKI ya Standard Chartered imesaini makubaliano ya kuikopesha Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Fedha na Mipango Dola za Marekani bilioni 1.46 (sawa na Sh. trilioni 3.3), kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya pili wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora.

Kipande hicho kina urefu wa kilomita 550 katika mkakati wa kuboresha njia za usafiri nchini.

Akizungumza jana wakati wa kusaini mkataba huo, Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo nchini, Sanjay Rughani, alisema kwa miaka 103 ya uwepo wa benki hiyo nchini mkataba huo ni wa kihistoria kuwahi kufanyika baina yake na serikali.

Alisema utasaidia kupunguza tatizo la usafiri na usafirishaji wa mizigo pamoja na kuokoa muda unaopotea katika shughuli za usafiri kwa treni za kawaida ambazo haziendi kasi kama ilivyo kwa treni za kisasa.

"Mkataba huu utaenda kugusa maisha ya watu wengi na hakuna kitu kizuri katika maisha kama kusaidia wengine," alisema Rughani.

Akizungumza kuhusu mkopo huo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema kusainiwa kwa mkataba huo kutawezesha ujenzi wa reli hiyo ya kisasa kufika mpakani mwa Uganda, Rwanda, Burundi na Kigoma kukamilika kwa wakati na kusaidia kuboresha maisha ya wananchi kiuchumi, kukuza kilimo na kuboreshwa kwa huduma za kijamii.

"Mkopo huu ni takribani Sh. trilioni 3.3 za wale wanaosema kuwa deni la taifa linakuwa niendelee kusisitiza kuwa deni la taifa ni himilivu," alisema Dk. Mpango.

Kwa mujibu wa waziri huyo, ni muhimu kukopa kwa kuwa uwekezaji huo ni wa hadi miaka 200 ijayo na kwamba reli hiyo itaenda kwa kasi na kubeba mzigo mkubwa kuliko iliyopo sasa, kukuza uchumi wa taifa na wa mtu mmoja mmoja, kukuza kilimo na biashara.

"Kuna baadhi ya wabia wetu tena wa siku nyingi tu tuliwaomba waingie kwenye safari hii kwenye kuchangia hili na ni mkopo wala siyo kwamba wanatupa bure, lakini wametukatalia kwa hiyo Standard Chartered hawa tunawashukuru sana," alisema Dk. Mpango.

## Wanafunzi watano wagongwa, wafariki dunia wakitoka shuleni

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

WANAFUNZI watano wa Shule ya Msingi Ndelenyuma iliyoko katika Halmashauri ya Madaba mkoani Ruvuma, wamefariki dunia na mwingine kujeruhiwa kutokana na kugongwa na gari wakati wakitoka shuleni.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alidai tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa nane mchana kwenye barabara ya kutoka Njombe kwenda Songea, ambayo wanafunzi hao walikuwa wanatembea kandoni mwake.

Alidai wanafunzi hao waligongwa na gari lenye namba za usajili T 443 AQT aina ya Landcruser, mali ya Kampuni ya Camsat.

Aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Glory Kilasi (12), Ushindi Juma (12), Isaya Mkani (13), wote wa wanafunzi wa darasa la nne, Evaristo Miligo (10), mwanafunzi wa darasa la Pili, na Victor Luoga, (10), mwanafunzi wa darasa la kwanza.

Kamanda Maigwa alimtaja aliyejeruhi kuwa ni Hilda Kilasa (12), mwanafunzi wa darasa wa la nne, ambaye baada ya ajali hiyo, alikimbizwa katika hospitali ya mkoa kwa ajili ya matibabu na anaendelea vizuri.

Alidai kuwa gari hilo lililokuwa linatoka Njombe kwenda Songea katika Kijiji cha Ndelenyuma, liliacha njia na kuwagonga wanafunzi hao sita kisha likapinduka.

Alidai gari hilo lilikuwa linaendeshwa na mwanamume aliyemtaja kwa jina moja la Salum na baada ya ajali hiyo, alikimbia na kutokomea kusikojulikana.

Kamanda Maigwa alidai chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi wa dereva ambaye hakujali hali ya mvua kubwa iliyokuwa ikinyesha katika kijiji hicho.

Alidai kuwa baada ya kugongwa, wanafunzi hao walidondokea mtaroni na kwamba, watatu walisombwa na maji na miili yao kuopolewa takribani mita 100 kutoka eneo la tukio na jitihada zinafanywa kumkamata dereva huyo.


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRIME MINISTER'S OFFICE
LABOUR, YOUTH, EMPLOYMENT AND THE PEOPLE WITH DISABILITIES
OCCUPATIONAL SAFETY AND HEALTH AUTHORITY (OSHA)

**Awards for Occupational Safety and Health (AOSH) 2020**

Theme of the year: Violence and harassment in the world of work




**Introduction**
In commemorating World day for Safety and Health at Work and as a part of National OSH promotion and awareness creation activities, Occupational Safety and Health Authority (OSHA) is inviting all owners of workplaces or employers to compete for the Awards for Occupational Safety and Health (AOSH).

**Aim**
To encourage private and public workplaces throughout Tanzania to develop, implement and evaluate strategies that help achieve a healthier and safer work environment.

**Entry Eligibility**
Applications are open only for workplaces which are registered and operated in Tanzania Mainland, and having OSHA Registration Certificate. All workplaces in both public and private sectors and from all sizes, economic sectors and categories as shown in the Application Form are encouraged to participate. If your workplace has planned or implemented any innovative idea or program which contributed in the promotion of safety and health at your workplace you are encouraged to apply. All applications selected for the awards will be visited for verifications. Safety and health information to be verified are shown in the Application Form.

**Rules for Participation**
i) Download the Application Form from the website www.osha.go.tz, or collect it from the nearest OSHA office.
ii) Complete the Form Field in Permanent Ink or Electronically. Note that incomplete Forms may not be considered.
iii) Applicant should pay entry fee of TZS 50,000/= non-refundable, Payments will be done electronically through GePG. Please visit the nearest OSHA office or contact through email or phone to get your Control Number (**zakaria.sumuni@osha.go.tz,** 0754789752, 0715914628).
iv) Print Application Form and have it signed by the authorized person, complete with Company Stamp. The completed Application Form must be submitted by 6th March 2020, 15:30 HRS. Do not attach any document during submission except for proof of payment.
v) The Form may be submitted in any of the following ways:-
   (a) To the Chief Executive, OSHA, P.O Box 519 Dar es Salaam; or submit the hard copy to the nearest OSHA Offices located in Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Arusha, Mbeya, Mtwara, Tanga, Njombe, Morogoro and Bukoba
   (b) Email to: **info@osha.go.tz** or, **zakaria.sumuni@osha.go.tz**
vi) Competitors for AOSH must participate on the Exhibition to show their competency
vii) All participants and winners of Awards are invited to attend the award giving ceremony to be held on the **28th April 2020** in Mwanza Region, and they may be asked to be available for media interviews or other publicity.
viii) All written information will be verified by the Award Team. Participants are subject to OSH audits including site audit.

215630002

# Fidia inavyouweka njia panda uchimbaji wa graphite Ulanga

## ■Waziri: Kuwajibikia jamii lazima
## ■Mwekezaji: Shule, zahanati... zaja

Na Salome Kitomari

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, ilieleza mkanganyiko uliojitokeza katika vipengele vinavyowezesha mradi wa kuwekeza kwenye uchimbaji wa madini ya graphite, ukikwamishwa na kutotekelezwa kwa mahitaji muhimu ya kisheria, ikiwamo fidia. Fuatilia sehemu ya mwisho, inayojumuisha ufafanuzi kutoka kwa wahusika wakuu:**

.........................................................................

Maria Mwenti, Diwani wa Uponela, anasema katika eneo lake kuna vijiji viwili, kimoja kikiitwa Lyandu ambacho kilibainika kuwa na madini hayo katika utafiti uliofanyika miaka minne iliyopita.

"Wametueleza kuwa kuna madini mengi ambayo mchakato wa kuyatoa umeanza, ila bado hatujaelewa maana kitongoji ambako madini yamegundulika ndiko kwenye miundombinu yote ya zahanati, shule na kanisa.

"Vitongoji vingine vimetawanyika sana na wakisema huduma hizo waziondoe ziende kwingine, watakuwa wamevuruga mpangilio wetu, hadi sasa hatujui mikataba ikoje zaidi ya kuelezwa kuwa wana leseni na mikataba yote muhimu.

"Tunachotarajia ni kuwa kampuni itakayowekeza, ilete mabadiliko makubwa kwenye kata yetu ili tuone manufaa na siyo utajiri utoke ardhini halafu sisi tuendelee kuwa maskini na tukose huduma muhimu.

"Tunatamani kuona tunajengewe shule, zahanati na kituo cha afya cha kata. Tunaona wanaendelea na kazi zao za tathmini, lakini hatushirikishwi kujua kinachoendelea, mimi kama mwakilishi wa wananchi nilitarajia nishirikishwe," analalamika.

Neema Lyafwila, mkazi wa eneo hilo, anasema kwa muda ambao wameishi bila kupata fidia, wameshindwa kufanya shughuli za maendeleo.

### UFAFANUZI KISHERIA

Wakili wa Kijitegemea, Harold Sugusia, anasema kuna sheria tatu ambazo zinagusa na suala hilo ambazo ni Sheria ya Ardhi, Sheria ya Madini na Sheria ya Uwekezaji.

Anasema Sheria ya Ardhi inasema ikitokea kuna mgongano wa kisheria katika masuala ya ardhi, sheria hiyo (Sheria ya Ardhi) ndiyo itatawala na kama kuna hizo sheria nyingine, kitakachopaswa kuangaliwa ni utaratibu wa Sheria ya Ardhi kuhusu fidia.

"Inasema kama mtu alikuwa anamimili eneo lake, likachukuliwa kwa faida ya umma, atalipwa kwa bei ya soko, kama walifanywa tathmini na ikafanywa na mtaalamu wa tathmini na ripoti ikitoka, ndiyo watu wajipange kwa ajili ya kulipwa fidia," anasema.

Kwa mujibu wa Wakili Sugusia, madini yote yaliyo chini ya ardhi ni mali ya serikali na wananchi wanapaswa kulipwa fidia kabla ya kuanza uchimbaji.

Anasema kama tathmini ya awali ilifanyika muda mrefu na bei ya soko na hali ya maisha imebadilika, inabidi kuangalia kama ardhi imeongezeka thamani kwa kiwango gani, ili muda ukiisha walipwe kwa bei ya soko kwa wakati wanaondoka.

### KAULI YA TRANS GRAPHITE

Meneja Uhusiano wa Jamii wa Kampuni ya Tans Graphite, Benard Mihayo, anasema vitongoji vitatu kati ya sita katika Kijiji cha Epanko ndiyo vitahamishwa na kwamba huduma zote muhimu za kijamii zitawekwa.

Anasema walipata leseni mwaka 2015, lakini wameshindwa kuanza kazi kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Madini, ambayo yalilazimu kampuni kujipanga upya na kuna mambo wanajadiliana na serikali kabla ya kuanza uchimbaji.

"Tumeunda kamati tisa ambazo zimewakilisha makundi yote kwenye jamii, hadi sasa asilimia 82 ya wananchi wamekubali kulipwa fidia ambayo itaanza kulipwa baada ya kampuni kukubaliana na serikali," anasema.

Mihayo anaendelea kueleza kuwa mwekezaji huyo anatarajia kuwekeza zaidi ya Sh. bilioni 3.7 na kati yake Sh. bilioni mbili ni za ujenzi wa nyumba za kisasa za wananchi hao.

"Tumetengeneza mpango wa maendeleo wa miaka miwili baada ya kuwajengea wananchi nyumba za kisasa katika eneo tutakalowahamishia, tutawapa mbolea na pembejeo zote muhimu kwa ajili ya kuboresha ardhi mpya watakayokwenda kuitumia," anaahidi.

Anasema kwa mujibu wa sheria, walipaswa baada ya kutangaza kulipa fidia, kufanya hivyo lakini ikipita miezi sita bila kulipa, watatakiwa kulipa pamoja na faini ya asilimia sita. Anasema walipanga kuanzia Januari mwaka jana, kujenga nyumba 350 kwa ajili ya wananchi wanaohama kupisha mradi. Kwa upande wa huduma za kijamii, anasema wamepanga kujenga Shule ya Msingi Epanko yenye madarasa 14 ikiwamo darasa la awali ambayo itabeba wanafunzi 332.

Pia anasema watajenga zahanati ya kisasa, kituo cha afya na nyumba tatu za madaktari, ofisi za kijiji na miundombinu ya barabara ya kuingia na kutoka kwenye eneo la mradi.

Anabainisha kuwa leseni waliyopewa ni ya miaka 12 na wanaruhusiwa kuihuisha na kwamba watakuwa wanalipa mrabaha wa asilimia 0.3 kwa halmashauri.

### WAZIRI ANENA

Hivi karibuni akizungumza na wananchi wa Mahenge, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alizitaka kampuni zote zinazowekeza kwenye sekta ya madini, kutekeleza ahadi ya uwekezaji kwenye huduma za jamii kama walivyoahidi wakati wanaomba leseni.

"Niwatoe wasiwasi wananchi kuwa hakuna mtu hata mmoja atakayekuja Tanzania kuchimba madini, aondoke na kuwaacha wananchi wanashangaa, zama hizo zilipendwa.

"Wawekezaji wote watakaokuja, watachimba na madini watakayoyapata faida yake lazima irudi Tanzania," alisisitiza.

Waziri Biteko pia alisema soko la madini ambalo limeanzishwa Aprili mwaka jana Ulanga, limewezesha serikali kupata mapato, akibainisha kuwa hadi sasa, fedha iliyopatikana kutokana na mauzo ya madini hayo ni Sh. milioni 396 wakati kwa miaka mitano iliyopita walipata Sh. milioni nne tu.



Waziri wa Madini, Doto Biteko.

Alisema matarajio ya wizara yake ni mapato kuongezeka zaidi pale wawekezaji hao watapoanza kazi rasmi.

Akizungumzia Kampuni ya Mahenge Resources, Waziri Biteko alisema: "Uwekezaji wao ni wa Dola za Marekani milioni 23 zitakazojenga mgodi huo wa Mahenge Resources. Kikwazo walichonacho ni fidia kwa wananchi, tayari tumeshawaelekeza waikamilishe haraka kabla ya uwekezaji, wameomba katika mchakato huu timu ya uthamini iwe na wawakilishi.

"Tayari nimemwelekeza Mkuu wa Wilaya wa hapa, wawe na wawakilishi wa kijiji kwenye timu hiyo ili baadaye kusitokee malalamiko."

Waziri Biteko alisema kampuni hiyo imeshapewa sampuli mbalimbali za madini hayo ambazo walizipeleka katika maabara tofauti na wamejiridhisha, kinywe ya Tanzania ni bora kuliko zinazopatikana maeneo mengine duniani.

### GRAPHITE NI NINI?

Mtaalamu wa miamba kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Hudson Nkotagu, anasema madini ya graphite kwa Kiswahili yanafahamika kama grafiti na yanapatikana katika ukanda ambao kitaalamu wanauita 'Mozambican Belt', unaotokea Ethiopia na kupitia katika nchi za Afrika Mashariki hadi Msumbiji.

"Mara nyingi ukanda huo una miamba yenye umri wa zaidi ya miaka bilioni 1.2 'metamophic', ambazo zina joto la chini, kati na juu sana.

"Miamba ambayo imetengenezwa kwenye joto la chini ndiyo inaweza kuwa na hiyo miamba yenye madini ya graphite ambayo ni kama viumbe hao kama mimea ambayo hupikwa kwenye joto la chini na kutengeneza madini hayo," anasema.

Anaeleza kuwa madini hayo kwa Tanzania yako Mirerani mkoani Arusha, Mahenge mkoani Morogoro na Ngachu mkoani Lindi, ambako wanakuita Ukanda wa Usagarani.

Prof. Nkotagu anasema graphite ni madini yenye nguvu kwa kiwango kikubwa kupita malighafi nyingine yoyote duniani, yakifananishwa na chuma cha pua mara 200.

"Hiyo sifa inayafanya yaweze kutumika kwenye vitu vingi kama kutengeneza madaraja, bodi za ndege, gari, kofia za pikipiki na vitu vingine vigumu vigumu. Pia yanaweza kuvutika sana kwa asilimia 20 hadi 25 ya urefu wake," anafafanua.

Anaongeza kuwa sifa nyingine ni membamba na kwamba ukichukua gramu moja, unaweza kufunika uwanja wa mipira wa miguu (kapeti, na ni mepesi kuliko unywea wa kuku.

Anasema madini hayo yana uwezo wa kusafirisha joto kuliko vitu vingi duniani, yanasafirisha umeme kuliko hata nyaya za kopa na ndiyo maana kwenye kila kinu, kuna kidogo kimewekwa ili umeme uweze kupita kwa haraka.

"Ndiyo maana wanatumia kwenye ndege, ndege inahitaji vitu kama hivyo kwa kuwa vinaweza kupitisha umeme kwa haraka sana," anafafanua.

Anaongeza kuwa graphite inaweza kuchuja maji na kuondoa madini mengine yote na ina uwezo wa kuyachuja maji ya bahari yakawa maji ya kunywa.

"Madini hayo yanatengeneza betri za magari na magari aina ya Voxwagon na Mercedes Benz na BMW wanataka miaka 2020/25 asilimia 25 ya magari wanayotengeneza duniani, yawe ya umeme wa kutumia graphite," anasema.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanaisukuma dunia kusaka mbinu za kupunguza hewa ukaa, yatayasukuma mataifa mengi kunaanza kutengeneza magari ya umeme na graphite itahusika kwa kiasi kikubwa kupitisha na kuhifadhi umeme kwa muda mrefu.

Anajata sifa nyingine kuwa ni kutumika kutengenezea breki za magari, kwenye chuma cha pua, kutumika viwandani kwa ajili ya vilainishi mbalimbali na kwamba ina soko kubwa duniani.

### GRAPHITE YA TANZANIA

Profesa Nkotagu anasema nchi inayoongoza kwa kuwa na grafiti nyingi ni Uturuki ambayo mwaka 2017 ilikuwa na Metric tani milioni 90, ikifuatwa na Brazil yenye ikiwa na Metric tani milioni 70, China tani milioni 55 huku Tanzania na Msumbiji zikiwa na tani milioni 17.

"Grafiti ya Tanzania ni asili na yenye ubora kwa asilimia 99, katika kuchakata, uchafu ni kidogo, Ukilinganisha na wengine, ya Tanzania ni namba moja kwa kuwa ina ubora wa hali ya juu," anasema.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, nchi za Marekani na China ndiyo wanunuzi wakubwa kutokana na utengenezaji wa ndege.

# Iddi Simba afariki, kuzikwa leo Kisutu

**Na Mwandishi Wetu**

MWANASIASA mkongwe na Waziri wa zamani wa Viwanda na Biashara, Iddi Simba, amefariki dunia. Taarifa iliyosambaa jana katika mitandao ya habari na kuthibitishwa na mtoto wake, Ahmad Simba, ilisema Simba alifariki dunia katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, alikokuwa akipatiwa matibabu.

Ahmad alikaririwa akisema familia, ndugu, jamaa na marafiki walikuwa wanakusanyika nyumbani kwa marehemu kwa ajili ya kupanga mipango ya maziko yake.

Hata hivyo, taarifa zilizopatikana jana jioni zilisema mwanasiasa huyo atazikwa leo katika makaburi ya Kisutu, Dar es Salaam, baada ya Sala ya Ijumaa.

Iddi Simba, ambaye alizaliwa Oktoba 8, 1935 alipata elimu yake katika vyuo vikuu vya Punjab, Pakistan na Toulouse, Ufaransa, licha ya kuwa mwanasiasa, alianza kazi katika utumishi wa umma na baadaye taasisi za fedha za kimataifa.

Alianza utumishi wa umma akiwa Mkurugenzi wa Mipango Msaidizi katika iliyokuwa Wizara ya Uchumi na Mipango na baadaye aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji Mbadala wa Benki ya Dunia mwaka 1966 hadi 1968.

Baada ya hapo aliteuliwa kuwa Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki nafasi aliyoishika kwa miaka 10 hadi mwaka 1978. Mwaka 1978 hadi 1980 alikuwa Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Kutokana na kustaafu utumishi katika taasisi hizo, Iddi Simba alijikita kwenye biashara hadi kifo chake, lakini alishika nyadhifa mbalimbali za kisiasa.

Miongoni mwa nyadhifa hizo ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM kuanzia mwaka 1996 hadi 1999 na kwa nafasi hiyo akawa mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na Mjumbe wa Halmashauri Kuu (NEC). Sambamba na nafasi hizo, aliwahi kuwa Mbunge wa Ilala kuanzia mwaka 1995 hadi 2015 na Waziri wa Viwanda na Biashara mwaka 2000 hadi 2002 alipojiuzulu kutokana na kashfa ya vibali vya uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi.

## Balozi wa Iran avifunda vyombo vya habari

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa Iran nchini Tanzania, Mousa Farhang, ameviitaka vyombo vya habari kuacha kutegemea habari za vyombo vya magharibi kwa kuwa hazina maslahi kwa nchi za Afrika na zile zinazoendelea.

Amesema vyombo hivyo vya muda mwingi vimekuwa vikiandika mambo mabaya tu kwa nchi zinazoendelea kwa maslahi yake hatua ambayo imesababisha vyombo vingi vinavyotegemea taarifa hizo kuiga mkumbo na kuandika mambo mabaya yakiwamo ya nchi zao.

"Vyombo vya habari vya kimagharibi vimekuwa vikieleza mabaya tu ya nchi zingine. Hivi kuna uwezekano wa kuwa na 'nguo chafu tu bila kuwa na hata nguo moja safi?" Alihoji Balozi Farhang jana alizungumza na menejimenti ya kampuni ya The Guardian Limited, jijini Dar es Salaam wakati wa ziara yake.

Balozi huyo alisisitiza kuwa vyombo vya habari nchini havina budi kutambua kuwa wajibu wao ni mkubwa kwa maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, hivyo vinapaswa kuwa makini na propaganda za nje zinazoweza kurudisha nyuma maendeleo ya nchi.

Alisema vyombo vya nchi hizo vinaweza kuandika habari zenye mlengo wa chuki dhidi ya kiongozi fulani wa nchi fulani lakini vimekuwa vikichukulia jambo hilo kwa mtazamo wa kitaifa na si mtu binafsi.

"Kwa mfano unaweza kuwa humpendi (Rais John) na si nchi kwa ujumla lakini inakuwaje uadui wako na Magufuli ukawa ni wako na Tanzania nzima? Hili si sahihi na vyombo vya habari vinapaswa kuwa makini," alisema.

Sambamba na hilo, Balozi Farhang alivionya vyombo vya habari kuhusu kasumba ya kuchapisha picha na taarifa kuhusu misaada inayotolewa na taasisi mbalimbali kwa jamii zenye uhitaji. Alisema hatua hiyo pia inadhalilisha jamii inayopatiwa misaada hiyo.








TASAF
TANZANIA SOCIAL ACTION FUND
MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII

KIPINDI CHA PILI CHA AWAMU YA TATU

**UTANGULIZI**

Kipindi cha Kwanza cha Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF kilitekelezwa kuanzia 2012 na kukamilika Desemba 2019. Utekelezaji ulifanyika katika halmashauri 159 za Tanzania bara, Unguja na Pemba na kufikia kaya milioni1.1 zenye zaidi ya watu milioni 5.

Tathmini ya utekelezaji wa sehemu ya kwanza inaonyesha kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Mpango huu umefanikisha azma ya serikali ya kupunguza umaskini nchini. Takwimu zinaonesha kwamba umaskini wa mahitaji ya msingi umepungua kwa asilimia 10 na umaskini uliokithiri umepungua kwa asilimia 12 kwa kaya maskini.

Utekelezaji umewezesha walengwa kujikita kwenye ufugaji, uvuvi, kilimo na biashara na kujiimarisha kiuchumi. Vile vile Mpango umeongeza idadi ya watoto kutoka katika kaya maskini kuandikishwa shule kwa kiwango cha asilimia 7.2. katika sekta ya afya, Mpango umeongeza mahudhurio ya kliniki kwa watoto walio na umri chini ya miaka 5 kwa kiwango cha asilimia 1.5

Kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

Kipindi cha Pili kinatekelezwa katika halmashauri 185 za Tanzania bara, Unguja na Pemba katika vijiji/mitaa/shehia zote ikiwa ni pamoja na Vijiji/Mitaa/Shehia zaidi ya 5,000 ambavyo hazikufikiwa katika utekelezaji wa kipindi cha Kwanza. Kipindi cha Pili cha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kitafikia kaya milioni 1.4 zenye watu wapatao milioni 6 kote nchini.

Madhumuni ya Kipindi cha Pili cha TASAF ni kuwezesha kaya zilizoandikishwa kutumia fursa za kuongeza kipato, huduma za kiuchumi na kijamii na kuendeleza rasilimali watu husussan watoto.

Taarifa ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2011/2012 inaonesha asilimia 28.2 ya watanzania wanaishi katika umaskini huku asilimia 9.7 wanaishi katika umaskini uliokithiri hivyo utekelezaji wa Kipindi cha Pili utawezesha kaya maskini kujikwamua kutoka kwenye umaskini na kufanya kazi na kujiimarisha kiuchumi na kuiwezesha nchi kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025

Utekelezaji wa Kipindi cha Pili cha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

Shughuli kuu zitakazofanyika ni kutoa fursa ya ajira za muda kwa kaya maskini zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi kushiriki katika shughuli za uzalishaji na kuboresha miundombinu ya barabara za vijijini, elimu, afya, maji na hifadhi ya mazingira. Kuhamasisha walengwa kujiunga katika vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza katika shughuli za uzalishaji mali na kutoa ruzuku kwa masharti ya elimu na afya kama kichocheo cha mahudhurio ya watoto shuleni na kliniki ili kupata elimu na huduma za afya na hivyo kuwajengea maisha bora. Aidha wadau katika ngazi mbali mbali watajengewa uwezo kwa njia ya mafunzo ambayo yatawawezesha kutekeleza na kutimiza majukumu yao kwa ufanisi.

**Matarajio**

Matarajio ya Serikali kupitia utekelezaji wa TASAF ni kupunguza kiwango cha umaskini kwa kutoa fursa kwa walengwa kushiriki kwenye kazi za kilimo na uzalishaji na hivyo kuchochea ukuaji wa viwanda, kuboresha miundombinu ya elimu afya hivyo kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto na kuongeza kiwango cha wanafunzi wanaomaliza darasa la saba na kupitia miradi ya kuongeza kipato kaya maskini ziweze kuboresha lishe kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, na kupunguza udumavu na utapiamlo kwa watoto.

*Kipindi cha Pili cha Awamu ya III ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kitazinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.*

*Kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam, tarehe 17/02/2020*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kamati za maadili maofisa mahakama zinahitaji bajeti

**SERIKALI** imeombwa kutenga fedha kwa ajili ya kamati za Maadili za Maofisa wa Mahakama za Mikoa na Wilaya ili ziweze kutekeleza majukumu yake kama sheria inavyozitaka.

Ombi hilo lilitolewa na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, kwa ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), kwa ajili ya kuwawezesha maofisa hao kutekeleza wajibu wao kama inavyotakiwa.

Kamati za Maadili za Maofisa wa Mahakama zimekuwa zikikabiliwa na changamoto ya kutotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kutokana na upungufu wa bajeti.

Kamati hizi ziliundwa baada ya kutungwa kwa sheria ya Usimamizi wa Mahakama namba 4 ya mwaka 2011, na sheria hiyo pia inazitaka mahakama hizo kukutana na kuwasilisha taarifa zake kwa Tume ya Utumishi wa Mahakama.

Waziri Mahiga alitoa ombi hilo alipokuwa akizindua mwongozo wa uendeshaji wa kamati za maadili za maofisa wa Mahakama juzi jijini Dodoma, na kusema wizara yake itahakikisha Tume ya Utumishi wa Mahakama inapatiwa rasilimali fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli zake ikiwamo Kamati za Maadili za Maofisa wa Mahakama kwa ufanisi unaotakiwa.

Chombo hiki kina umuhimu mkubwa kwa muhimili huo katika utekelezaji wa majukumu yake ya kutoa haki. Ikumbukwe kuwa suala la maadili lina umuhimu wa pekee kwa watumishi wa Mahakama.

Kazi ya kutoa haki inahitaji watu wenye maadili, uaminifu, weledi na uadilifu wa hali ya juu, hivyo wajumbe wa kamati na maofisa wa mahakama hawanabudi kutekeleza majukumu yao katika mazingira bora, wezeshi na rafiki.

Ili waweze kutekeleza wajibu wao inavyotakiwa, hawanabudi kuwezeshwa kwa bajeti, ambayo inahusisha fedha na vifaa.

Kama inafikia hatua Waziri mwenye dhamana ya Katiba na Sheria kulitolea jambo hilo kilio kuwezeshwa kwa bajeti, ina maana kuwa shughuli za chombo hicho hazitekelezwi inavyopaswa kama sheria na kanuni zilizokianzisha zinavyoelekeza.

Kutokana na umuhimu wa kuimarisha dhana ya utawala bora kupitia sheria ya uendeshaji wa Mahakama, ndio maana Serikali iliamua kuruhusu uwapo wa kamati za maadili za maofisa wa Mahakama ambazo ni ya Maadili ya Majaji, Kamati ya Maadili ya Maofisa wa Mahakama na Kamati ya Maadili ya Mahakama ya Mkoa na Wilaya.

Kutokana na umuhimu huo, ndio maana Waziri Mahiga anasema kuwa kamati hizi zina nafasi kubwa katika kusimamia, kuendeleza na kudumisha maadili ya utumishi wa mahakama.


Tunaona kuwa umuhimu wa kamati hizi haunabudi kuishawishi serikali kupitia Tamisemi kutenga bajeti kwa ajili hiyo ili majukumu yao yatekelezwa kama sheria inavyotaka.

Kwa kufanya hivyo, bila shaka majukumu hayo yatatekelezwa kama inavyotakiwa, na ni imani yetu kuwa hatua hiyo itasaidia kuwakumbusha watumishi wote kuzingatia maadili.

Aidha, hatua hiyo itawafanya watumishi wachache wanaoendelea na vitendo vya ukiukaji wa maadili kuacha mara moja ili kulinda heshima ya mhimili wa Mahakama kwa jamii sambamba na usalama wa ajira zao.

Tunakubaliana kabisa na kauli ya wakuu wa mikoa nchini ambao ni walezi wa kamati hizo kupitia kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, kuwa palipo na maadili pana amani, haki, uaminifu katika utendaji kazi, umoja na ushirikiano, na kwamba kuwapo kwa maadili pia ni ni kichocheo cha maendeleo ya Taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Nidhamu ya bodaboda ikichekewa, tutalia sana

**UKIPITA** katika barabara zinazotumiwa na mabasi ya mwendokasi, utaona kila penye kivuko, kuna tangazo ambalo haziruhusu bodaboda kupita wakiwa wamebeba abiria.

Pamoja na kuandikwa kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza, bado madereva wa bodaboda wanapita wakiwa wamebeba abiria.

Hapo katika mustakabali wa usalama barabarani, inazua maswali nini sasa kifanyike? Iko wazi kinachotakiwa hapo ni hatua madhubuti. Zipi? Pale usafiri wa bodaboda unapopita katika maeneo hayo, mara moja kinachotakiwa ni mamlaka za dola kuchukua hatua zinazoleta mabadiliko.

Panapaswa kuhakikishwa abiria waliopo wanashushwa, pia dereva wa bodaboda anatakiwa kushuka katika chombo chake, anakisukuma na baada ya hapo anaruhusiwa kupanda chombo kuendelea na safari yake.

Ninashuhudia pamoja na katazo hilo, bado watumiaji vyombo hivyo wanaendeleza tabia. Madereva wa bodaboda wamekuwa wakikiuka taratibu na kuamua kupita katika njia hizo, huku wakiwa wamepanda bodaboda zao. Niseme ni ukiukwaji mkubwa.

Walioamua kuweka utaratibu huo walikuwa na busara kubwa kuhusiana na usalama barabarani. Waliona mazingira ya kiashiria cha ajali inayoweza kuleta maafa kwao na umma kwa jumla, watu wakapata ulemavu wa namna mbalimbali.

Bodaboda mara nyingi zimekuwa zikikiuka sheria za usalama barabarani na kusababisha watu kupoteza maisha au kupoteza viungo.

Hiyo yote inatokana na madereva wa bodaboda kutokuwa makini na kazi wanazozifanya? Madereva hao wanajua sheria inawataka wabebe abiria mmoja, lakini haohao wako mstari wa mbele kukiuka sheria, wanabeba abiria zaidi ya mmoja.

**Tumekuwa tukishuhudia uendeshaji mbaya wa bodaboda unaofanywa na baadhi ya madereva wa vyombo hivyo. Imefika hatua, kwamba madereva hao wanaoendesha kwa kasi bila ya kujali chochote mbele yao na kuzua hatari, ikiwamo na maisha ya abiria wao, wachukue hatua.**

Pia, dereva wa bodaboda kawaida ya kubeba abiria zaidi ya mmoja na mara nyingi, hata uendeshaji wao si ulio salama hata kidogo. Kuna viashiria vingi.

Tukumbuke, hivi sasa katika barabara kama za jiji la Dar es Salaam, kuna magari ya mwendokasi zinapokutana na zuio la aina yoyote isiyo ya kawaida, ni wazi kuna ishara zaidi na kunapokuwapo zuio lolote, lazima jamii isifanye ukaidi. Ajali inaweza kutokea muda wowote.

Abiria nao mnaopanda bodaboda mkapita katika alama ya 'zebra' ni wajibu wenu kidereva mjiandae kushuka ili mkivuka upande wa pili, muendelee na safari zenu.

Pia, abiria kama hiyo sheria ya kushuka katika zebra za mwendokasi unaijua, ni muhimu usiipuuzie hata kidogo, kwa sababu walioweka wana maana kubwa katika usalama.

Tumekuwa tukishuhudia uendeshaji mbaya wa bodaboda unaofanywa na baadhi ya madereva wa vyombo hivyo. Imefika hatua, kwamba madereva hao wanaoendesha kwa kasi bila ya kujali chochote mbele yao na kuzua hatari, ikiwamo na maisha ya abiria wao, wachukue hatua.

Ni hao hao bodaboda wanapoona foleni kubwa, hawajali chochote na wanajichomeka katikati ya magari, bila ya kujali kinachoweza kutokea mahali hapo

Niwakumbushe abiria wezangu, iwapo mtaendelea kuwachekea bodaboda na kuwafumbia macho, mjue chochote kinaweza kuwapata na msilaumu pale mtakapopata ulemavu.

# HABARI PICHANI



Balozi wa Iran nchini, Mousa Farhang (kushoto), akizungumza na Meneja Mkuu wa Kampuni ya The Guardian Ltd, Srinivas Chintaruri (kulia), Mhariri Mtendaji wa Nipashe, Beatrice Bandawe na Mhariri Msaidizi, Epson Luhwago, alipotembelea chumba cha habari cha kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam jana.



Balozi wa Iran Mousa Farhang (kulia), akikabidhi zawadi ya kumbukumbu kwa Meneja Mkuu, Srinivas Chintaruri, baada ya mazungumzo.

**PICHA ZOTE: SELEMANI MPOCHI**



Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, akifafanua kuhusu utendaji kazi wa chumba cha habari kwa Balozi wa Iran nchini, Mousa Farhang (kushoto) na ujumbe wake.



Balozi wa Iran, nchini, Mousa Farhang (kushoto), akitembelea chumba cha habari. Kulia ni Meneja Mkuu, Srinivas Chintaruri.



Balozi Farhang akiangalia baadhi ya machapisho ya matangazo alipotembelea kiwanda cha uchapishaji cha The Guardian Ltd.



Mhariri Mtendaji wa Nipashe, Beatrice Bandawe (kushoto) na Meneja Raslimali Watu wa TGL, Emmanuel Matondo, wakijadiliana jambo na Balozi Farhang.

# Lukuvi kutekeleza agizo la Rais JPM Jumatatu

**Na Munir Shemweta,**
DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, anatarajiwa kwenda katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni Jumatatu kurudisha umiliki wa ekari 750 kwa manispaa hiyo kama ilivyoelekezwa na Rais.

Jumanne, Rais John Magufuli alitoa siku saba kuanzia siku hiyo kwa Wizara ya Ardhi kurejesha umiliki wa eneo hilo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kigamboni baada ya kufutwa miaka iliyopita ili umiliki wake kuwa chini ya serikali kupitia wizara hiyo.

Akizungumza kwa njia ya mtandao jana akiwa Abu Dhabi, Falme za Kiarabu anakohudhuria kikao cha mawaziri wa Afrika kuhusu masuala ya nyumba na maendeleo ya miji, Lukuvi alisema Jumatatu atakuwa kwenye Ofisi za Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwa ajili ya utekelezaji wa agizo hilo la Rais.

"Jumatatu tarehe 17 Februari, saa tano asubuhi, nitakuwa Ofisi za Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni kwa ajili ya kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kukabidhi ardhi ambayo iko katika eneo la Kigamboni," aliahidi.

Kwa mujibu wa Rais Magufuli, pamoja na kufuta umiliki wa eneo hilo ili kuwa chini ya serikali, umiliki wake kwa muda mrefu haujarerejeshwa katika Manispaa ya Kigamboni na kutaka miliki hiyo kurejeshwa ndani ya wiki moja ili wananchi wapange wanavyotaka.

Hata hivyo, Rais Magufuli alionya kuhusu matumizi ya ardhi hiyo kwa halmashauri hiyo, akitahadharisha kuwa isije ikatumika vibaya kwa kuwa si ya viongozi, bali ni kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Kigamboni.



Maofisa Washiriki kutoka Chuo cha Ulinzi wa Taifa cha Tanzania, wakikata kiu kwa maji ya madafu wakiwa katika ziara yao ya mafunzo, katika Jeshi la Magereza, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JESHI LA MAGEREZA**

# Rugemalira aibua mengine kortini

**INATOKA UK. 2**

wa Sh. bilioni 1.5.

Alidai ameandika barua ya nyongeza na kuikabidhi Takukuru ili watakapotoa majibu watoe kwa usahihi.

Kadhalika alidai Februari 11, mwaka huu, alitoa notisi inayoelezea matatizo hayo yalivyokuwa na kwamba kuna vipengele vya sheria havitekelezwi katika notisi hiyo na kwamba wasipomwondolea mashtaka yanayomkabili dhidi ya kesi hiyo, hawataweza kukamilisha upelelezi na filimbi alizopiga zitasaidia kukamata wezi waliohusika.

Mshtakiwa huyo aliomba kukutana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, kabla ya kwenda mahabusu kwa ajili ya kumpa ufafanuzi kuhusu kesi hiyo na kwamba kama hawatamtoa katika kesi hiyo ataleta maombi maalum ya kutaka kuondolewa kwenye kesi hiyo.

Baada ya kusikiliza maelezo hayo, Hakimu Shaidi alisema, itatajwa Februari 27, mwaka huu.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Harbinder Sethi na Joseph Makandege.

Katika kesi ya msingi, Makandege anakabiliwa na mashtaka matano likiwamo la kusababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 980,000 pia yapo ya utakatishaji wa fedha.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka hayo Desemba 20, 2019, baada ya kuunganishwa na washtakiwa Seth na Rugemalira.

Makandege anadaiwa kuwa, kati ya Oktoba 18, 2011 na Machi 19, 2014 katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, Kenya, Afrika Kusini na India, akiwa na wenzake walikula njama ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Pia anadaiwa kuongoza genge la uhalifu katika nchi hizo akiwa si mtumishi wa serikali akishirikiana na watumishi wa umma kwa kuratibu na kufadhili mpango wa uhalifu.

Katika shtaka la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, Makandege anadaiwa kuwa kati ya Januari 23, 2014 na Februari 2014, alijipatia Dola 380,000 katika Benki ya Stanbic iliyopo Kinondoni na Dola 600,000 katika benki ya UBL (T) Ltd iliyopo Wilaya ya Ilala, fedha zilizotoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa nyakati tofauti.

Kwa upande wa washtakiwa Sethi na Rugemalira walifikishwa mahakamani hapo zaidi ya miaka miwili wamekaa rumande, kutokana na upelelezi wa kesi yao kutokukamilika.

Washtakiwa Sethi na Rugemalira kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 12 yakiwamo ya utakatishaji fedha na kusababisha hasara ya Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh. 309,461,300,158.27 kwa mara ya kwanza walifikishwa mahakamani hapo Juni 19, 2017.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa Oktoba 18, 2011 na Machi 19, 2014 jijini Dar es Salaam walikula njama katika nchi za Afrika Kusini, Kenya na India ili kutenda kosa.

Ilidaiwa katika mashtaka ya kujipatia fedha kwamba kati ya Novemba 28 na 29, 2011 na Januari 23, 2014 katika Makao Makuu ya Benki ya Stanbic, Kinondoni na Benki ya Mkombozi tawi la Mtakatifu Joseph, kwa ulaghai washtakiwa hao walijipatia kutoka Benki Kuu ya Tanzania, Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh. 309, 461,300,158.27.

Pia washtakiwa wote wanadaiwa kuisababishia serikali hasara na inadaiwa walitenda makosa hayo Novemba 29, 2013 katika Benki ya Stanbic tawi la kati Kinondoni, kwa vitendo vyao waliisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh. 309,461,300,158.27.

Kati ya Novemba 29, 2013 na Januari 23, 2014 maeneo tofauti Dar es Salaam kwa pamoja walitenda kosa la kutakatisha fedha kwa kuchukua fedha kutoka BoT ambazo ni Dola za Marekani milioni 22.1 na Sh. bilioni 309.4, wakati wakijua fedha hizo ni zao la kujihusisha na genge la uhalifu.

## Maambukizi homa ya ini tishio

**Na Mary Geofrey**

ASILIMIA 40 ya watu 2,000 waliofanyiwa utafiti wa kubaini iwapo wameathirika na maambukizi ya Virusi vya Homa ya Ini (Hepatitis B), wana maambukizi hayo na wapo katika hatari ya kupata saratani ya ini.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Mfumo wa Chakula na Ini kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. John Rwegasha, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza kwenye kongamano lililokutanisha wataalamu wa afya kujadili maendeleo ya mradi wa tiba ya virusi vya homa ya ini ulianzishwa na MNH miaka minne iliyopita.

Alisema kati ya waliobainika kuwa na virusi vya homa ya ini asilimia 90 wanapata maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Alisema mradi huo unatarajiwa kukamilika mwakani na kwamba lengo lake ni kubaini kiwango cha maambukizi ya ugonjwa huo ulioenea kwa kasi nchini kutokana na kukosa tiba pamoja na vitendanishi kwa ajili ya uchunguzi.

Dk. Rwegasha alisema mradi huo ambao umefadhiliwa na Marekani, una vifaa vya kufanya vipimo na umefanikiwa kwa kiasi kikubwa baada ya kuwafanyia tathmini watu 2,000.

"Tumegundua kuna walioathirika kati yao wana tatizo la ini kusinyaa na wengine wameweza kuwa na saratani ya ini," alisema Dk. Rwegasha.

Alisema wanaopata maambukizi hayo ni kuanzia umri wa miaka 30 hadi 40 na kwamba ukiwa na maambukizi huweza kukaa mwilini kwa zaidi ya miaka 20 kabla ya dalili.

"Kulikuwa na mwitikio zaidi hasa Dar es Salaam na nchi nzima. Asilimia 80 ya watu tuliofanyiwa tathmini wamegundulika wana uwezo wa kujitibu wenyewe kupitia kinga yao," alieleza Dk. Rwegasha.

Alieleza kuwa kati watu 1,400 sawa na asilimia 80 wenye maambukizi, wamejitengenezea kwa kinga yao na kwamba jamii itambue homa ya ini ni ugonjwa ambao miili ya binadamu, ina uwezo wa kudhibiti kwa kinga ya asilimia 95.

Alisema changamoto iliyopo baada ya watu kugundua wana maambukizi hawakurudi kwa daktari kwa ajili ya tiba na ushauri na kwamba hiyo inahatarisha afya zao kwa kuwa wanaweza kupata magonjwa nyemelezi.

"Hawa asilimia 20 wanaweza kupata maambukizi, wanatakiwa kufanyiwa uchunguzi kila mwaka, mwitikio ni mdogo kwa kuwa mradi unaisha mwaka kesho bado tunahitaji watu kuchunguzwa na kutoa chanjo kwa wanaozaliwa," alieleza.

HABARI KITAIFA

# Ndalichako aomba wawekezaji elimu

**Na Enock Charles**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, amewaomba wawekezaji na wadau katika sekta ya elimu nchini, kuwekeza katika Mkoa wa Dodoma kwa kuwa ndiko yaliko makao makuu ya nchi na kuna uhitaji mkubwa wa shule mkoa humo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam katika uzinduzi wa Shule ya Turkish Maarif iliyoko Boko, Profesa Ndalichako alisema serikali imejipanga kuboresha elimu nchini na hivyo kuwataka wawekezaji kujitokeza katika sekta ya elimu kutokana na upungufu wa shule uliopo.

"Kwa sasa makao makuu ya nchi yamehamia rasmi Dodoma, nawaomba wawekezaji na wadau wa elimu kuwekeza katika jiji letu la Dodoma kwa sababu bado kuna upungufu wa shule," aliomba. Profesa Ndalichako alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau ambao watasaidia katika kuboresha sekta ya elimu nchini ili kutimiza azma yake ya kuhakikisha kila mtoto anapata elimu bora.

"Ndugu zetu kupitia taasisi yao ya Turkey Maarif Foundation, tunatambua sekta ya elimu ni muhimu sana katika taifa letu, hivyo tunawahamasisha kuendelea kuwekeza katika maeneo mengine mfano Dodoma," alisema.

Waziri huyo alisema Uturuki imekuwa na ushirikiano wa muda mrefu na Tanzania katika kuwekeza kwenye sekta ya elimu na kuwapongeza kwa hatua ya kujenga shule katika maeneo mbalimbali nchini, akizitolea mfano shule zao zilizoko katika mikoa ya Dar es Salaam, Zanzibar na Arusha na kuwakaribisha kujenga shule katika Mkoa wa Dodoma.

Alisema serikali imeipa kipaumbele sekta ya elimu kwa kutoa elimu bila malipo ikitenga zaidi Sh. bilioni 28 kila mwezi ili kuboresha sekta ya elimu nchini kama nyenzo umuhimu ya kufikia uchumi wa kati.

Akizungumzia shule za taasisi hiyo, Balozi wa Uturuki nchini, Ali Davutoglu, alisema wameamua kujenga shule hizo nchini kutokana na ushirikiano mzuri uliopo baina ya Tanzania na Uturuki na amani iliyopo nchini.

"Shule hii tunayoizindua leo (jana), itahudumia wanafunzi 600, Turkish Maarif ni moja ya shule maarufu hapa Tanzania zenye takriban wanafunzi 1,900," alisema.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Big Fish, Abraham Mndeme, alipokwenda kuzindua teknolojia ya kisasa ya ufugaji wa samaki katika mabwawa, inayotumiwa na kampuni hiyo iliopo Kigamboni jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# DC ataka wachimbaji kuondoka eneo la shule

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, amezuia uchimbaji wa madini ya dhahabu unaofanywa na wachimbaji wadogo katika eneo la Shule ya Msingi Mwabomba, Halmashauri ya Ushetu, baada ya wachimbaji kuvamia eneo hilo.

Akizungumzia jana na wachimbaji katika eneo hilo, Macha alisema uchimbaji wa madini uendelee nje ya mipaka ya shule kwa kuwa serikali haiwezi kubadili matumizi ya maeneo ya shule bila utaratibu.

Aliwataka wachimbaji waliopo waanze kufanya taratibu za kuondoka katika eneo hilo na hadi kufikia Jumatatu (Februari 17), asiwepo mchimbaji.

Aliagiza viongozi wa serikali ya kijiji kwa kushirikiana na kamati ya shule na wataalam wa halmashauri kwenda kuwaonyesha mipaka ya shule wachimbaji hao ili wasiendelee na uvamizi katika maeneo ya shule.

Awali, Diwani wa Kata ya Idahina, Yuda Lunyalula, alisema tangu Februari 5-11, serikali ya kijiji na mamlaka zingine ndani ya kijiji zimepata zaidi ya Sh. milioni 22 kutokana na makusanyo ya ushuru.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ushetu, Michael Matomola, alisema halmashauri hiyo ilikwisha uelekeza uongozi wa kijiji kuwatangazia wachimbaji wasiendelee katika eneo la shule.

Baadhi wa wachimbaji waliomba wapewe muda wa zaidi ya wiki moja ili kuondoa usumbufu na madhara yanayoweza kujitokeza kutokana kusimamishwa ghafla.

Uvamizi wa eneo la shule ulianza tangu Februari Mosi, mwaka huu.

# Waandikishaji wapigakura wapewa mafunzo

**Na Mwandishi Wetu**

KAIMU Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Faudhia Nombo, amefunga mafunzo ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kwa watendaji wa kata, watakaokuwa maofisa waandikishaji wasaidizi ngazi ya kata.

Mafunzo hayo yaliyosimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), yalianza kutolewa Februari 10 na kumalizika juzi katika Bwalo la Maofisa wa Polisi Oysterbay, jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na maofisa watendaji kutoka kata 20 za manispaa hiyo.

Akifungua na kufunga mafunzo hayo, Nombo alisema mafunzo hayo ni chachu kwa maofisa hao na kwamba wanapaswa kutumia nafasi hiyo vizuri ili kuisaidia serikali kupata idadi kamili na sahihi ya wananchi watakaopiga kura katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba, mwaka huu.

Nombo alisema waandikishaji hao wanapaswa kuhakikisha wanafuatilia na kusikiliza mafunzo hayo kwa umakini mkubwa kwa kuwa kazi hiyo ni nyeti na ni kwa maslahi maendeleo ya nchi.

Mafunzo hayo, alisema yanahusisha mfumo mzima wa namna ya mchakato wa uandikishaji ambao umegawanyika katika maeneo matatu.

Aliyataja maeneo hayo kuwa ni uandikishaji wa mwananchi mpya kabisa, uboreshaji wa taarifa za mpigakura kwenye daftari (hii ni iwapo mwananchi alihama eneo la makazi au iwapo taarifa zilikosewa) pamoja na kumwondoa mpiga kura kwenye daftari kutokana na sababu mbalimbali kama vile kifo.

Pia alisema mafunzo hayo yatahusisha uingizaji wa taarifa za wapigakura katika mfumo wa kuandikisha wapigakura pamoja na waandikishaji wasaidizi.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo pia yalihusisha kuapishwa kwa waandikishaji wasaidizi ngazi ya kata, namna ya ujazaji wa fomu mbalimbali na namna ya kutumia sanduku litakalotumika kubeba vifaa mbalimbali vilivyounganishwa na kufanya kazi pamoja kwa ajili ya kuingiza taarifa binafsi za mpigakura.

"Kazi hii mliyopewa ni muhimu kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi mkuu ifikapo Oktoba, mwaka huu. Tunaboresha daftari la wapigakura kwa sababu kuna wengine wametimiza miaka 18 hivi karibuni na wengine wamehama makazi yao. Kwa hiyo mchakato huu ni muhimu sana niwaombe mkafanye kwa uangalifu mkubwa kama mlivyoelekezwa na watoa mada," alisema Nombo.

"Mnatakiwa kutumia lugha nzuri

# Uboreshaji daftari la kudumu wapigakura waanza Pwani, Dar

**Na Elizabeth Zaya**

UBORESHAJI wa daftari la wapigakura kwa Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani, utaanza leo, wananchi wakihimizwa kujitokeza ili kushiriki kwenye uchaguzi mkuu baadaye.

Uboreshaji huo utafanyika pia katika siku za mwisho wa wiki na hata katika siku za sikukuu.

Ofisa Elimu, Idara ya Habari na Elimu ya Mpigakura kutoka Tume ya Uchaguzi (NEC), Titus Mwanzalila, alisema hayo wakati wa kutoa mafunzo kwa wakufunzi wa wananchi kuhusu daftari hilo yaliyoandaliwa na Mtandao wa Uangalizi wa Uchaguzi Tanzania (TACCEO).

Mwanzalila alisema ni vema wananchi wa mikoa hiyo wakatumia vizuri siku saba zilizotolewa ili kujihakikishia kuwa na sifa ya kupiga kura.

Alitaja makundi yanayotakiwa kujiandikisha kuwa ni pamoja na waliopoteza kadi zao, kuboresha taarifa za watu ambao majina yao yapo kwenye daftari lakini wamefariki dunia, waliohama vituo vyao vya awali na wale watakaotimiza umri wa miaka 18 ifikapo Oktoba mwaka huu.

"Hatuandikishi wenye kadi za kupigia kura ambazo hazijaharibika wala ambazo hazijapotea wala hawajahama maeneo yao ya makazi," alisema.

Alisema kazi hiyo ya kuboresha daftari ni kwa awamu ya kwanza na uboreshaji mwingine utafanyika Machi mwaka huu.

Alisema katika utekelezwaji wa kazi hiyo haihitajiki kwenda na nyaraka zozote kwa ajili ya kuboresha ila kwa yule aliyepoteza kadi, anahitajika kutaja majina kamili kama yalivyokuwa kwenye kadi iliyoharibika.

"Mashine ya BVR inarekodi majina yote zaidi ya milioni ishirini yaliyokuwa yameandikwa mwaka 2015, kwa hiyo kama ulipoteza kadi, unatakiwa kwenda kituoni na kutaja majina kwa usahihi uliyotumia kujiandikisha mwaka 2015," alisema.

Mwanzalila alisema katika kazi hiyo yapo makundi yatakayopewa kipaumbele zaidi, ikiwa ni pamoja na watu wenye walemavu, wajawazito, wenye watoto wachanga na wazee.

Ofisa Sheria wa NEC, Fausta Mahenge, alisema ni haki ya mtu kuandikishwa na mwandishi msaidizi ndiye anayekutana na mwananchi aliyefika kituoni kujiandikisha.



Wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu katika mgodi wa Mtalingi Mine, uliopo Nyakagwe wilayani Geita, mkoani Geita, wakichenjua dhahabu kwa kutumia zebaki bila ya kuvaa vifaa kinga. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Serikali yafikiria kuondoa kodi vifaa uvuvi

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imesema itaangalia uwezekano wa kuondoa kodi kwenye vifaa vya uvuvi, kwa lengo la kuboresha sekta hiyo, kuongeza ajira kwa Watanzania na kukuza pato la taifa.

Hayo yalisema juzi na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, wakati akizindua teknolojia mpya ya ufugaji wa samaki inayotumiwa na kampuni ya Big Fish, iliopo Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

Teknolojia hiyo ni ya kutumiwa mabwawa machache na kuvuna samaki wengi ambayo imetolewa Uholanzi na inatumiwa na kampuni hiyo inayomilikiwa na mzawa na kuongea ajira kwa Watanzania.

Alisema, vifaa vya kilimo vina msamaha wa kodi, lakini bahati mbaya vifaa vya uvuvi havina msamaha huo, hivyo kuna haja ya kuangalia uwezekano wa kuiondoa ili kuleta tija kwenye sekta hiyo.

"Lakini kuna tatizo katika vifaa hivi vya uvuvi, kutokana na ukweli kwamba vinaweza kutumika kwenye shughuli nyingine kinyume cha ilivyokusudiwa na kusababisha ukwepaji wa kodi, hivyo tuko makini," alisema Ulega.

Alifafanua kuwa ufugaji wa samaki wa teknolojia ya kisasa unatumia mabomba, ambayo pia yanaweza pia kutumika katika ujenzi wa nyumba na inawezekana watu wasio waaminifu wakadanganya kuwa wanataka kutumia kwa ajili ya uvuvi ili wapate msamaha na kumbe sivyo.

"Hii ni changamoto ambayo ninaona iwapo kutakuwa na msamaha kwenye vifaa vya uvuvi, kutokana na ukweli huo nilioueleza, lakini jambo la msingi ni uaminifu kwa ajili ya kuleta maendeleo ya sekta ya uvuvi," alisema.

Alisema, sekta ya uvuvi inachangia katika pato la taifa kwa wastani wa asilimia 1.7 kwa mwaka na pia imetoa ajira milioni 4.5 ingawa bado inakabiliwa na changamoto nyingi.

Naibu Waziri alitaja moja ya changamoto hizo ni kutopatikana kwa chakula bora cha samaki, hali inayosababisha samaki wasikue kwa haraka inavyotakiwa na pia uzalishaji kupungua.

"Suala la chakula bora cha samaki ni muhimu sana, unaweza kukuta mtu anaweka chakula, katika bwana na kusema, baada ya miezi sita watakuwa tayari wanafaa kuliwa, lakini matokeo yake sivyo, inaweza kuchukua miezi tisa hadi 12," alisema.

Alisema, hiyo inatokana na chakula kutokuwa kile kinachotakiwa, na kuongeza kuwa ni muhimu suala la chakula bora cha samaki likapewa uzito kwa ajili ya kuzalisha samaki wengi zaidi.

Aliishukuru Serikali ya Uholanzi kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali ya Tanzania kwa kuwezesha kuimarika kwa kampuni ya Big Fish ambayo imeajiri vijana wa Kitanzania.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Abraham Mndeme, alishukuru serikali kwa kuunga mkono juhudi anazofanya za kuwekeza katika sekta ya uvuvi na kuongeza ajira kwa Watanzania.

"Vilevile niishukuru serikali ya Uholanzi kwa kuniwezesha kupata vifaa vya kisasa, ambavyo vinatusaidia kutumia eneo dogo na kufuga samaki wengi, " alisema Mndeme.

# Maisha wachimbaji madini hatarini matumizi zebaki

**Na Marco Maduhu,** GEITA

WACHIMBAJI wadogo wa madini ya dhahabu nchini yapo hatarini kutokana na kutumika zebaki kuchenjulia dhahabu, bila ya kuvaa vifaa kinga.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkurugenzi wa Taasisi ya kiraia FADeV inayojishughulisha na kuendeleza wachimbaji wadogo wa madini nchini, Theonestina Mwasha, wakati alipoambatana na waandishi wa habari kwenye mgodi mdogo wa madini wa Mtalingi Mine uliopo eneo la Nyakagwe, wilayani Geita mkoani humo.

Mwasha alisema moja ya kazi wanayoifanya ya kuendeleza wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu, ni kutoa elimu ya usalama wao hasa wanapoingia chini ya maduara kuchimba dhahabu, pamoja na kutumia zebaki kuchenjulia dhahabu wavae vifaa kinga ili wawe salama na kuepuka athari mbalimbali.

"Wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu idadi yao kubwa hawana elimu ya umuhimu kuvaa vifaa kinga pale wanapotafuta dhahabu wakiwa ndani ya maduara na hata kuchenjua dhahabu kwa kutumia zebaki, hawavai viatu vya usalama, groves, na kutumia mikono ikiwa tupu hali ambayo ni hatari kwa afya zao," alisema Mwasha.

"Mchimbaji anavyo chenjua dhahabu mikono yake ikiwa tupu, akipatwa na mchubuko na zebaki ikiingia mwilini tayari inaanza kumletea madhara ya kiafya taratibu ikiwamo kichwa kuuma, kupoteza kumbukumbu, kutosikia, kuathiri figo na hatimaye kupoteza maisha," aliongeza. Mmoja wa wachimbaji hao, Boniphace Charles, alisema wanatambua kuwa zebaki ina madhara kwao na kubainisha kuwa walishazoea kuchenjua dhahabu wakiwa mikono peku, huku wakiomba elimu itolewe zaidi ya umuhimu wa kuvaa vifaa hivyo.

Naye mmiliki wa mgodi huo mdogo wa madini ya dhahabu, Mtalingi Hamzeh, alisema wanatambua madhara ya kutumia zebaki kuchenjulia dhahabu na kufanya wanapogawa vifaa kinga kwa watumishi wao, hawavitumii licha ya awali kupewa elimu na taasisi hiyo ya FADeV, wakidai wameshazoea kufanya kazi wakiwa mikono tupu.

Alisema licha ya kutambua madhara hayo ya zebaki, na wachimbaji wadogo kutokuwa na mitaji mikubwa wameshindwa kumudu gharama za kutumia njia nyingine salama ya kuchenjulia dhahabu, na kutoa wito kwa taasisi za kifedha zitoe mikopo kwao ili waondokane na matumizi hayo ya zebaki.

# DC awapasha madiwani ubunifu mapato

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amewaomba madiwani wa Halmashauri ya Meru kuwa wabunifu wa kuanzisha vyanzo vya mapato na kuacha kufanya siasa za madaraka.

Akizungumza jana wilayani humo kuhusiana na kauli za madiwani wa halmashauri hiyo kuwa kuna upotevu wa zaidi ya Sh. milioni 300 kutokana na vitambulisho vya machinga, Muro alisema hilo siyo kweli. "Kama Sh. milioni 300 wanapigia kelele, lakini aliyeleta vitambulisho ameleta fedha za ujenzi wa vituo vya afya, zahanati, miradi ya maji vijiji kumi na mishahara yetu, wakiwamo madiwani wenyewe zaidi ya Sh. bilioni 30 anatuletea, hivyo hiyo siyo hoja ya msingi," alisema.

Alisema vema wakajielekeza kuwaza vyanzo vya mapato visivyomuumiza mwananchi mnyonge na vitambulisho hivyo vimeletwa na Rais John Magufuli ili kumwezesha mwananchi afanye biashara popote na kumpunguzia makali ya maisha. Muro alisema ni vema wakaacha porojo na siasa za madaraka, ambazo kwa sasa hazina nafasi, bali siasa inayotakiwa ni ile ya kuletea wananchi maendeleo.

Aidha, alisema vitambulisho hivyo vimesaidia kasi ya uchumi hasa vijijini kwa sababu wananchi amepata fursa ya kujinyanyua kiuchumi.

Diwani Isaac Kanuya, alisema ugawaji wa vitambulisho vya machinga vimechangia kushusha mapato ya halmashauri.

Alisema vitambulisho hivyo vimesababisha upotevu wa zaidi ya Sh. milioni 300 kwenye soko lao kwa sababu wengi wao walikuwa wakitoa ushuru kila siku Sh. 500, lakini kwa sasa wanatoa Sh. 20,000 kwa mwaka na kusababisha halmashauri kushindwa kupata mapato kama zamani.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Willy Njau, alisema hakuna haja ya kulalamikia uamuzi wa serikali kwa sababu ulishapitishwa, bali wao wajielekeze kwenye mikakati ya kutafuta vyanzo vya mapato kama kujenga vibanda ili wakusanye mapato zaidi badala ya kulalamikia Sh. milioni 300.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu (wa tatu kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 25 kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo (wa tatu kushoto), kwa ajili ya ununuzi wa vitanda pacha 47 vya hosteli ya wanafunzi wa Shule mpya ya Sekondari ya Mrisho Gambo. Wengine ni maofisa waandamizi wa mkoani humo na benki hiyo. **MPIGAPICHA WETU**

# Babati waondokana na adha ya maji

Na Cynthia Mwilolezi, MANYARA

WAKAZI 650 wa Kijiji cha Sangara wilayani Babati mkoani Manyara, wameondokana na changamoto ya muda mrefu wa ukosefu wa maji, baada ya mradi wa maji wa gharama ya Sh. milioni 229 kuzinduliwa.

Mradi huo unatoa maji lita 352,800 kwa siku, sawa na lita 14,700 kwa saa, unatumia mfumo wa malipo kabla ya huduma kwa njia ya elektroniki.

Mkurugenzi wa Shirika la WaterAid, Abel Dugange, akizungumza jana kwenye uzinduzi wa mradi huo, alisema, waliingia makubaliano ya kutekeleza mradi huo mwaka jana na Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Shirika la Habitat for Humanity, kampuni ya Water na Taasisi ya Fedha ya Unit Trust of Tanzania (UTT-MFI).

Dugange alisema kabla ya kutekeleza mradi huo, hali ya upatikanaji wa maji kwenye kijiji hicho, ilikuwa asilimia 20 tofauti na lengo la Taifa la asilimia 85 ya huduma za maji vijijini.

"Mradi huu umelenga kuhamasisha ubunifu na kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu na uendeshaji wa miradi ya maji ili kurahisisha upatikanaji wa huduma endelevu na hakika ya majisafi na salama vijijini," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, akizindua mradi huo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo, Alexander Mnyeti, aliwataka wakazi wa eneo hilo kuutunza ili uwe endelevu.

Kitundu alisema lengo la serikali ifikapo mwaka 2020 asilimia 85 ya waliopo vijijini wawe wamepata majisafi na salama na mwaka 2025 iwe asilimia 95 na mwaka 2030 iwe asilimia 100.

Mbunge wa Babati Vijijini, Vrajilal Jituson, alisema mradi huo ni wa mfano, kwani umeanzia Babati kisha wilaya za Korogwe mkoani Tanga na Arumeru mkoani Arusha zikafuata. Mkazi wa kijiji hicho, Magdalena Bayo, alisema awali walikuwa wanachota maji umbali mrefu, kwenye visima na makorongo ila mradi huo umewasaidia kwani upo karibu nao.

## Exim yachangia ununuzi vitanda vya wanafunzi

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya Exim Tanzania imechangia kiasi cha Sh. milioni 25 kwa ajili ya ununuzi wa vitanda pacha 47 vya hosteli ya wanafunzi wa Shule mpya ya Sekondari ya Mrisho Gambo iliyopo mkoani Arusha.

Hatua hiyo ni mwendelezo wa benki hiyo katika kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha sekta ya elimu hapa nchini.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi msaada huo iliyoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu alisema, mchango huo ni sehemu ya mpango wa uwajibikaji kwa jamii unaotekelezwa na benki hiyo ukifahamika kwa jina "Exim Cares" ukilenga kusaidia jamii.

"Benki ya Exim tunaamini kuwa tunalo jukumu kubwa la kufanya katika kuwezesha mabadiliko chanya katika jamii zinazotuzunguka. Elimu ni kati ya maeneo yetu ya kuzingatia na mpango huu unaendana na mkakati wetu wa kubadilisha maisha ya wanafunzi chini ya mpango wa 'Exim Cares' kupitia vitendo endelevu," alisema.

Matundu alisisitiza kwamba: "Benki ya Exim tunavutiwa zaidi katika kuleta athari chanya kwenye jamii ambazo tunatoa huduma zetu, hivyo kwa kuangalia nafasi yetu tumeaona kwamba kwenye hili tunaweza kusaidia vitanda pacha vipatavyo 47 vikiwa na uwezo wa kubeba wanafunzi zaidi ya 100."

Alitoa wito kwa taasisi na wadau nchini kuhakikisha wanawekeza kwenye uwezeshaji wa vijana kupitia elimu kutokana na ukweli kuwa bado wanakabiliwa na changamoto nyingi.

"Tumebaini kuwa kuna changamoto zinazoathiri vijana wa leo hususani wanafunzi ambazo zinaweza kuwaongoza kuelekea kwenye tabia zisizokubalika ndani ya jamii. Benki ya Exim, tunaamini kwamba kuna haja ya kuelekeza umakini na kuzingatia uwezeshaji wa vijana kupitia elimu. Tutaendelea kuwekeza katika hili na kutimiza wajibu wetu kwa miaka mingi ijayo," aliahidi.

Alipongeza serikali kwa kutoa elimu ya msingi bure kwa watoto wote hatua ambayo imekuwa ni msaada mkubwa kwa watoto wanaopitia changamoto mbalimbali za kiuchumi ikiwamo yatima, watoto wenye mahitaji maalum ya kielimu pamoja na vikundi vingine vyenye vya watoto wanaoishi mazingira magumu.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Gambo aliipongeza benki hiyo lwa msaada huo huku akibainisha kuwa umetolewa kwa wakati muafaka. "Kupitia msaada huu kutoka benki ya Exim tutaweza kuwasaidia wanafunzi wetu kukaa hosteli, haswa wale ambao kwa sasa wanatembea umbali mrefu kwenda na kurudi. Kwa kweli kupitia msaada huu msaada huu utawawezesha kujifunza vizuri na kutambua ndoto zao za masomo, " alisema Gambo.

Alisema mahitaji ya mradi huo ni vitanda 100 na magodoro ambayo utagharimu Sh. milioni 53.7.

# Waonywa kuharibu majengo ya zahanati

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imewaonya wananchi wa vijiji vya Kitowo na Kiraracha vilivyopo Kata ya Marangu Magharibi katika Wilaya ya Moshi, kutojaribu kuharibu kwa makusudi majengo na miundombinu ya Zahanati ya Kitowo ambayo imejengwa kwa fedha za ufadhili.

Juzi Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, aliwataka wananchi wa vijiji hivyo kutokuwa wabinafsi na kutumia rasilimali hiyo vibaya ikiwamo kuziharibu.

"Si fikra sahihi kufikiri kwamba binadamu walio karibu na rasilimali hizi kwa sasa wana haki ya kutumia ovyo na bila utaratibu miradi inayojengwa na wafadhili. Natoa onyo kwenu msijaribu kuharibu miundombinu ya zahanati hii ambayo imejengwa kwa fedha za Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, nataka rasilimali zote za hifadhi zitumike vizuri ili ziwe endelevu."

Alisema zahanati hiyo ya Kitoweo ni lazima ilindwe kwa nguvu zote ili kizazi kijacho kirithi rasilimali hizo, kwa kuwa na wana haki ya kunufaika.

Warioba pia aliwakumbusha wananchi hao kuwa majisafi yanayotiririka kutoka kwenye Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro yananufaisha wananchi wengi katika mikoa mitano, hivyo wanapaswa pia kulinda hifadhi hiyo.

Aliwataka wananchi hao kuwa makini na wanasiasa hususani katika mwaka huu ambao taifa linaelekea katika uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, kwa kuwa wanasiasa walaghai huchomoza na kupotosha mambo mbaimbali.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Dk. Alex Kazula, aliishukuru Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro kwa kusogeza huduma za afya kwa wananchi wa vijiji vya pembezoni.

Kukamilika kwa ujenzi wa zahanati hiyo, kunaongeza idadi ya zahanati kufikia 96 katika Wilaya ya Moshi. Zahanati hiyo itawanufaisha zaidi ya wananchi 15,000 kutoka kwenye vijiji sita vilivyomo katika Kata ya Marangu Magharibi.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Kamishna Mwandamizi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Herman Batiho, alisema ujenzi wake umetumia jumla Sh. 238, 994, 540.




Gavana wa Klabu ya Lions Kanda ya District 411C Tanzania, Shofiuddn Babul (wa tatu kushoto), pamoja na Rais wa Lions Club ya Moshi-Kibo, Vishal Pithia (wa nne kushoto), wakiwa na wanachama wa klabu hiyo wa Tanzania na Ubelgiji, baada ya kuweka jiwe la msingi na kuzindua ujenzi wa chuo maalumu cha ufundi kwa watu wenye ulemavu wa kusikia cha Msandaka, katika Manispaa ya Moshi, mapema wiki hii. Ujenzi wa chuo hicho, utagharimu zaidi ya Sh. milioni 700. **PICHA: JAMES LANKA**

# Uhaba vifaa tiba waikabili Hospitali Wilaya Mwanga

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

HOSPITALI ya Wilaya ya Mwanga, inakabiliwa na uhaba mkubwa wa vifaa tiba kama vipimo vya damu, vipimo vya kemia na vipimo vya CD4.

Ukosefu wa vifaa hivyo katika hospitali hiyo, unadaiwa kuwapo kwa miaka miwili sasa, hai ambayo inachangia kuzorotesha shughuli za utoaji wa huduma za afya.

Kutokana na hali hiyo, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, ameutaka uongozi wa hospitali hiyo kuandaa mkakati madhubuti utakaowezesha kuwapo kwa vipimo hivyo muhimu vya afya.

Dk. Ndugulile alitoa agizo hilo jana, wakati alipotembelea Hospitali ya Wilaya ya Mwanga kujionea hali ya utoaji huduma na kubaini kuwa hospitali hiyo haina vipimo hivyo. Baada ya kufanya ukaguzi, Dk. Ndugulile alisema: "Kwa miaka miwili sasa hakuna vipimo vya msingi katika hospitali hii, tunawakosesha huduma wananchi. "Haiwezekani hospitali kubwa ndani ya wilaya kukosa vipimo vya msingi, haiwezekani mtu hapa sasa hivi anahitaji kipimo cha damu atoke hapa aende Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi kwa ajili ya vipimo."

Katika hatua za kutafuta ufumbuzi wa changamoto hiyo, Waziri Ndugulile aliishauri kamati ya wilaya hiyo kuhakikisha wanatenga fedha kwa ajili ya kununua vifaa tiba. Aidha, Naibu Waziri huyo alishauri kuwa kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) wao wanatoa mkopo wa majengo na vifaa kwa taasisi za umma na binafsi, hivyo wanaweza kukutana na NHIF na kujadili kuhusu suala hilo.

Awali, Mbunge wa Mwanga (CCM), Prof. Jumanne Maghembe, akitoa salamu zake alisema changamoto ya kijiografia ndani ya wilaya hiyo inachangia wananchi kukimbilia hospitali za wilaya jirani kupata huduma.

"Wilaya yetu hii ina upande wa mlimani na huku tambarare, wananchi wengi walio huku tambarare wanaona ni bora kwenda Moshi kwa ajili ya matibabu kuliko kwenda juu mlimani iliko hospitali ya wilaya," alisema Prof. Maghembe.

Prof. Maghembe alisema wameshaanza mchakato wa kujenga hospitali nyingine teule katika eneo la tambarare ili wananchi wanaoishi maeneo hayo waweze kupunguziwa adha ya kwenda milimani kwa muda mrefu.

# Wawekezaji mashambani walalamikia mifugo

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WAWEKEZAJI wa mashamba ya uzalishaji wa mazao ya biashara katika Wilaya ya Siha, wamelalamikia makundi makubwa ya mifugo kutoka wilaya jirani za Longido na Arumeru kuingia katika maeneo yao na kusababisha hasara kutokana na kuharibu mazao hayo.

Mifugo hiyo inadaiwa kuvamia mashamba ya Mountain Side na Mawenzi yaliyopo eneo la West Kilimanjaro.

Meneja wa Shamba la Mawenzi, Alex Mosha, akizungumza na Madiwani wa Wilaya hiyo waliotembelea mashamba ya wawekezaji, alisema mifugo hiyo inayoingia kutoka wilaya za jirani mkoani Arusha imekuwa ikiharibu mazao yao.

"Kiujumla tatizo kubwa ambalo huwa linatusumbua ni mifugo kuingia shambani na kuharibu mazao, lakini tumechunguza tukagundua huwa inatusumbua ni ile inayotoka Longido na Arumeru mkoani Arusha," alisema mmoja wa wawekezaji hao.

Baada ya taarifa hiyo, Diwani wa Ngarenairobi, Patrick Kimario, aliliomba Baraza la Madiwani la Wilaya hiyo kutunga sheria ndogo na kuishauri serikali jinsi ya kuwalinda wawekezaji hao ili uwekezaji wao uwe salama na kuwavutia wengine.

Kimario aisema: "Mmeona wenyewe karibu wawekezaji wote wamezungushia nyaya zenye shoti ya umeme kwa lengo la kuzuia mifugo isiingie kwenye mashamba yao, hii ni jambo la kufikirisha sana.

"Mmesikia kwenye taarifa zao kwamba tatizo kubwa ni wafugaji wa jamii ya Kimasai kuingiza mifugo yao katika mashamba yao bila kujali kama kuna mazao na kuwasababishia hasara kubwa."

Alisema kwa malalamiko hayo, sasa ni vyema Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), kuja na mkakati wa ulinzi dhidi ya wawekezaji ili kuzalisha mazao yao kwa wingi na halmashauri yao iweze kupata fedha na kuongeza mapato.

"Tusipoangalia wawekezaji watakimbia wote, kwa sababu hakuna mwekezaji ataweza kuwekeza sehemu isiyo salama, mfano eneo la Ndarakuwai lilivamiwa na wafugaji wa jamii ya Kimasai na nadhani tuwe wakali tusiruhusu jambo hili litokee tena."

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Juma Jani, alisema kutokana na malalamiko hayo, wilaya hiyo itahakikisha ulinzi wa mashamba hayo unakuwa endelevu ili kuvutia na wengine kuja kuwekeza wilayani humo.

Naye Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Ndaki Muhuli, aliahidi kulifanyia kazi suala hilo na kwamba madiwani wasiwe na wasiwasi.



Ukurasa 14

Wawekezaji ‘graphite’ Ulanga walipoanza maisha kwa ofisi ya kijiji



Ukurasa 16

Ilivyo kampeni maalum serikalini kuwapaisha kinamama kiuchumi


# BUFE

IJUMAA FEBRUARI 14, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 15

## Umewahi kuwaona nyani na simba wako pamoja?



## Sheria kuweka mazingira bora sekta huduma ndogo za fedha

Ukurasa 18

**Rita yaanika mapinduzi yake toka utendaji hadi makusanyo** Ukurasa 20

BIASHARA

# Wawekezaji madini 'graphite' Ulanga walipoanza maisha kwa ofisi ya kijiji

• Waziri shuhuda, adokeza ya fidia, mengi mapya yatajwa




Waziri wa Madini, Doto Biteko, akikabidhi funguo za ofisi za Serikali ya Kijiji cha Mdindo, Kisewe na Nawenge wilayani Ulanga, baada ya kujengwa na kampuni ya uchimbaji madini Mahenge Resources. Kulia kwa Waziri ni Mwenyekiti wa kampuni hiyo, John de Vries. **PICHA ZOTE: ROMANA MALLYA**

**Na Romana Mallya, aliyekuwa Mahenge**

FEBRUARI Mosi mwaka huu, imekuwa tarehe muhimu kihistoria kwa wanavijiji wa Mdindo, Kisewe na Nawenge wilayani Ulanga mkoani Morogoro, baada ya kukutana kwenye uwanja uliozungukwa na milima yenye uoto wa asili, kupokea majengo mapya matatu ya ofisi za vijiji vyao.

Licha ya mvua kubwa kunyesha, baadhi ya barabara ndani ya vijiji zikipata changamoto kutopitika, mamia ya wanakijiji walijikusanya katika uwanja huo uliopo Mahenge, ambako makabidhiano ya ofisi hizo yalifanyika.

Hapo pameigharimu kampuni ya Mahenge Resources Sh. milioni 51 na iliyoko katika mchakato kujenga mgodi mkubwa wilayani humo, kwa ajili ya kuchimba madini ya kinywe (graphite).

Ni madini yanayotumika kutengeneza bidhaa mbalimbali kama vile breki, kinga za mashine, betri za simu, kompyuta mpakato (laptop) na penseli.

Shughuli za makabidhiano kiofisi kwa upande wa serikali, alikuwapo Waziri wa Madini, Doto Biteko, aliyeambatana na Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, Ngolo Malenya, mbunge wa jimbo hilo, Goodluck Mlinga na viongozi wengine sekta ya madini.

Kampuni ya Mahenge, alikuwapo Mwenyekiti, John De Vries, ambaye pia ni Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Black Rock Mining kutoka Australia.

> **Wananchi watapata ajira za kitaalamu na zisizo za kitaalamu, kupitia kufanya biashara na hivyo kupata fursa ya kuuza vitu mbalimbali katika mgodi huu.**

Kabla ya viongozi hao kuwasili eneo hilo, wingu lilifunga mawinguni na hatimaye mvua kubwa ilishuka huku burudani za ngoma za asili zikiendelea kuashiria kusherehekea yale yaliyohidiwa na mwekezaji, kabla ya ujenzi wa mgodi; kujenga ofisi na kulipa wananchi fidia.

Eneo ziliko ofisi hizo ni umbali wa kilomita 231 kutoka mjini Morogoro, ikiwa ni safari ya kuvuka miji midogo, vijiji vingi na barabara za lami na nyingine vumbi.

**WAZIRI BITEKO**

Akizungumza katika makabidhiano hayo, Waziri Biteko anaeleza namna alivyoguswa na mafanikio yaliyofanywa na kampuni hiyo, akisema: "Ningependa kutoa maoni yangu kwa nini mafanikio ya mradi huu ni muhimu Tanzania. Wachimbaji madini wana wajibu mkubwa kuendeleza rasilimali zilizopo chini ya ardhi na kuzifanya zilete tija kwa wadau."

Kuhusu ofisi zilizozinduliwa, Waziri Biteko anasema ni ishara nzuri ya kampuni ya madini inayowajibika kwa umma.

"Ni kielelezo chema cha kampuni inayotimiza wajibu wake wa kurudisha manufaa ya mradi kwa wananchi yanayojulikana kama 'Corporate Social Responsibility (CSR).'"

Anadokeza kufahamishwa mradi wa Mahenge Resources utatumia reli ya Tazara kusafirisha bidhaa zao, kuanzia Ifakara hadi Bandari ya Dar es Salaam.

"Wananchi watapata ajira za kitaalamu na zisizo za kitaalamu, kupitia kufanya biashara na hivyo kupata fursa ya kuuza vitu mbalimbali katika mgodi huu," anasema na kuendelea:

"Hii inamaanisha sehemu kubwa ya fedha zitokanazo na mgodi, zitabaki hapa hapa. Hili ndilo jambo la msingi zaidi kwenye sera yetu ya madini."

Waziri Biteko anarejea tamko la tarehe 24 ya mwezi uliopita, Rais Dk. John Magufuli, aliposema: ""Tunahitaji mgawanyo sahihi wa mapato yatokanayo na uvunaji rasilimali zetu (win win situation)... Rais Magufuli ana maono kwamba sekta ya madini itakuwa inachangia asilimia 10 ya pato la taifa ifikapo mwaka 2025."

Kwa mujibu wa Biteko, kwamba ni jambo linalowezekana iwapo kutaendelezwa uanzishwaji migodi mipya mikubwa, ya kati na midogo na kufikia ndoto hiyo, ni budi sheria zilizopo zifuatwe.

Waziri Biteko anaeleza maono yake kwa mradi wa Mahenge Resources, kwamba utafungua njia kwa awamu hiyo mpya ya migodi mikubwa na kati nchini.

"Ninaamini kinywe au graphite itakuwa sehemu muhimu ya ujenzi huu wa mgodi mipya mikubwa. Hii itaifanya wilaya ya Ulanga na eneo hili la Mahenge litambulike kimataifa kama mzalishaji wa kinywe bora duniani.

Anasema hitaji la kinywe linaongezeka umuhimu na umaarufu wake, kwa sababu ya kutumika kutengenezaa betri na vifaa vingine vya kielektroniki.

"Simu zetu zote tulizo nazo zina graphite kwenye betri zake. Upatikanaji wake utazidi kuongezeka umuhimu kadri dunia inavyoendelea kuhamia kwenye teknolojia ya magari ya umeme, kwa lengo la kulinda mazingira na kupambana na mabadiliko ya tabia nchi yatokanayo na moshi wa magari," anaeleza, huku akifafanua nafasi ya sifa kurudi Mahenge.

Waziri anaeleza kuwa na taarifa za kampuni hiyo kuanza hatua za uthamini, fidia na uhamishaji makazi, akisema:"Nitoe rai kwa maofisa wa serikali wanaoshiriki mchakato huu kutoka katika ngazi zote, kuanzia taifa hadi ya kijiji, kushiriki kikamilifu."

"Naiasa kampuni ya Mahenge Resources kuendelea kushirikiana na wananchi wa Mahenge katika kuwaletea maendeleo endelevu kutokana na kubarikiwa kuwa na madini haya," anasema.

Kuhusu ofisi zilizozinduliwa, Waziri Biteko anasema: "Ni kielelezo chema cha kampuni inayotimiza wajibu wake wa kurudisha manufaa ya mradi kwa wananchi yanayojulikana kama 'Corporate Social Responsibility (CSR)' (uwajibikaji wa shirika kwea jamii).

**KAMPUNI ILIKOANZIA**

Anasema, kampuni hiyo kwa muda mrefu ilikuwa katika utafiti na kufikia hatua ya kuwekeza kwenye graphite ya Mahenge.

"Uwekezaji wao ni wa Dola za Marekani milioni 23 (Sh. bilioni 50.6) zitakazojenga mgodi huo wa Mahenge Resources. Changamoto waliyo nayo ni fidia kwa wananchi.

"Tayari tumeshawaelekeza waikamilishe haraka kabla ya uwekezaji, wameomba katika mchakato huu timu ya uthamini iwe na wawakilishi.

"Tayari nimemuelekeza Mkuu wa Wilaya wa hapa wawe na wawakilishi wa kijiji kwenye timu hiyo ili baadae kusitokee malalamiko."

Waziri Biteko anasema kampuni imeshapewa sampuli mbalimbali za madini hayo ambazo walizipeleka katika maabara tofauti na wamejiridhisha, Kinywe ya Tanzania ni bora kuliko zinazopatikana maeneo mengine duniani.

**MANENO YAO**

Amina Juma mkazi wa Mahenge, anasema endapo kampuni zinazojishughulisha na shughuli ya uchimbaji wa madini zikifuata sheria za nchi, zitawawezesha wananchi kunufaika na miradi hiyo mikubwa.

"Tanzania tumebarikiwa madini ya aina mbalimbali, huku kwetu tuna madini ya Kinywe endapo wawekezaji hawa wanaokuja kuwekeza wakifuata sheria ninaamini sisi wananchi tutaondokana na



Wananchi wa Mahenge, Wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro, wakishuhudia uzinduzi wa moja ya jengo kati ya matatu ambayo yamejengwa na kampuni ya Madini ya Mahenge Resources kwa ajili ya matumizi ya ofisi ya Serikali ya Kijiji.

umaskini," anasema.

Joseph Peter anasema, mikataba ya madini iliyotiwa saini mbele ya Rais Dk. Magufuli kama wawekezaji wataitekeleza, itaongeza uchumi wa nchi wa wananchi nao hawatalia njaa.

Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Black Rock Mining, John de Vries, anasema imani yake ni kwamba, Tanzania itapata maendeleo makubwa katika sekta ya madini kupitia madini hayo ya Kinywe.

Aidha, anafafanua kuwa wajibu wao kama mwekezaji ni kuhakikisha wanarejesha manufaa kwa jamii.

"Tulipowauliza mlisema mnataka makazi bora zaidi, mlisema mnataka funguo, kuwapa funguo ndio dira yetu katika uthamini, hili ni deni letu na leo tumeanza kwa kutoa funguo za ofisi hizi," anasema.

Anasema hadi sasa wamewaomba wanahisa wao na tayari wameshapata Dola za Marekani milioni 23 kwa ajili ya uwekezaji huo na kwamba wanahitaji kuwa na fedha nyingi zaidi kwa ajili ya fidia.

"Tupo katika hatua muhimu ya mchakato wa kujenga mgodi, tunawasiliana na benki zenye mitaji mikubwa ili tufanikishe hili na tuweze kukabidhi serikalini asilimia 16 kama mkataba wa madini unavyosema," anasema.

Vries anasema kampuni hiyo imechukua tahadhari kubwa ili wasiahidi kitu ambacho baadaye washindwe kukitekeleza.

"Chochote tutakachoahidi tutakitekeleza, tunaamini hivi karibuni tutapata funguo kwa ajili ya mradi huu ikiwa ni pamoja na fidia zenu kwa wale watakaopisha uwekezaji huu," anasema.

Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, Ngolo Malenya, anasema kampuni hiyo imekuwa ikishirikiana nao katika shughuli mbalimbali za kijamii.

"Mwaka jana tulikuwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 38, tulifanya harambee na kampuni hii ya Mahenge ilichangia Sh. Milioni 15, katika shughuli za Mwenge wa Uhuru walitoa sare za watoto wa alaiki zenye thamani ya Sh. Milioni 10 na leo wanatukabidhi ofisi za vijiji vitatu vinavyogusa maeneo yao ya uwekezaji," anabainisha.

> **"Tulipowauliza mlisema mnataka makazi bora zaidi, mlisema mnataka funguo, kuwapa funguo ndio dira yetu katika uthamini, hili ni deni letu na leo tumeanza kwa kutoa funguo za ofisi hizi.**

Mbunge wa Jimbo la Ulanga, Goodluck Mlinga, alisema kampuni hiyo imetoa mchango mkubwa katika maeneo hayo na imekuwa ikishirikisha jamii.

Aidha, Mlinga aliwataka Tanesco kuhakikisha umeme unafika kwa wananchi ambao bado hawajapata nishati hiyo.

Kampuni ya Mahenge Resources itakapoanza uchimbaji inatarajia kuzalisha tani 80,000 kwa mwaka na uzalishaji huo baadae utafikia mpaka tani 250,000 kwa mwaka na utachangia Dola za Marekani milioni 100 (sawa na Sh. Bilioni 226).

Aprili 24, mwaka 2018, wananchi wa Mahenge, walishuhudia tani 500 zikisafirishwa kupitia usafiri wa Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (Tazara), katika stesheni iliyopo Ifakara, mzigo ukielekea Bandari ya Dar es Salaam, kwa kuzisafirisha kwenda Canada.

Uzinduzi wa usafirishaji wa madini hayo ulifanywa na kampuni hiyo na ulifanyika viwanja vya stesheni ya Tazara, Ifakara ambao ulishuhudiwa na Ofisa Madini.

Uwepo wa Kinywe, unaifanya Tanzania kuwa moja ya mataifa yanayozalisha kwa wingi madini hayo. Katika miradi hiyo mitatu mikubwa, ina uwezo wa kuzalisha jumla ya tani 240,000 kwa mwaka za madini hayo.

Mradi wa Namangale unaelezwa kuwa na uwezo wa kutoa tani 100,000 pamoja na Mahenge, ambayo ikikamilika na kuanza kufanya kazi, itaifanya Tanzania kuwa nchi ya pili kwa kuzalisha madini hayo duniani, ikitanguliwa na China inayozalisha zaidi ya tani 700,000 kwa mwaka.

Nchi ya India inashika nafasi ya tatu kwa kuzalisha tani 170,000 na Brazili nafasi ya nne ikizalisha tani 80,000, Canada, Korea Kusini na Uturuki wanazalisha tani 30,000. Zingine ni Russia inayozalisha tani 14,000, Mexico tani 8,000, Ukraine na Zimbabwe tani 6,000, Madagascar tani 5,000, Sri Lanka tani 4,000, Norway tani 2,000 na nchi nyingine zinazalisha tani 1,000.

# Umewahi kuwaona nyani na simba wako pamoja?

• Shuhudia maajabu haya



Nyani na mtoto wa simba katika maisha ya pamoja. **PICHA: BBC**





**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

NI maajabu ya aina yake, wana utalii wa Afrika Kusini, kunasa ushuhuda usio kawaida, nyani akimbeba mwana wa simba katika mbuga za kitaifa za wanyamapori ya Kruger. Anasema kwamba hawajawahi kuona.

Mkurugenzi wa Kurt Safari, anasema kwamba msimu wa mvua unafanya kuwa vigumu kuwaona wanyama hao, akiongeza: "Ni msimu wa mvua katika mbuga ya Kruger na miti imekuwa mikubwa huku nyasi zikiwa ndefu. Wakati nyani wanapoondoka katika barabara na kuingia katika nyasi , sio rahisi kuwaona.'.

Schultz anasema kwamba, mwana simba huyo aliyekuwa amebebwa na nyani, alikuwa hatarini ana anongeza: "Nyani huyo wa kiume aliruka kutoka tawi moja hadi jingine, akimbeba simba huyo mdogo kwa muda mrefu. Mwana huyo wa simba alionekana kuchoka, japokuwa hakuonekana kuwa na jeraha.

"Nimeshuhudia nyani wakiwashambulia watoto wa chui na nimesikia nyani wakiwaua watoto wa simba, lakini sijawahi kuona jinsi nyani anavyomlea vizuri mwana wa simba".

Schultz anaeleza mtazamo wake kwamba, hadhani kwamba mwana simba huyo ataendelea kuishi salama. **BBC**

BIASHARA

# Ilivyo kampeni maalum serikalini kuwapaisha kinamama kiuchumi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SEKTA ya Maendeleo ya Jamii nchini, hivi sasa kitaifa imo katika orodha ya mafanikio makubwa katika kuhakikisha jamii inajiletea maendeleo, kwa kutumia fursa zilizopo.

Inawezekana kukawapo maeneo mtambuka katika tathmini hiyo, lakini Nipashe imeangukia katika sura kuu tatu, chini ya kivuli cha Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Hapo panatajwa: Uwezeshaji wanawake kiuchumi, huduma kwa wazee, ustawi wa watoto na usimamizi wa mashirika yasiyo ya kiserikali. Majukumu hayo yote yaaangukia katika Idara ya Maendeleo ya Jamii.

Ni idara inashughulikia masuala ya ustawi na jinsia kwa kuweka kipaumbele katika kuwezesha wanawake kiuchumi.



Wananchi wa Kijiji cha Chibumagwa, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. John Jingu (mwenye miwani) wakibeba tofali wakati wa kampeni ya kitaifa kuhamasisha wananchi kuboresha makazi inayoendelea katika vijiji nchini. **PICHA ZOTE: HISANI YA WIZARA**

### UWEZESHAJI WANAWAKE

Katika jitihada za Wizara kuwezesha wanawake kiuchumi, Serikali kupitia Benki ya Posta Tanzania, imeendelea kuwawezesha wanawake kupata mikopo yenye masharti nafuu katika mikoa 26 nchini, kiasi cha Sh.Bilioni 2.5 zimetolewa kwa wanawake wajasiriamali 3,035 wa mikoa 26 nchini.

Pamoja na mikopo ya masharti nafuu, serikali pia imeendelea kuhamasisha wanawake kujiunga na vyama vya ushirika wa kuweka na kukopa, maarufu Saccos zipatazo 130 zilizoanzishwa katika mikoa Mara, Mwanza, Tanga, Kigoma, Dodoma, Kagera, Shinyanga, Simiyu, Rukwa, Ruvuma, Mbeya, Lindi, Mtwara, Geita, Manyara na Dar es Salaam.

Ripoti iliyopo ni kwamba, serikali imekuwa ikitoa mafunzo kuhusu urasimishaji na uboreshaji bidhaa na kuunganishwa na Mamlaka za Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa (TFDA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), yaliyotolewa kwa wanawake wajasiriamali 7,713 ili kuongeza ubora wa bidhaa na kuwawezesha kupata taarifa za masoko ya bidhaa zao.

Pamoja na utoaji mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake, inaelezwa serikali pia imeendelea kutenga fedha asilimia tano kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake katika Halmashauri 185.

Aidha, serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko huo unaongezeka kila mwaka, Sh.Bilioni 3.4 zilitolewa mwaka 2016/17; Sh. bilioni 8.8 mwaka 2017/18; Sh. bilioni 16.3 na mwaka 2018/19; Sh. bilioni 11.1 zilitolewa kuwezesha wanawake wengi zaidi kuinuka kiuchumi.

> **"Mpaka kufika Machi, mwaka huu serikali ilianzisha mabaraza ya watoto 19 katika ngazi ya mikoa, mabaraza 121 katika ngazi ya halmashauri za manispaa, wilaya, miji.**

### NGUVU KWA WANAWAKE

Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mkoa Rukwa



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akishiriki ujenzi wa vyumba vya bweni la wasichana wa Shule ya Sekondari Kirare,jijini Tanga ikiwa, kuunga mkono juhudi za wananchi.

mwaka 2018, Waziri mwenye dhamana, Ummy Mwalimu, anawataka Wakurugenzi wa Halmashuri zote nchini kutenga asimilia nne kwa ajili ya mikopo ya wanawake yenye tija, itakayoweza kuwasaidia kuongeza vipato vya kujikwamua kiuchumi.

Waziri Ummy anasisitiza kufikia azma ya Tanzania ya Viwanda, halmashauri hazina budi kujiwekea mikakati ya utoaji mikopo mikubwa itakayowawezesha wanawake na wananchi kwa ujumla kufikia azma zao.

Kuhusu utekelezaji wa agizo hilo kutoka kwa Waziri, kuna halmashauri 185 zimetoa Sh.Bilioni 39.7 katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ndani ya miaka minne, ikinuia kuwezesha mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wajasiriamali 877,071.

Serikali, pia imeshafanya uhamasishaji kwa wanawake wajiunge na mifuko ya hifadhi ya jamii na kutoa mafunzo kwa wanawake wajasiriamali 207 wa Mkoa wa Mwanza, kuhusu namna ya kujiunga na mifuko hiyo.

### SHERIA MPYA

Sheria ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa imeongezewa kifungu kuzielekeza halmashauri zote kuchangia asilimia 10 ya mapato yao ya ndani, kwa ajili ya mikopo ya masharti nafuu kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Hiyo imeenda na utaratibu wa kuondoa kero kwa wajasiriamali wanawake, kwa mamlaka za serikali za mitaa zinawajibika kutenga maeneo ya biashara kwa wajasiriamali, wakiwamo wanawake na sasa kuna halmashauri 150 zimeshatenga maeneo ya biashara na viwanda.

Pia, serikali imetenga maeneo rasmi yenye ukubwa wa hekta 15,822.64 kwa ajili ya biashara kwa wajasiriamali, Hapo inajumuisha mama lishe, wauza mboga katika mikoa ya Arusha, Iringa, Mara, Rukwa, Tanga, Shinyanga, Mwanza, Kilimanjaro,

Singida, Morogoro, Singida, Manyara, Njombe, Kagera, Dar es Salaam, Dodoma, Lindi, Geita, Tabora na Ruvuma.

### HUDUMA WAZEE

Idara hiyo imekuwa na jukumu la kushughulikia ustawi wa wazee nchini na imendelea kuhakikisha wazee wanatambuliwa na kupatiwa huduma za matibabu bila malipo.

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wazee Duniani hivi karibuni mkoani Mtwara, Waziri Ummy, anasema serikali imewatambua wazee 1,897,021 katika halmashauri 185, ndani ya mikoa 26 ya Tanzania Bara, wazee 766,227 walipatiwa vitambulisho vya matibabu sawa na asilimia 40 ya wote wanaostahili.

Waziri Ummy, anaongeza kufikia Juni, 2019 idadi ya wazee waliopatiwa vitambulisho vya matibabu bure wameongezeka kutoka 213,025 akiwataja wanaume kuwa 106,129 na wanawake 106,896 mwaka 2015/16 hadi kufikia wazee 766,227. Kati yao wanaume wako 391,647 na wanawake 374,577.

Katibu Mkuu, anayeshughulikia idara hiyo, Dk. John Jingu, anasema serikali inatoa huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu kwa wazee wasiojiweza wanaoishi katika makazi 16 ya wazee yanayomilikiwa na serikali.

Dk. Jingu pia anasema, Mkakati wa Kutokomeza Mauaji ya Wazee (2018 - 2023) umeandaliwa ili kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu haki za msingi kwa wazee na kuongeza kuna wabaraza ya wazee 8,183 yameanzishwa katika halmashauri kuwezesha upatikanaji haki kwa wazee nchini.

### USTAWI WATOTO

Dk. Jingu anasema, ili kuhakikisha watoto wanalindwa dhidi ya uonevu, ukatili, udhalilishaji, utumikishwaji

na mila potofu, serikali imeanzisha Mtandao wa Mawasiliano ya Simu Namba 116, ili kuwezesha jamii kutoa taarifa za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Kupitia mtandao huo, kuna jumla ya watoto 3,833 waliofanyiwa ukatili waliwezeshwa kupata huduma za chakula, vifaa vya shule, huduma za sheria na afya.

Anasema serikali imeanzisha vituo vya huduma jumuishi za pamoja kushughulikia wanaosumbuliwa na katika mikoa tisa nchini anayoitaja kuwa ni: Mbeya, Dar es Salaam, Pwani, Kilimanjaro, Arusha Shinyanga, Iringa, Mwanza na Tabora.

Lingine linalotajwa katika hilo, kuna Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto 11,520 zimeanzishwa, katika mgawanyo maalum: Mbili katika ngazi ya taifa; zingine 26 ngazi ya mkoa; 112 katika ngazi ya halmashauri; 2,592 ngazi ya kata; na 8,788 ngazi ya kijiji/mtaa.

Dk. Kingu anasema serikali imeratibu upatikanaji huduma za misingi za malazi, chakula, mavazi, matibabu na elimu kwa watoto walio katika mazingira hatarishi, wanaoishi katika makao ya watoto katika mikoa 26.

"Watoto wanaoishi katika makao ya watoto wanaongezeka kila mwaka ambapo mwaka 2015/16 makao ya watoto yalihudumia watoto 4,379, mwaka 2016/17, watoto 4,515; mwaka 2017/18, watoto 6,132; na mwaka 2018/19, watoto 13,420," anasema

Katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Afrika mwaka huu mkoani Geita, Waziri Ummy, anasema katika kuimarisha haki ya ushiriki wa mtoto, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhimiza Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza bajeti ya kuwezesha utendaji wa mabaraza ya watoto.

Anasema mabaraza hayo yanatoa fursa kwa watoto kujadili masuala mbalimbali yanayohusu haki na ustawi wao na pia kuishauri Serikali kuhusu masuala hayo.

Vilevile, Waziri Ummy anasema mpaka kufika Machi, mwaka huu serikali ilianzisha mabaraza ya watoto 19 katika ngazi ya mikoa, mabaraza 121 katika ngazi ya halmashauri za manispaa, wilaya, miji.

Aidha katika ngazi za kata kuna jumla ya mabaraza 733, sambamba na kuwapo mabaraza 795 katika ngazi ya kijiji ambayo, yamekuwa na mchango mkubwa.

Katika kuimarisha ustawi na maendeleo ya familia nchini, anasema wizara hiyo yenye dhamana na ustawi wa jamii, imetoa mafunzo ya malezi chanya kwa wazazi na walezi 635 kwenye ngazi ya familia ndani ya jumla ya halmashauri 132 katika mikoa 26 nchini, kuhusu stadi za malezi chanya kwa watoto.

Aidha, elimu hiyo imewezesha kuanzishwa kwa vikundi vya Malezi 1,184 katika halmashauri 15 za mikoa saba.

### USIMAMIAJI NGO

Pia, kwa kipindi hicho serikali imeendelea kusajili, kufuatilia na kuratibu shughuli za mashirika yasiyo ya kiserikali, ili kukuza mchango wako katika kusaidia jamii kufikia maendeleo yao.

Taarifa iliyopo ni kwamba, serikali imeanzisha mfumo wa kielektroniki wa uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) unaowezesha kufanyika kwa malipo ya ada mbalimbali, inayotekelezwa na asasi hizo zisizo za kiserikali na wanufaika miradi.

Pia, anataja kwamba ni mfumo unaosaidia kujua kiasi cha fedha kilichotumiwa na wafadhili kwa miradi inayotekelezwa, ili kujenga uwazi na uwajibikaji, sambamba na kuboresha uratibu wa mashirika kwa manufaa ya wananchi na maendeleo ya Taifa.

# Biashara katika picha




Mkurugenzi wa Idara ya Biashara ya Vodacom Tanzania Plc, Linda Riwa (katikati) akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, katika uzinduzi wa kampeni mpya ya "Wajanja hatuzimi data" ambapo wateja wanapata vifurushi na bando zilizoongezwa thamani zaidi pamoja na kifurushi kipya cha data cha Jimwage. Kulia ni Mkuu wa Idara ya Bidhaa za wateja, Celvin Mmasy. **NA MPIGAPICHA WETU**



Mchuuzi wa mahindi mabichi akichemsha pembeni ya barabara katika eneo la Mbezi Juu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Wachuuzi wa matikitimaji wakiwa wameyamwaga chini huku wateja wakiendelea kuchagua, nje ya soko la Sabasaba, jijini Dodoma jana. Tikiti moja liliuzwa kwa bei ya 2,000/- hadi 5,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

UCHUMI

# Sheria kuweka mazingira bora sekta huduma ndogo za fedha

- Itaweka nidhamu, uwazi katika Saccos, Vikoba
- Riba tata, fedha kuibwa kwenye vibubu kukoma
- Faini, vifungo kwa wakiukaji zawekwa bayana




Chama cha kuweka na kukopa katika tukio la kuwezeshwa.

**Na Theodatus Muchunguzi**

KUKOSEKANA kwa sheria ya kusimamia, kuratibu na kuendelea sekta ndogo ya fedha kwa muda mrefu nchini, kumesababisha huduma kutolewa kiholela, huku watumiaji na watoa huduma wakiathirika.

Sekta hiyo inatajwa kuwa na umuhimu mkubwa kwa Watanzania wengi ambao wanaitumia kupata huduma za fedha. Kwa mujibu wa Naibu Kamishna wa Idara ya Maendeleo ya Huduma Ndogo za Fedha wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dionisia Mjema, takribani asilimia 80 ya Watanzania wanatumia huduma hizo.

Kutokuwapo kwa sheria hiyo tangu Uhuru, huduma zimekuwa zikitolewa katika mazingira yasiyo rafiki, huku watumiaji wa huduma hizo wakijikuta wametapeliwa. Kwa mfano, kuna waliopoteza mamilioni baada ya kushindwa kuvuma mbegu walizozipanda katika Deci na wengineo.

Pia kuna watoa huduma ambao wamekuwa wakiathirika kutokana na kuwakopesha watumiaji, lakini wateja hao hawarejeshi mikopo sababu ikiwa wakopeshaji kutokuwa na taarifa sahihi za wakopaji, hivyo wakati mwingine kuingia mitini.

> **"Pia kukosekana takwimu na taarifa tajwa na kusababisha Serikali kutojua mchango wa sekta ndogo ya fedha katika uchumi wa Taifa.**

Baada ya kubaini kasoro zote zilizokuwa zikiathiri sekta hiyo na kushindwa kuboreka na kuwa endelevu, serikali hatimaye ilianza kuchukua hatua kadhaa kwa ajili ya kuziba mapungufu hayo.

Lengo la serikali wakati wa kuanzisha mchakato huo mwaka 2007 lilikuwa ni kuitambua sekta hiyo, kuisimamia, kuiratibu, kuiendeleza na kuiwezesha ili iwasaidie wananchi katika kujikwamua na umaskini. Mchakato huo ulianza rasmi mwaka 2012 kwa utafiti na kukamilika mwaka 2018 ilipotungwa rasmi sheria hiyo kisha kufuatiwa na utungwaji wa kanuni zake mwaka 2019.

Kanuni hizo ambazo zilitungwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), zimejikita katika maeneo mengi kwa kuweka masharti kuanzia usajili na utoaji wa leseni kwa madaraja yanayojuhusisha na utoaji wa huduma ndogo za fedha.

Zinaweka mazingira ya kuhakikisha kwamba watoa huduma wanatambulika, wanavyoendesha shughuli zao pamoja na kuwa na utaratibu wa kuwa na taarifa za wateja wanaowahudumia..

Sekta ndogo ya huduma za fedha inajumuisha watoa huduma katika madaraja manne. Daraja la kwanza linahusisha taasisi zinazopokea amana wakiwamo wakopeshaji binafsi wakati daraja la pili linahusisha taasisi za huduma ndogo za kifedha zisizopokea amana wakiwamo wakopeshaji binafsi, watoa huduma kwa njia za kielektroniki na kampuni za mikopo.

Madaraja haya mawili kwa mujibu wa Shanii Mayosa, Mwanasheria, ambaye ni mjumbe wa kikosi kazi cha utoaji elimu kwa umma kuhusiana na sheria hii ambayo inaelekeza kuwa muda wa mwisho kwa watoa huduma za kujisajili au kuwa na leseni ni Oktoba 31, mwaka huu, yanasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Daraja la tatu ni vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (Saccos). Makundi haya matatu sheria hii inataka kukata leseni kwanza kabla ya kuanza kutoa huduma wakati na daraja la nne linalojumuisha vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha kama Vikoba halibanwi kuwa na leseni bali kujisajili tu. Katika usimamizi na uratibu wa daraja la tatu na nne, BoT, imekasimisha madaraka kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa ajili ya Saccos na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya Vikoba.

Alizungumza mjini Morogoro wiki iliyopita wakati wa ufunguzi wa semina ya wahariri uliyoandaliwa na mamlaka za serikali zinazohamasisha umma kuhusu sheria hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James, alisema changamoto zilizoathiri usimamizi, udhibiti na ustawi wa sekta ndogo ya fedha ni taasisi za huduma ndogo za fedha kutoa mikopo kwa wananchi kwa vigezo na masharti magumu hivyo kusababisha madhara kwa wananchi, ikiwamo viwango vikubwa vya riba na tozo, kukosekana kwa uwazi wa masharti ya mikataba na mikopo.

Katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Kamishna wa Idara ya Maendeleo ya Sekta ya Fedha nchini, Dk Charles Mwamwaja, James alitaja changamoto nyingine ni utoaji holela wa mikopo uliosababisha limbikizo la madeni kwa wateja, utaratibu usiofaa wa ukusanyaji wa madeni unaosababisha wananchi kupoteza mali zao na kujitokeza kwa baadhi ya wananchi wasio waaminifu na wanaotumia mwanya wa kutokuwapo kwa sheria mahsusi kutoa huduma ndogo za kifedha.

Kwa mujibu wa james, mambo mengine yaliyoathiri ni kuwapo kwa baadhi ya taasisi za huduma ndogo za fedha zisizotoa gawio au faida kwa wanachama au wateja wanao weka fedha kati ya asilimia 25 hadi 30 kama dhamana ya mikopo na ukosefu wa takwimu au taarifa sahihi za uendeshaji wa taasisi za watoa huduma ndogo za fedha.

Pia kukosekana takwimu na taarifa tajwa na kusababisha Serikali kutojua mchango wa sekta ndogo ya fedha katika uchumi wa Taifa. Aidha alisema tatizo jingine lililobainika ni ukosefu wa utaratibu wa kuwalinda watumiaji wa huduma ndogo za fedha na kuwapo kwa mianya ya utakatishaji wa fedha haramu kutokana na taasisi za huduma ndogo za fedha kutokuwa na utaratibu wa kisheria unaozitaka kutekeleza matakwa ya sheria ya udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu.

Katibu Mkuu huyo kadhalika, alibainisha kuwa Wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari watafikisha elimu hiyo kuhusu sheria na kanuni kwa makundi mengine mbalimbali ya kijamii ili wananchi waweze kutumia huduma ndogo za kifedha kwa weledi na kusaidia katika kupunguza umaskini.

Kwa upande wake, Dk. Mwamaja, anasema lengo la serikali ni kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kunufaika na rasilimali nyingi zilizopo nchini kupitia fursa za kiuchumi na kwamba hilo litawezekana kwa kutumia sekta ndogo ya huduma za fedha.

Dk. Mwamaja anasema kuna umuhimu mkubwa wa kuwakumbusha wananchi kuzitumia huduma ndogo za fedha kufanya uwekezaji na kwamba fedha hazina thamani bila kuziwekeza.

"Halmashauri zina wataalamu

UCHUMI

# Sheria kuweka mazingira bora sekta huduma ndogo za fedha

ambao wanaweza kuwasaidia kuwaendelea na kwa kuzitumia fursa hizi zitawasaidia kuongeza kipato kuondokana na umaskini kwenye halmashauri zetu 185 nchini," anasema Dk. Mwamaja.

"Sekta hii ni pana, lakini pia zipo fursa nyingi zinazotolewa kupitia mabenki, bima, hisa na mifuko ya kijamii, ni lazima wananchi washiriki kwa kuwapa elimu kuwa wakishiriki wanaweza kunufaika kiuchunmi na kuondokana na umaskini," anasema Dk. Mwamaja, na kuongeza kuwa jambo la msingi ni kutolewa kwa ujumbe mzuri ambao hauna upotoshaji.

Kutokana na sheria hii kuipa BoT mamlaka ya usimamizi pamoja na kumpa Waziri mwente dhamana ya Fedha na Mipango mamlaka ya uhamasishaji, utelekezaji wa sheria na kanuni zake utaweza kuitambua, kuiboresha, kuiendeleza na kuiwezesha sekta ndogo ya huduma za fedha baada ya utekelezaji wake kuanza Novemba 1, mwaka huu.

Kuna mazuri mengi ya kuiweka katika mstari sekta hii ikiwamo kuwalinda watumiaji na watoa huduma. Kwa mfano kwa upande wa madaraja ya tatu na nne; kwa maana ya Saccos na Vikoba ambayo yalikuwa na changamoto kubwa kanuni zimekuja na dawa ya kuzitibu.

Josephat Kasamalala, mjumbe wa kikosi kazi cha kuhamasisha sheria hiyo kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika, anataja baadhi ya mambo yaliyoko kwenya kanuni hizo kuwa ni kuzitaka Saccos kutoa gawio kwa wanahisa wake, kitu ambacho hakikuwapo katika vyama viongi.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, Saccos zitatakiwa kuongeza mtaji pale itakapotokea chama husika mtaji wake kuanza kupungua. Vile vile, inaweka muda kwa vyama hivyo kuwa na mkaguzi wa hesabu kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

Vikoba navyo vimewekewa kanuni za kuhakikisha kuwa vinakuwa endelevu na vinatoa huduma katika mazingira ya uwazi, tofauti na kabla ya kuja kwa sheria hiyo mpya.

Zahara Msangi, mjumbe wa kikosi kazi cha uhamasishaji wa sheria mpya kutoka Tamisemi, ambayo imekasimiwa mamlaka na BoT kusimamia vyama hivyo, anaeleza kuwa kanuni ya 18 inaziruhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa kukifutia usajili chama chochote kilichosajiliwa na kukaa muda mrefu bila kutekeleza majukumu.

Kanuni pia zinavikataza vikundi hivyo kuwa na matawi, haviruhusiwi kupokea amana na vinatakiwa kufungua akaunti benki kwa ajili ya kumbukumbu, tofauti na sasa ambapo fedha za wanachama zinatunzwa katika akaunti binafsi au kwenye vibubu.



Wateja wa benki wakipatiwa huduma tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Vikoba navyo vimewekewa kanuni za kuhakikisha kuwa vinakuwa endelevu na vinatoa huduma katika mazingira ya uwazi, tofauti na kabla ya kuja kwa sheria hiyo mpya.**

Msangi anafafanua zaidi kuwa chini ya sheria hii, Vikoba vinatakiwa kuwasilisha taarifa serikalini kila robo mwaka, kutakiwa kufanya uchaguzi wa viongozi, kitu ambacho hakifanyiki sasa, hivyo kusababisha baadhi ya wanakikundi kuwa viongozi wakati wote, na matokeo yake kukosekana uwajibikaji na vikundi kufa.

Kanuni pia zinaitaka mamlaka (Tamisemi) kufuatilia vikundi kwa kuangalia changamoto na kujiridhisha na uendeshaji wa shughuli zao.

Mayosa anasema kuwa kuna adhabu kadhaa zilizoainishwa kwa wale ambao watakwenda kinyume cha sheria hii. Kwa mfano, upande wa Saccos ni faini ambayo si chini ya Sh. milioni 10 na si zaidi ya Sh. milioni 50 au kifungo kisichozidi miaka miwili na isiyozidi mitano. Upande wa Vikoba faini si chini ya Sh. milioni moja au isiyozidi Sh. milioni 10.

Sheria hii imekuja wakati mwafaka, ambao makundi mengi ya jamii yanahitaji huduma za sekta ndogo ya fedha ambazo zina uwazi, kuaminiana na zinazotambulika. Kinachotakiwa ni kwa watoa huduma kuomba leseni ambayo itakuwa inatolewa ndani ya siku 60 na vikundi vya Vikoba kuomba usajili na kusajiliwa ndani ya siku 14.



Kamishna wa Idara ya Maendeleo ya Sekta ya Fedha nchini, Dk Charles Mwamwaja.

Jambo la msingi na muhimu ni kwa kikosi kazi kutoa elimu ya umma kwa wadau na umma kwa ujumla ili kuwapo uelewa kuwa lengo la sheria hii ni zuri la kutambuliwa kwa sekta, kusimamiwa, kuendelezwa na kuwalinda watumiaji na watoa huduma.

UCHUMI

# Rita yaanika mapinduzi yake toka utendaji hadi makusanyo

## • Uandikaji wosia sasa ni foleni • Vyeti watoto; kata, shule, kliniki • Elektroniki yaibua mageuzi mapato



Shughuli ya usajili wa vizazi ilipofanyika mkoani Mara hivi karibuni. **PICHA: MAKTABA**

**Na Maneno Selanyika**

KATIKA kuboresha utumishi wa umma chini ya Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma (Public Service Reform Program), serikali ilifikia uamuzi wa kuboresha Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali, ambayo ndani yake ilikuwa na Kitengo cha Msajili Mkuu.

Lengo lilikuwa kuboresha huduma zitolewazo na idara tajwa, ili thamani ya fedha inayotolewa na serikali, ilingane na huduma zinazotolewa. Mchakato wa kuanzisha wakala ulianza Februari 2003 na ilipotimu Juni 23, 2006 wakala ulizinduliwa rasmi ukipewa jina la Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita).

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Rita, Emmy Hudson, anasema uanzishwaji wa Rita imefanyika chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Sura ya 245 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Desemba 12, 2005.

Anasema kazi zote zilizokuwa zikifanywa na Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali, zikiwamo za usajili wa vizazi na vifo chini ya Msajili Mkuu, sasa zinafanywa na wakala huo.

Anazitaja huduma zinazotolewa na wakala Rita kuwa ni pamoja na kusajili vizazi na vifo na kutoa vyeti vya vizazi na vifo, kutayarisha takwimu za vizazi na vifo, ndoa na talaka, kutoa leseni za kufungisha ndoa kwa viongozi wa dini na kutoa vibali maalum vya kufunga ndoa bila kutangaza siku 21.

Nyingine ni kutoa vibali ili kuruhusu ndoa ifungwe mahali maalum mfano katika hoteli, hospitali, na hata kama watahitaji kufunga ndoa mahali pengine popote zaidi ya hizo zilizotajwa.

> “ **Wakala pia unasajili ndoa na talaka na kutoa nakala za shahada za ndoa na talaka, kutoa shahada ya kutokuwapo na pingamizi la kufunga ndoa kwa raia wa Tanzania anayetaka kufunga ndoa nje ya nchi.**

“Wakala pia unasajili ndoa na talaka na kutoa nakala za shahada za ndoa na talaka, kutoa shahada ya kutokuwapo na pingamizi la kufunga ndoa kwa raia wa Tanzania anayetaka kufunga ndoa nje ya nchi,” anasema.

Kwa upande wa huduma za udhamini, Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu huyo anazitaja huduma hizo kuwa ni kusajili na kutoa hati ya usajili kwa wadhamini wa vyama vya siasa, vikundi, makanisa, misikiti na mali.

Huduma nyingine ni kusimamia mali isiyokuwa na mwenyewe au ya watu walio chini ya umri wa utu uzima (miaka 18), kusimamia mirathi na kuendesha mashauri ya mirathi, ufilisi na udhamini mahakamani, na kutayarisha na kuhifadhi wosia.

Anabainisha kuwa huduma za usajili wa vizazi, vifo na ndoa zinapatikana katika ofisi zote za wakuu wa wilaya nchini zikisimamiwa na Katibu Tawala wa Wilaya.

Anasema huduma nyingine zote zilizobaki, zinapatikana Ofisi ya makao makuu ya Rita jijini Dar es Salaam na ofisi ya Kanda ya Kati Dodoma huku wakiendelea na maandalizi ya kufungua ofisi nyingine katika kanda za kusini, kaskazini na nyanda za juu kusini.

### MAFANIKIO MIAKA 4 YA JPM

Hudson anasema katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, Rita imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutoa huduma tajwa hapo juu kwa wananchi na wadau mbalimbali.

Anasema kuwa ili kuboresha huduma, wakala umekuwa na programu na mikakati mbalimbali kwa lengo la kupanua wigo wa wananchi kupata huduma. Anasema katika uongozi wa Rais John Magufuli, wamekuwa na mkakati wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu (CRVS), uliobuniwa kwa lengo la kuongeza kasi ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu nchini ambayo ni vizazi, vifo, ndoa, talaka, watoto wa kuasili.

Anasema mkakati huo umesaidia kutoa vyeti vya kuzaliwa watoto wa umri chini ya miaka mitano, usajili ukifanywa katika ofisi za watendaji wa kata na vituo vya tiba vinavyotoa huduma za mama na mtoto, na huduma hizo zinapatikana bila malipo.

Anabainisha kuwa mikoa 12 imefikiwa kati ya 15 ambayo mpango huu unatekelezwa nchi nzima na kwa kipindi cha miaka minne, watoto 3,244,034 wamepata vyeti vya kuzaliwa, kulinganisha na watoto 800,460 waliopata vyeti katika kipindi hicho wakati wa uongozi wa serikali ya awamu ya nne.

Hudson pia anasema katika utekelezaji wa mpango wa Mpango wa Usajili wa Watoto wa Umri wa Miaka 5-17, utekelezaji umefanyika katika wilaya 13 katika mikoa ya Mara, Simiyu, Singida, Njombe, Shinyanga na Ruvuma na zaidi ya wanafunzi 335,583 wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa.

Kiongozi huyo wa Rita pia anasema wakala katika kipindi hicho cha miaka minne umeboresha mfumo wa usajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watu wazima kwa kuongeza matumizi ya teknolojia na uhamasishaji kwa wananchi na kwamba wananchi 433,850 wamepata huduma kupitia kampeni za uhamishaji.

“Pia kumefanyika maboresho katika sheria iliyoanzisha wakala. Hatua za kuipitia sheria zilifanyika mnano Septemba 2019, Bunge lilipopitisha marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo ambayo tayari imetiwa saini na Mheshimiwa Rais na sasa kanuni zinaandaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa maboresho hayo.

“Maboresho yaliyofanyika yanatoa nguvu ya kisheria kwa ugatuzi wa majukumu ya usajili kwenda karibu na wananchi, waliko katika ofisi za watendaji wa kata na vituo vya tiba pamoja na matumizi ya Tehama,” anasema.

Hudson anasema mafanikio mengine ni kuzinduliwa kwa Mfumo wa Usajili wa Njia ya Kielekroniki (BRS4G), kulikofanyika Juni 23, 2018. Anasema mfumo huo umefanya mabadiliko katika miundombinu ya mifumo ya Tehama kwenye nyanja mbalimbali za utoaji huduma ikiwa ni pamoja na kuweka vifaa vya kisasa vilivyo na uwezo mkubwa zaidi wa kutunza kumbukumbu na kubadilishana taarifa na mifumo ya taasisi nyingine.

“Kwa sasa huu ndiyo mfumo mama unaotumika katika taasisi na unatumika katika ofisi zote za wilaya Tanzania Bara na ofisi ya makao makuu,” anasema.

Anabainisha kuwa tayari mfumo huo umeunganishwa na mifumo ya Vitambulisho vya Taifa, Idara ya Huduma za Uhamiaji, Daftari la Mpigakura na taasisi nyingine kama Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Baraza Mitihani (Necta), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HELSB) na wako mbioni kuunganisha na mfumo wa Tasaf.

Anasema mafanikio mengine ni kuwezesha ofisi za wilaya kutumia kompyuta, akibainisha kuwa wakati serikali ya awamu ya tano inaingia madarakani ni ofisi 24 tu za wilaya 24 (asilimia 17) zilizolikuwa zinatumia kompyuta katika kuingiza taarifa na kuzalisha vyeti.

Anasema ofisi katika wilaya nyingine zote zilizobaki, zilikuwa zinatumia mashine ya ‘type writer’ ambayo ufanisi wake ni mdogo na haina uwezo wa kutunza kumbukumbu, lakini sasa wamesimika mifumo ya kompyuta katika wilaya zote 142.

Hudson anasema Rita pia imejiunga katika mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ya serikali (GePG) tangu Novemba 2017, na umeiwezesha kuongeza makusanyo yake kutoka wastani wa Sh. bilioni 3.8 mwaka 2014/2015 hadi Sh. bilioni 6.8 mwaka 2018/2019, sawa na ongezeko la asilimia 178.9.





# Wanafunzi watajwa kuathiriwa mitandao

**Na Nebart Msokwa,**
RUNGWE

WANAFUNZI wa vyuo na shule za sekondari nchini wametajwa kuwa ndio kundi linaloathirika zaidi na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii kutokana na kuingia kwenye mawasiliano bila kujua sheria zinazosimamia sekta ya mawasiliano.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Masoko wa Mamlaka ya Mawasiliano nchini (TCRA), Dorice Mlimbila, wakati wa mwendelezo wa kutoa elimu ya matumizi sahihi ya wanafunzi wa Chuo cha Ualimu cha Mpuguso kilichopo wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya.

Alisema kundi hilo huwa linarubuniwa zaidi na kuanza kuandika ama kutuma vitu visivyofaa kwenye mitandao hiyo ya kijamii wakiwa hawajui madhara yake.

Alisema baada ya kubaini tatizo hilo ndio maana taasisi hiyo imeamua kuanza kutoa elimu kwa makundi hayo ambayo ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

"Kwa hiyo lengo hasa la haya mafunzo ni kuwaeleza ni vitu gani wanapaswa kuvifanya na vitu gani hawatakiwi kuvifanya kwa mujibu wa sheria zinazosimamia mawasiliano ya mitandao," alisema Mlimbila.

Alisisitiza kuwa TCRA ndio chombo ambacho kina mamlaka ya kufuatilia mwenendo wa matumizi ya mawasiliano nchini na hivyo lazima ihakikishe kuwa mawasiliano hayo yanafuata sheria. Wakufunzi wa Chuo cha Ualimu Mpunguso, walisema wamekuwa wakipokea kesi nyingi za wanafunzi kuhusiana na ukiukwaji wa maadili katika kutumia mitandao ya kijamii hali ambayo iliwalazimu kufanya utaratibu wa kuwapatia elimu.

Mmoja wa wakufunzi hao, Flora Kangu, alisema kuna kipindi baadhi ya wanafunzi waliunda kundi la kijamii la 'Whatsap', lakini uongozi wa chuo ulipofuatilia ulibaini kuwa kundi hilo halina maslahi kwa wanafunzi hao kutokana na vitu walivyokuwa wanavifanya.

Alisema kundi hilo lilikuwa ni la moja wapo ya mabweni ya wanafunzi hao na kwamba awali walijua litakua linatumika kwa shughuli za maana lakini baadaye wanafunzi hao walikuwa wanatumiana vitu ambavyo sio vya maadili mema.

"Hawa wanafunzi waliunda kundi hilo mhula uliopita, tulipofuatilia tulibaini kuwa vitu wanavyotumiana sio vya kimaadili, walikuwa wanatumiana picha ambazo sio nzuri na walikuwa wanahamasishana kufanya vitu ambavyo sio vizuri," alisema Kangu.

Alisema uongozi wa chuo hicho unaamini kuwa elimu iliyotolewa na maofisa wa TCRA itawasaidia wanafunzi hao kuepuka kufanya makosa ya kimtandao.

Nao baadhi ya wanafunzi wa chuo hicho walisema elimu waliyoipata itawasaidia kuepuka kufanya makosa ambayo yatawagharimu maisha yao endapo watafikishwa mahakamani.

Mmoja wa wanafunzi hao, Charles Daniel, alisema maofisa wa TCRA waliwaeleza kuwa endapo mtu atashtakiwa kwa makosa ya mtandao, anaweza kufungwa jela ama kulipa faini ambayo ni kubwa.

Mkuu wa TCRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Asajile John, alisema Mamlaka hiyo inalo jukumu la kuhakikisha watumiaji wa mawasiliano ya mitandao wanapata huduma bora.

Alisema huduma bora ni pamoja na kuwa na matumizi sahihi ya mitandao hiyo ikiwamo kutafuta fursa za kiuchumi badala ya kutumiana matusi na picha zisizofaa.



Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akinunua mahitaji mbalimbali ya nyumbani katika Soko la Matola, jijini Mbeya juzi. **PICHA: MICHAEL MSOMBE**

# Takwimu kikwazo utengaji maeneo wafugaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UKOSEFU wa takwimu sahihi za mifugo kwenye vijiji kumetajwa kuwa moja ya sababu za Serikali za Vijiji kushindwa kutenga maeneo ya malisho yanayokidhi mahitaji ya wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini, hivyo kusababisha migogoro ya wafugaji na wakulima kuendelea.

Hayo yalisemwa na wadau wa mifugo mkoani Mbeya wakati wa mkutano wenye lengo la kujadili matatizo yanayoikabili sekta hiyo pamoja na njia za kuzitatua ili kuiendeleza kwa maslahi ya taifa.

Mkutano huo uliwakutanisha maofisa mifugo wa kata zote za Jiji la Mbeya, Watendaji wa Halmashauri na Maofisa kutoka katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya, Hassan Mkwawa, alisema takwimu za mifugo ni muhimu wakati wa kupanga matumizi bora ya ardhi katika eneo lolote nchini.

Alisema maeneo mengi kwenye vijiji yanatengwa kwa ajili ya mifugo, lakini baada ya muda yanaonekana ni madogo kutokana na kutengwa bila kuwa na takwimu sahihi ya mifugo ya maeneo husika.

"Sasa hivi maeneo mengi yananunuliwa na watu binafsi na hivyo kufanya maeneo yanayomilikiwa na vijiji kupungua, sasa ni vizuri tukawa na takwimu sahihi za mifugo ili tutatuwe tatizo hili la upungufu wa malisho," alisema Mkwawa.

Alisema kitendo cha maeneo ya malisho kutotosheleza mahitaji ya mifugo ndio chanzo cha wafugaji kuingiza mifugo yao kwenye maeneo ya wakulima na hivyo kuzua migogoro ambayo imekuwa ikisikika katika maeneo mbalimbali nchini.

Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani kutoka katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Angelo Mwilawa, alisema wizara hiyo imejipanga kutoa elimu kwa wafugaji ili wafuge kisasa na kwa tija kuliko ilivyo sasa.

Alisema lengo la elimu hiyo ni kutaka wafugaji wafuge mifugo michache ambayo inaendana na malisho yaliyopo badala ya kufuga mifugo mingi ambayo inakuwa haina ubora na hata tija yake ni ndogo.

"Tunatoa elimu ya namna ya kuboresha nyanda za malisho na kutumia mbegu bora za malisho, na tutawafundisha wafugaji namna ya kuhifadhi maeneo yao ili sasa wafuge kisasa na wapate tija zaidi," alisema Mwilawa.

Alisisitiza kuwa sekta ya mifugo ni miongoni mwa sekta zinazoliingizia taifa fedha nyingi za kigeni na hivyo ni lazima juhudi zifanyike za pamoja ili kuiboresha.

Hata hivyo baadhi ya wafugaji waliohudhulia mkutano huo, walisema elimu ya namna ya kufuga kisasa ni muhimu kwao kwa sasa kutokana na kukerwa na migogoro ambayo imekuwa ikiibuka.

Mmoja wa wafugaji hao, Dishon Kalonga, alisema wanahitaji kupatiwa elimu ambayo itawawezesha kuwa na mifugo michache inayoendana na maeneo yao ya malisho.

# Chalamila aendeleza kibano kwa wanafunzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewatahadharisha wanafunzi wa shule za sekondari mkoani humo wanaoharibu kwa makusudi miundombinu ya shule kuwa atawashughulikia kama alivyowafanya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kiwanja wilayani Chunya.

Alitoa tahadhari hiyo juzi alipofanya ziara ya kutembelea shule mbalimbali ambazo zimewahi kukumbwa na majanga ya kuungua na moto ambapo alisema baadhi ya maeneo moto huo ulisababishwa na wanafunzi.

Akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondai Usongwe, Chalamila, alisema shule yoyote ambayo wanafunzi watachoma miundombinu ataamuru vyombo vya dola kuwavamia na kuwashughulikia ili kuwa fundisho kwa wengine.

"Nimeona niwatambulishe hawa jamaa waliovaa magwanda ili muwajuwe, siku mkichoma shule, wanajeshi watatoka upande wao, polisi upande wao, maaskari Magereza watatokea upande wao na watawaweka chini ya ulinzii," alisema Chalamila.

Alisema wanafunzi wa Shule ya Kiwanja waliochoma mabweni watano kati yao watano tayari wapo jela na watatoka baada ya miaka mitano na kwamba wakitoka jela bado watapata adhabu nyingine.

Alisisitiza kuwa serikali inatumia fedha nyingi kutekeleza Sera ya Elimu bila malipo na hivyo haitamvumilia mwanafunzi yeyote ambaye ataharibu miundombinu kwa makusudi.

Aliwatahadharisha pia wanafunzi wenye tabia mbaya ambao wanavuta bangi na ambao wanashiriki mapenzi wakiwa bado wanasoma kitu ambacho alisema atawashughulikia.

Chalamila akiwa ameongoza na wajumbe mbalimbali wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, alitembelea shule ambazo zilipata madhara ya moto ikiwamo, Panda Hill na Usongwe ambazo zipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na Harison Uwata Girls ambayo ipo upande wa Jiji la Mbeya.





# Mawaziri SADC kujadili madhara ya maafa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAWAZIRI wanaoshughulikia maafa kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), wanatarajiwa kujadili namna ya kuwekeza katika kupunguza madhara ya maafa yatokanayo na ukame na mafuriko ili kuondokana na matumizi ya fedha za maendeleo kukabiliana na hali hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Wenye ulemavu, Jenista Mhagama, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano wa kwanza wa mawaziri hao utakaofanyika Februari 18 hadi 21, mwaka huu, visiwani Zanzibar.

Alisema baadhi ya nchi wanachama ikiwamo Comoro, Malawi, Msumbiji na Zimbabwe kwa mwaka 2019 zilipata mafuriko yaliyosababishwa na vimbunga Idai na Kenneth na kuzigharimu kukabiliana na hali hiyo.

Alibainisha takribani Dola za Marekani bilioni 10 zilitumika kurejesha miundombinu huku gharama za misaada kukabiliana na madhara zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 323.

"Ili kupunguza gharama kubwa katika urejeshaji wa hali hiyo, ndio maana katika mkutano huu wa SADC tutajadiliana namna ya kuwekeza katika kupunguza madhara ya maafa, kwa kuwa gharama za usimamizi wa maafa kama ya ukame na mafuriko huzilazimu nchi kuelekeza rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo," alisema.

Alieleza kuwa fedha hizo badala ya kutumika kwenye shughuli za maendeleo zinatumika kukabiliana na hali hiyo.

Mhagama alisema nchi nyingi za ukanda huo zimekuwa zikiathiriwa na majanga ya asili mara kwa mara na kusababisha madhara makubwa.

"Tutakumbuka pia ukame wa mwaka 2016 ambao uliathiri takribani watu milioni 40 katika ukanda huu na kusababisha ukosefu wa chakula, idadi hii iliongezeka hadi watu milioni 41.6 katika nchi 13 kwa msimu wa 2018/19," alisema.

Alisema hali hiyo imekuwa ikichangia kuduma za ukuaji wa uchumi wa kikanda, hivyo hawana budi kuchukua hatua kwa pamoja za kupunguza madhara, kuimarisha utayari wa kikanda na uwezo wa kukabiliana na maafa.

Kwa upande wa Tanzania, Mhagama alisema, serikali imeanza kufanya tathmini ya athari ya mvua kwenye mikoa mbalimbali nchini na mkoa wa Tanga ukiwa tayari umeshafanyiwa.

Alitaja mambo mengine yatakayojadiliwa kuwa ni pamoja na kupitisha mkakati wa kujiandaa na kukabiliana na maafa wa kikanda 2016 -2030, kujadili na kuridhia mfumo mkakati wa ustahimilivu wa kikanda 2020/25.

"Kupokea taarifa za maendeleo ya utekelezaji wa mkakati wa mabadiliko ya tabia nchi na mpango kazi wake, mpango wa pamoja wa mazoezi ya nadharia ya kukabiliana na dharura, utafiti na njia mbadala za kukabiliana na majanga katika kutoa huduma za kibinadamu, urejeshaji wa miundombinu kutokana na majanga ya asili," alisema.




Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, akizungumza wakati wa kufungua mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Usimamazi wa Bima nchini (TIRA), jijiji Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TCRA yawanoa waandishi wa habari

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Mawasiliano nchini (TCRA) Kanda ya Kati, imewataka waandishi wa habari kuzingatia kanuni za taaluma ya habari ili kutoa taarifa zenye weledi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui wa TCRA, Joseph Mapunda, wakati akifungua mafunzo ya waandishi wa habari, Kanda ya Kati uliofanyika jijini hapa.

Mapunda alisema taaluma ya habari ni mhimili wa nne hivyo wanapaswa kuusimamia ipasavyo kwa kutoa taarifa zenye mashiko. Naye mwandishi mkongwe, Abdul Ngalawa, alisema mafunzo kwa wanahabari wa vyombo vya habari jinsi ya kuripoti taarifa mbalimbali za uchaguzi na nyingine ni muhimu kwa kuwa yanawajengea uwezo wa kufanya kazi kwa weledi.

Alisema matumizi ya teknolojia yamesababisha ongezeko la vyombo vingi vya habari nchini hivyo kuhitaji mafunzo mara kwa mara.

"Hivi sasa vyombo vya habari ni vingi sana vinafikia 450 hivyo TCRA imeona vema kutoa mafunzo haya ili kuepusha wao kukiuka miongozo na taratibu katika majukumu ya kazi zao za kila siku," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa TCRA, Kanda ya Kati, Antonio Manyanda, alisema katika uchaguzi mkuu wa viongozi mbalimbali mamlaka hiyo imeona kuna umuhimu wa kupata mafunzo.

Manyanda alisema walianza kutoa mafunzo Kigoma, Tabora na hivi sasa Dodoma na baadaye watamalizia Morogoro ili kuhakikisha wanahabari wote wanapata mafunzo ya namna ya kutoa taarifa.

Alisema TCRA inasimamia vitu vingi hivyo ni vyema mafunzo hayo yazingatiwe ili kujiweka sawa kabla ya uchaguzi kuanza.

"Mafunzo haya yatakuwa endelevu lengo ikiwa ni kutaka kuwa na wanahabari walio imara na wenye uwezo wa kutoa taarifa mbalimbali kwa jamii," alisema.

# Kaya 250 Kongwa zapata msaada

**Na Mwandishi Wetu,** KONGWA

CHAMA cha Msalaba Mwekundu (Red Cross), kimetoa msaada wa vifaa mbalimbali kwa kaya zaidi ya 250 Wilaya ya Kongwa zilizoanguka kutokana na mvua.

Vitu hivyo ni pamoja na magodoro, mablanketi na vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 30.

Akikabidhi msaada huo kwa Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejembi, Rais wa chama hicho nchini, David Mwakiposa, alisema msaada huo utapunguza makali ya maisha kwa waathirika wa maafa hayo katika kata tatu za wilaya hiyo.

Mwakiposa alisema kuanguka kwa kaya hizo kumesababisha watu kupoteza makazi, vyakula, mavazi na kuharibika kwa miundombinu, jambo linalohitaji nguvu ya pamoja kuwasaidia.

Hata hivyo, alisema chama hicho mkoa kitaendelea kufuatilia kwa karibu maisha ya watu hao katika kipindi hicho cha masika ili kushauri na kuhakikisha wananchi hawakosi mahitaji ya kibinadamu.

Alitaja kata zilizokumbwa na maafa hayo kuwa ni Mkoka, Mtanana na Sagala.

Akipokea msaada huo, Ndejembi alisema utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza uchungu na ugumu wa maisha kwa wananchi huku akiomba taasisi mbalimbali kutoa misaada zaidi.

Ndejembi alisema maeneo yaliyokumbwa na tatizo hilo, kwa sasa watu wanaishi katika taasisi na nyumba za majirani jambo ambalo limesababisha mrundikano wa familia ambao ni hatari kwa afya zao.

"Nimekabidhiwa msaada huu ambao naona umekuja kwa wakati muafaka, mimi na Mkurugenzi wangu Dk. Omary Mkulo, tutafikisha vifaa hivi kwa muda muafaka na uzuri madiwani wa maeneo husika wapo," alisisitiza Ndejembi.

Aliwataka wakazi wa maeneo hayo kutokata tamaa na kwamba licha ya kubomolewa nyumba zao, lakini watumie mvua hiyo kwa shughuli za kilimo.

Alisema Dodoma ni miongoni mwa mikoa ambayo imeathiriwa na mvua kubwa ya mwaka huu kwenye maeneo mbalimbali.

# 'Zanzibar chimbuko la lugha yetu ya Kiswahili'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, amesema lugha ya Kiswahili asili yake ni Zanzibar na ni miongoni mwa nchi ambayo wananchi wake wanazungumza lugha hiyo kwa ufasaha mkubwa.

Pembe alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Chakechake, Suleiman Sarahani Said, aliyetaka kujua nchi gani duniani wananchi wake wanazungumza Kiswahili kwa ufasaha mkubwa.

Alisema utafiti mbalimbali umefanywa na kubaini kwamba Zanzibar ndiyo chimbuko la lugha ya Kiswahili na wananchi wake wakiitumia lugha hiyo kuwa ni ya kwanza wanayozungumza.

Alisema juhudi mbalimbali zimechukuliwa katika kuendeleza na kukuza lugha hiyo ikiwamo kusomeshwa kuanzia maandalizi, msingi pamoja na sekondari hadi vyuo vikuu.

Alisema katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), tayari shahada ya ngazi za juu ya Uzamivu inatolewa kwa wanafunzi wanaohitimu Kiswahili ikiwa huu ni mwaka wa pili.

"Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika mikakati ya kukikuza Kiswahili na kukiendeleza tumekifanya Kiswahili kuwa ni lugha ya lazima kufundishwa shuleni katika ngazi ya maandalizi hadi msingi na sekondari," alisema.

Alisema juhudi zinachukuliwa kwa ajili ya kuona kwamba lugha ya Kiswahili haipotoshwi.

Alieleza kuwa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki zimeifanya Zanzibar kuwa ndiyo makao makuu ya lugha ya Kiswahili.

"Makao makuu ya lugha ya Kiswahili kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki yamewekwa Zanzibar ikiwa ni ushahidi tosha kwamba Zanzibar ndiyo kitovu cha lugha hiyo," alisema.

# Ataka miti kufanyiwa utafiti dawa za binadamu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TAASISI ya Utafiti ya Afya ya Zanzibar, imetakiwa kutumia mimea ya miti tofauti kwa ajili ya kufanya utafiti wa maradhi yanayowasumbua wananchi na kusababisha vifo.

Hayo yalisemwa na Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni, Yussuf Hassan Iddi, wakati akichangia taarifa ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi iliyowasilishwa na Mwenyekiti wake, Mwanaidi Kassim Mussa.

Alisema zipo dawa za mimea na mizizi ya miti mbalimbali ambayo imekuwa ikitoa tiba nyingi na baadhi ya watu kutoka nje ya nchi hufika Zanzibar kutafuta matibabu hayo.

Alisema katika Msitu wa Hifadhi ya Taifa huko Ngezi Pemba, upo mti aina ya mjafari ambao magome yake hutibu maradhi mbalimbali na baadhi ya watu hutoka Dubai na kwenda Kisiwani Pemba kutafuta mti huo.

"Mjafari ni maarufu na mjarabu kwa kutibu maradhi mbalimbali sugu yanayowasumbua wananchi wengi ikiwamo homa, malaria pamoja na tumbo la 'zingizi' ambalo huwasumbua wanawake wanapoingia katika hedhi.

Aliutaja mti mwingine unaojulikana kwa jina la Msoo ambao hutumiwa na waganga wa tiba ya kienyeji kwa ajili ya tiba kwa wanaume waliopungukiwa nguvu za kiume na kurudisha matumaini katika ndoa zao. "Mti aina ya msoo unategemewa sana na wanaume wengi kwa sababu hurudisha matumaini ya nguvu za kiume kwa watu wenye matatizo ya aina hiyo," alisema.

Alisema mti mwingine ni mlazalaza ambao husafiriwa na wananchi wengi kwa sababu uwezo wake mkubwa ni kutuliza ndoa zinazoyumba baada ya kujitokeza tofauti kwenye nyumba.

"Mti huu unawaniwa sana na waganga wa kienyeji kwa sababu unatumika kwa ajili ya kurudisha matumaini katika ndoa yenye misukosuko na tishio la kusambaratika," alisema.

Mwakilishi huyo alisema kwa mujibu wa taarifa walizopewa na wafanyakazi wanaolinda hifadhi ya msitu wa Ngezi, baadhi ya miti yenye uwezo wa kutoa tiba mbalimbali hivi sasa ipo katika tishio la kutoweka. "Ipo baadhi ya miti yenye uwezo wa tiba asilia ipo katika hatari ya kutoweka kwa sababu hakuna juhudi nyingine za kuotesha miti mipya," alisema.

Kauli hiyo iliungwa mkono na Mwakilishi Mussa Ali Mussa wa Jimbo la Ole Pemba, aliyetaka utafiti wa kina ufanyike katika kuwapatia tiba wananchi maradhi yanayowasumbua ikiwamo shinikizo la damu na kisukari.

Alisema maradhi ya kisukari hivi sasa yanaonekana kuwa tishio zaidi hata kuliko Ukimwi kwa sababu yakikupata basi ujue kwamba tayari unanyemelewa na ulemavu wa kukatwa mguu au kifo. "Tunataka ufanyike utafiti unaotokana na tiba ya maradhi haya kutokana na mimea mbalimbali...miti yetu inatoa tiba nyingi, lakini tatizo hatujafanya utafiti wa kina kuhusu uwezo wa kutibu maradhi sugu," alisema.



Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo (kushoto), Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma (wa pili kushoto) na Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Maendeleo ya Wazee, Wanawake na Watoto, Modline Castiko, wakifuatilia kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Akunwa utendaji wenyeviti wanawake BLW

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, amewapongeza wenyeviti wa kamati za Baraza la Wawakilishi ambazo zinaongozwa na wanawake kwa kuonyesha uwezo mkubwa wa matayarisho na uwasilishaji wa ripoti zake kwa ufanisi mkubwa.

Juma alisema hayo baada ya wajumbe kumaliza kuchangia mjadala kuhusu taarifa ya kamati ya ustawi wa jamii ya Baraza la Wawakilishi iliyowasilishwa na Mwenyekiti wake, Mwanaidi Kassim Juma.

Alisema wenyeviti wa kamati za Baraza la Wawakilishi ambao ni wanawake watatu wameonyesha uwezo mkubwa wa kuongoza kamati hizo na hivyo kutoa matumaini kwamba wanawake wanaweza wakiwezeshwa.

Aliitaja Kamati ya Ustawi wa Jamii kuonyesha uwezo mkubwa katika kuzielekeza wizara mbili zinazohusika na kamati hiyo ikiwamo Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

"Nimefurahishwa na uwasilishaji wa taarifa ya kamati ya ustawi wa jamii ya Baraza la Wawakilishi chini ya Mwenyekiti wake Mwanaisha ambaye imezielekeza vizuri wizara mbili kuhusu utendaji na utekelezaji wa majukumu yake," alisema.

Kamati tatu za Baraza la Wawakilishi zinaongozwa na wanawake ikiwamo ya kusimamia ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa chini ya Mwenyekiti wake Panya Ali Abdalla.

Kamati nyengine ni ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale ambayo inaongozwa na Mwantatu Mbaraka Khamis.

# Masauni ataka wapelelezi kunolewa vizuri vyuoni

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, ameagiza wapelelezi waandaliwe vizuri vyuoni kwa sababu wao ndio chanzo cha msongamano wa mahabusi gerezani na kupindishwa kesi.

Masauni alitoa agizo hilo juzi jioni mara baada ya kufanya ziara ya kikazi ya kutembelea Shule ya Polisi Tanzania iliyopo Moshi mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza chuoni hapo, Masauni aliutaka uongozi wa shule hiyo kuhakikisha inafundisha kwa weledi wapelelezi ili kuondokana na upelelezi usio na kiwango na msongamano gerezani.

"Hakikisheni mnatoa mafunzo kwao ili wanapokuja mtaani wafanye kazi kwa weledi na jamii iweze kufaidika na huduma za Jeshi la Polisi.

"Rais John Magufuli alipokuwa akihutubia katika Maadhimisho ya Siku ya Sheria aligusia suala la wapelelezi kuwa chanzo cha mrundikano wa mahabusi katika magereza yetu na mimi hii leo nimetoka Gereza la Arusha nimeongea na wafungwa na mahabusi."

Alisema wafungwa na maabusi wamelalamikia upelelezi wa kesi zao kupindishwa na kibaya zaidi wengine wamehukumiwa vifungo kutokana na upelelezi usio makini.

"Hili ni tatizo kubwa, haiwezekani Rais alalamike kila siku, maagizo ya serikali kwenu mjitahidi kupika vizuri wapelelezi wenu," alisema.

Kaimu Kamanda, Kamishna Msaidizi, Omar Khamis, aliahidi kuyafanyia kazi maagizo hayo ili yalete tija.

Alisema shule hiyo ina wanafunzi 856 na kati yao wanaume 725 na wanawake ni 131 ambao wako katika mafunzo mbalimbali na wote wanaendelea vizuri na masomo.

Katika ziara hiyo, Masauni alipata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ya shule hiyo ikiwamo sehemu za kulala, madarasa uwanja wa paredi, vyumba vya kompyuta na ukarabati wa bwalo la chakula.



Taka zikiwa zimetelekezwa kwenye kituo cha daladala cha Machinga Complex, Karume, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho kinasababisha kero na kuhatarisha afya za wananchi wanaotumia kituo hicho. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Bajeti Moro yajikita huduma elimu, afya

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KAMATI ya Ushauri Wilaya ya Morogoro, imepitisha bajeti ya Sh. bilioni 75.3 kwa mwaka wa fedha 2020/2020, ambapo pamoja na mambo mengine, vipaumbele vikiwa elimu na afya.

Mchumi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Sadoth Kaijage, alisema hayo wakati akiwasilisha bajeti kwa wajumbe wa kikao cha kamati ya ushauri ya wilaya. Kikao hicho kiliendeshwa na Katibu Tawala wa Wilaya ya Morogoro, Ruth John kwa niaba ya mkuu wa wilaya hiyo, Regina Chonjo.

Kaijage, alisema katika mwaka wa fedha 2020/2021 halmashauri inakisia kukusanya kiasi cha Sh. bilioni 8.4 ambapo shilingi milioni 498.8 ni uchangiaji wa huduma za afya, huku shilingi milioni 271.7 ni uchangiaji wa ada za wanafunzi kutoka katika vyanzo vya ndani.

Alisema kiasi hicho ni ongezeko la Sh. bilioni 1.7 ambayo ni sawa na asilimia 26.43 ya makadirio ya mwaka 2019/2020 ya kiasi cha Sh. bilioni 6.7.

Alisema katika mwaka wa fedha 2020/2021 halmashauri inatarajia kupokea kiasi cha shilingi bilioni 7.4 kutoka Serikali Kuu na wahisani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ambapo serikali kuu inatarajia kuchangia shilingi bilioni 5.8 wakati shilingi bilioni 1.6 ni fedha za nje.

Hata hivyo, alisema katika kuhakikisha mapato yanakusanywa mwaka ujao wa fedha, mikakati iliyowekwa ni kupitia upya mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa mapato kwa kuboresha maeneo ambayo yana mapungufu.

Pia kuendelea kuwashirikisha wadau katika kukusanya mapato, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kubaini mianya inayovujisha mapato, kupitia upya sheria ndogo za mapato na kutumia mifumo ya kielektroniki katika vyanzo vyote vya mapato.

Akichangia hoja ya ukusanyaji wa mapato mjumbe wa kikao hicho, Ismail Rashid Ismail aliipongeza Manispaa hiyo kwa ujenzi wa soko la kisasa na ukarabati wa Mto Kikundi na kushauri eneo la kikundi katika kata ya Sultan Area palipouzwa viwanja kuna eneo lilibaki lijazwe kifusi na litumike kama stendi ya bajaji ili kusaidia usafiri kwa wafanyabiashara na wanunuzi watakaokuwa wanafika kupata mahitaji katika soko hilo.

Naye Elizeus Rwegasira, alishauri kupunguza bei pendekezwa ya vioski vya soko kuu ambapo vioski vya juu vimependekezwa kulipiwa kodi ya Sh. 200,000 na vya chini Sh. 300,000, na kueleza endapo gharama zitakuwa kubwa, wananchi watashindwa kupanga na vitabaki wazi na kuifanya halmashauri kukosa mapato.

# Vijana wafagilia ufadhili mradi kukuza ujuzi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

VIJANA wanaopata mafunzo ya ufundi kupitia mradi wa uwezeshaji vijana kujiajiri unaofadhiliwa na Ubalozi wa Denmark kupitia Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (LIC), wameahidi kuendeleza ujuzi watakaopata kujiajiri na kuwafundisha vijana wengine.

Walisema hayo walipozungumza na waandishi wa habari waliotembelea kiwanda cha kutengeneza mashine za kuchakata mazao ya kilimo ikiwa ni sehemu ya ziara ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, kukagua miradi ya maendeleo iliyolenga kuwakwamua vijana kiuchumi mkoani Dodoma hivi karibuni.

"Tunaishukuru Serikali na Ubalozi wa Denmark kupitia mradi wa LIC kwa kuufadhili mradi ambao unakwenda kutuondolea tatizo la ajira kwani utatufanya kujiajiri kupitia mafunzo tunayoendelea kuyapata hapa," alisema Andrea Masanika, mmoja wa wanafunzi wanufaika.

Alisema mradi umemwezesha kupata mafunzo ya uchomeleaji vyuma fani ambayo itakuwa mwongozo katika kuendesha maisha yake na pia atakwenda kutoa ujuzi kwa vijana wengine endapo atafanikiwa kupata fedha za kufungua karakana yake.

"Tunaiomba serikali kupitia halmashauri zetu zituwezeshe kuanzisha karakana zetu ambazo zitakuwa sehemu ya kujipatia ajira na pia chuo kwa vijana wengine kupata ujuzi mbalimbali," alisema Masanika. .

"Niwaombe vijana wenzangu wachangamkie fursa za miradi ya maendeleo inapotangazwa ili wawe sehemu ya wanufaika wa miradi hiyo ambayo imelenga kuinua uchumi na kutengeneza ajira kwa vijana," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda hicho, Joel Ngosso, alishukuru Serikali kupitia Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) kwa kufanikisha mradi huu kukamilika kwani kupitia wao LIC ikamwona na kumwezesha kufikia ndoto yake.

"Ndoto yangu ni kuwapatia vijana ujuzi nilionao wa kutengeneza mashine ili iweze kuwasaidia katika kujiajiri hali itakayosaidia kupunguza tatizo la ajira nchini," aliema Ngosso.

Alisema LIC imeniwezesha kuniunganisha na umeme mkubwa, kupanua karakana ya kufundishia, vifaa vya ufundi na mitambo ya kufundishia ufundi hali ambayo imenipa hamasa ya kujitoa zaidi katika kufundisha.

Naye Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, alisema Baraza lake litaendelea kuhamasisha vijana katika kuchangamkia na kuibua fursa zinazojitokeza ili waweze kunufaika na miradi mbalimbali ya maendeleo inayoungwa mkono na wafadhili.

"Jukumu letu kama baraza ni kufanya uratibu na usimamizi miradi mbalimbali ya maendeleo na kuhakikisha walengwa wa miradi hii wananufaika kwa kuzingatia miradi inavyotaka," alisema Dk. Wanga.

## HABARI KIMATAIFA

## Papa: Waliofunga ndoa hawatakuwa mapadri

**VATICAN, Italy**

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki, Papa Francis, amekataa kuunga mkono pendekezo la kuwakubalia wanaume waliofunga ndoa kuhudumu kama mapadri katika eneo la Amazon.

Uamuzi huo ambao ingawa ungekuwa ni wa eneo la Amazon pekee, ungewapa hasira wahafidhina ambao tayari wanauchukulia uongozi wa Papa Francis kama wenye misimamo mingi ya wastani.

Miongoni mwa wahafidhina hao ni Kadinali Robert Sarah ambaye mwezi uliopita alichapisha kitabu kilichotetea hatua ya mapadri wa Kanisa Katoliki kutofunga ndoa. Papa mstaafu Benedict wa Kumi na Sita pia alihusika katika uandishi wa kitabu hicho.

Katika waraka uliosubiriwa kwa hamu, Papa Francis hakuzungumza chochote kuhusiana na mapendekezo ya maaskofu wa Amazon kuhusiana na suala la kuwafikiria wanaume walio kwenye ndoa kuwa mapadri na wanawake kuwa mashemasi. **DW**



Miongoni mwa maaskofu wa Amazon ambao waliwasilisha pendekezo kwa Papa la kutaka kuruhusiwa kuoa. **PICHA: REUTERS**

# Walioambukizwa virusi vya corona wafikia 60,000

**BEIJING,** China

CHINA imesema hadi kufikia jana idadi ya watu walioambukizwa virusi vya ugonjwa wa corona nchini humo imefika 60,000 hali inayoendelea kuzua wasiwasi mkubwa nchini humo na ulimwenguni.

Wakati China wakitoa takwimu hizo, maofisa wakuu wa Mkoa wa Hubei ambako ugonjwa huo ulianza wamefukuzwa kazi.

Hatua hiyo imekuja saa kadhaa baada ya Rais Xi Jinping kudai kuwa kuna matokeo chanya katika juhudi za kulidhibiti janga hilo ambalo sasa limewaua zaidi ya watu 1,355. Takwimu hizo zinaweka wasiwasi na zinachochea uvumi kwamba ukali wa ugonjwa huo bado umekithiri.

Tume ya Afya katika Mkoa wa Hubei, katikati mwa China, imetangaza vifo vipya vya watu 242 katika mkoa huo.

Vifo hivyo ni ongezeko kubwa zaidi llinaloshuhudiwa ndani ya saa 24 tangu kuzuka kwa ugonjwa huo Desemba, mwaka jana katika mji mkuu wa mkoa huo wa Wuhan. Wakati idadi ya watu walioambukizwa ikiongezeka, watu 10,000 wamewekwa katika karantini katika nchi ya Vietnam baada ya matukio sita kugunduliwa kwenye vijiji kadhaa, ikiwa ni mara ya kwanza kwa hatua kama hiyo kuchukuliwa nje ya China.

Jimbo la Hubei ambalo linachukua zaidi ya asilimia 80 ya maambukizi nchini China, kwa sasa linajumuisha matukio ya virusi vilivyogunduliwa katika vituo vya afya.

Hii inamaanisha ni pamoja na zile zinazoonyesha dalili, na kuwa na mashine za CT-Scan inayoonyesha mapafu yaliyoathirika, badala ya kutegemea tu vipimo vya Nucleic acid.

Kati ya vifo vipya 242 vilivyotokea mjini Wuhan, 135 ni vile vilivyotambulika kwa vipimo vya kliniki. **RFI**


SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

**TANGAZO KWA WAPANGAJI WA NYUMBA ZA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA**

Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) linapenda kuwatangazia Wapangaji na umma kwa ujumla kuwa limeanza zoezi la kuhakiki Wapangaji wake wote nchi nzima. Zoezi hili limeanza wiki hii na litaendelea muda wote hata siku za mwisho wa wiki na sikukuu ili liweze kukamilika mapema mwezi Machi 2020.

Ili kulifanya zoezi hili kuwa na mafanikio makubwa, Wapangaji wote wanatakiwa kutoa ushirikiano kwa Maafisa wa Shirika ambao muda wote watakuwa wamevaa vitambulisho vya kazi. Maafisa hao wa Shirika watapita majumbani au sehemu za biashara ili kuhakiki wapangaji hao kwa lengo la kuboresha taarifa zao.

Wakati wa uhakiki huu, wapangaji wanatakiwa kuwa na nyaraka za utambulisho ambazo ni:-

1. Mkataba wa Upangaji ulio hai
2. Stakabadhi ya malipo ya kodi ya pango ya mwezi husika
3. Nakala ya kitambulisho cha NIDA au kitambulisho cha Mpiga Kura, Hati ya kusafiria na au leseni ya Udereva iliyo hai kwa wapangaji wasiokuwa na vitambulisho vya NIDA.
4. Nyaraka za utambulisho na uthibitisho wa uhai wa kampuni ama taasisi husika kama vile leseni, memorandum and articles of association, and Cerificate of Incorporation.)
5. Stakabadhi ya malipo ya 'nominal rent" ya mwezi husika, Hati ya Upangaji ya muda mrefu "long term lease" ama sub title na nyaraka nyingine yoyote inayothibitisha umiliki binafsi (ex-owners na tenant purchasers).

Shirika linatoa rai kwa kila mpangaji ahakikishe amehakikiwa ili kuepuka usumbufu utakaoweza kujitokeza baada ya zoezi la uhakiki kukamilika. Ni matumaini yetu kuwa wapangaji wote watashiriki zoezi hili kikamilifu.

IMETOLEWA NA:
KITENGO CHA MAWASILIANO NA HUDUMA KWA JAMII NHC MAKAO MAKUU



SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

**TAARIFA KWA UMMA**

Shirika la Nyumba la Taifa linawashukuru wapangaji wake waliokamilisha kulipa kodi na malimbikizo waliokuwa wakidaiwa na Shirika. Aidha, Shirika linawapongeza wapangaji wengine waliokuwa wakidaiwa ambao wamefika katika Ofisi mbalimbali za Mikoa ya Shirika kuomba muda wa kukamilisha kulipa kodi na malimbikizo yao wanayodaiwa.

Hata hivyo, Shirika linapenda kuwatangazia wapangaji wake wote ambao bado wana malimbikizo na wale wote waliohama na madeni wakiwamo watu binafsi, taasisi za umma, wakala za serikali na kampuni binafsi kuwa majina ya wadaiwa hao sugu yataanza kutolewa kwenye vyombo vya habari kuanzia Februari 17, 2020. Baada ya majina ya wadaiwa sugu kutangazwa kwenye vyombo vya habari, Shirika litaanza mara moja kuchukua hatua za kisheria dhidi yao.

Kwa wale wanaofahamu kwamba upangaji wao ulipatikana kwa njia zisizo sahihi wanapaswa kutoa taarifa Makao Makuu ya Shirika ili waweze kuhalalishwa kwa kupewa upangaji.

Epuka usumbufu lipa kodi kwa wakati

**Imetolewa na:**

OFISI YA MAWASILIANO KWA UMMA NA HUDUMA KWA JAMII NHC- MAKAO MAKUU

# TIRA yatakiwa kuongeza ubunifu kufikia watu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, ameliagiza Baraza la Mamlaka ya Usimamizi wa shughuli za Bima Tanzania (TIRA), kuongeza ubunifu katika utendaji kazi wake ili kuwafikia watu wengi kutokana na kufikia asilimia 15 pekee ya watu nchini.

Dk. Kijaji aliyasema hayo jana wakati alipokuwa akitoa hotuba yake ya ufunguzi wa mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka ya usimamizi shughuli za Bima (TIRA).

Alisema hivi sasa watu wengi hawajaingia katika mfumo huo wa bima kutokana na kutokuwa na uelewa wa huduma hiyo.

Vile vile, alisema takwimu za mwaka 2017, zinaonyesha watu wazima milioni 27 ndio waliokuwa wamefikiwa na huduma angalau moja ya bima.

"Kwa hawa watu milioni 27, na kwa takwimu za idadi ya watu wote nchini ambao ni zaidi ya milioni 50 utaona kuwa watu wote waliofikiwa na huduma hii nchi nzima kuwa ni milioni nne pekee," alisema Dk. Kijaji.

Pia alisema sekta ya bima nchini ina mchango mdogo katika Pato la Taifa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita.

"Katika kikao hiki nataka mtafakari na kutoka na majibu kwanini sekta ya bima ina mchango wa asilimia 0.53, katika pato la taifa kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita hali hii ina maanisha kuwa nyinyi Tira hakuna mnacho kifanya kama mmeshindwa niambieni nimwambie na mimi yule mwenye mamlaka juu yangu kuwa hapa ndiyo mmefika mwisho," alisema.

Vile vile, aliwataka wajumbe wa baraza hilo kuhakikisha kuwa wanapojadili utekelezaji wa bajeti iliyopita pamoja na makisio ya bajeti ya 2020/21 waje na majibu ya bidhaa za bima ambazo zitajibu maswali ya makundi yote.

"Lazima TIRA muwe wabunifu kwa kuja na bidhaa za aina mbalimbali kwa wateja katika makundi yote, lazima wakulima wawe na bima yao, wafugaji, wavuvi, wachimbaji wadogo wa madini pamoja na watoto ambao wanakufa kutokana na kukosekana kwa fedha za matibabu," alisema Dk. Kijaji.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza hilo, Dk. Mussa Juma, alisema kuwa wana mikakati ya kuongeza wananchi wanaotumia huduma ya bima angalau moja kufikia asilimia 20 ifikapo mwaka 2021.

"Pia mikakati mingine ni kuhakikisha kuwa tunaongeza ukusanyaji wa mapato, uelewa kwa wananchi kuhusu huduma za bima kwa asilimia 45 ifikapo 2021, kufikia asilimia 30, ya Watanzania wenye bima mwaka 2021," alifafanua Dk. Juma.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akikata keki kuadhimisha miaka 43 ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), katika hafla iliyofanyika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kamati ya Bunge yapongeza uwekezaji SBL

**Na Mwandishi Wetu**

WAJUMBE wa Kamati ya Bajeti ya Bunge, wamepongeza uwekezaji unaofanywa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), unaohusisha upanuzi wa kiwanda chake cha Dar es Salaam.

Kampuni ya SBL inafanya upanuzi wa kiwanda cha Dar es Salaam, moja kati ya viwanda vyake vitatu. Upanuzi huo unaogharimu Paundi za Uingereza milioni 10, utasaidia kuongeza uzalishaji wa bia ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya wateja wa kampuni hiyo.

Akizungumza muda mfupi baada ya kutembelea kiwanda cha Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mahimba Ndaki, alisema, uwekezaji huo utasaidia kutengeneza ajira mpya kwa Watanzania na kuongeza mahitaji ya malighafi za kuzalisha bia kama shayiri, mahindi na mtama jambo ambalo litawaongezea wakulima kipato.

"Uwekezaji wenu endelevu unaenda sambamba na ajenga yetu ya Tanzania ya viwanda. Uwekezaji mkubwa kama huu unatia moyo na unaonyesha namna ambavyo mmejipanga vyema kutumia fursa zilizopo katika Tanzania ya Viwanda. Sisi tunawahakikishia ushirikiano wetu katika shughuli zenu za kila siku," alisema Ndaki.

Kwa upende wake, Mkurugenzi wa Mahusiano kwa Umma wa SBL , John Wanyancha, aliwaambia wajumbe wa kamati hiyo kwamba, upanuzi wa kiwanda hicho upo katika hatua za mwisho za kukamilika na utasaidia kuongeza ajira pamoja na mapato kwa serikali kupitia kodi.

Wanyancha aliongeza kuwa kwa sasa SBL inanunua Shayiri, mahindi pamoja na mtama kutoka kwa wakulima wazawa kwa ajili ya uzalishaji wa bia zake na kwamba mwaka jana ilinunua tani za ujazo 17,000 sawa na asilimia 70 ya mahitaji yote ya malighafi ambayo SBL inatumia kwa mwaka.

SBL pia imeajiri zaidi ya wafanyakazi 700 moja kwa moja na wengine maelfu kwa ajira zisizo za moja kwa moja kupitia mlolongo wa thamani ya biashara zake katika viwanda vyake vya Dar es Salaam, Moshi na Mwanza.

# Ajali Wami yaua mmoja

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

GARI aina ya Toyota Noah lenye namba za usajili T.396 BLE, lililokuwa likitokea Dar es Salaam kwenda Arusha limetumbukia katika Mto Wami uliopo Chalinze, Bagamoyo mkoani Pwani likiwa na watu saba ndani na kusababisha kifo cha mtu mmoja.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema, tukio hilo lilitokea Februari 12 majira ya saa 12 asubuhi katika eneo hilo na kusababisha kifo cha mtu mmoja.

Wankyo alitoa taarifa hiyo jana ofisini kwake na kueleza gari lenye namba za usajili T.729 DNA/T.389 DJX, aina ya Faw, mali ya Tanga General LTD, ikitokea Tanga kwenda Dar es Salam, ikiendeshwa na Habibu Dadi (44), mkazi wa Arusha iligongana na gari namba T.396 BLE Toyota Noah iliyokuwa ikiendeshwa na Abdallah Nocha (35), mkazi wa Bunju jijini Dar es Salam.

Alisema, katika ajali hiyo mtu mmoja aliyetambuliwa kwa jina la Jamilah Kindamba (42), mkazi wa Dar es Salaam alifariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa.

Kwa mujibu wa polisi, inasadikiwa kuwapo na mtoto wa miezi tisa katika ajali hiyo ambaye hata hivyo mwili wake haujapatikana hadi sasa.

Chanzo cha ajali hiyo kinadaiwa kuwa ni dereva wa gari la T. 729 DNA/T.389 DJX, kushindwa kumudu gari lake wakati akiwa kwenye mteremko, kuvuka daraja na kusababisha kutokea kwa ajali hiyo.

Kamanda Wankyo alisema majeruhi wawili waliokuwa katika gari ya Noah pamoja na madereva walifikishwa katika Hospitali ya Jeshi ya Kihangaiko kwa ajili ya matibabu.

**Katika ajali hiyo mtu mmoja aliyetambuliwa kwa jina la Jamilah Kindamba (42), mkazi wa Dar es Salaam alifariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa.**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NYUMBA INAUZWA MIL 70 ARUSHA NGULELO:,** SELF VYUMBA 3 KIMOJA MASTER, SITTING, JIKO NA STORE, INA UMEME âNA MAJI INAFAA KUISHI, FINISHING NA FENSI UNAIMALIZIA.MWENYE NYUMBA **0757 804 970**

**MKOPO WA HARAKA NA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL)** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumaliza tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga: **0758 112 332. Karibu EFL**


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA SHERIA**
**IDARA YA MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya KINONDONI**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NO. 37/2020**

Ombi la **BELINDA E. CHIRYAMKUBI** Usimamizi wa miradhi ya marehemu **ALEXANDER G. NDEMBEKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria Mahakamani wakati wa kusikilizwa kesi mnamo tarehe 19/02/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hii .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

115630302

**TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

Marcean Mayunga anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Nissan pick- up yenye namba za usajili T216ANA Chassis no A000078 na engine no QD32215560

Kwa yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Taarifa ya polisi KAH/ /RB/ 56/2020

1156301

**KUPOTEA KWA HATI MILIKI YA KIWANJA No. 173 BLOCK BLOCK A**

**RAISSA JAMES NTALIKA** anatangaza kupotea kwa hati ya Umiliki wa Kiwanja namba: 173 BLOCK "A" Yombo Vituka-Temeke-Dar es Salaam.

Yeyote atakaeiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **DAR/KIJ/RB/140829/2020**

115629302

**KUPOTEA KWA CHETI**



**NGUSO SEIFF MWINYISHEHE** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha sita chenye index namba **P3888-0513** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ST JOSE TRA CENTRE mwaka 2010. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/122570/2020.**

115629102

**CHETI KIMEPOTEA**



**AGNESS K. RUGARABAMU** anatangaza kupotelewa na cheti cha uuguzi GENERAL NURSING kilichotolewa na **HUBERT KAIRUKI UNIVERSITY** mwaka 2015.

Yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi **DSM/PHQ/RB/136747/2020.**

115629802


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# POGBA ASUBIRIA KWA HAMU KURUDI DIMBANI




**MANCHESTER,** England

PAUL Pogba amesema "hawezi kusubiri" kurudi dimbani kuichezea Manchester United wakati bingwa huyo wa Kombe la Dunia akichukua hatua nzuri kwenye majeraha yake ya enka yakielekea kupona.

Akiwa ameanza katika mechi tano tu za Ligi Kuu hadi sasa msimu huu, Pogba sasa anaonekana anakaribia kutoa huduma yake kwa kocha Ole Gunnar Solskjaer ambaye amemkosa kwa muda mrefu uwanjani.

Pogba aliposti video ikimuonyesha yupo gym Jumatano, huku akiendelea kupona majeraha yake na anatarajiwa kurudi dimbani haraka.

"Wiki nne baada ya kufanyiwa upasuaji, najihisi vizuri," alisema kwenye video hiyo aliyoiposti katika ukurasa wake wa Instagram.

Aliweka picha nyingine nyingi huku akiandika ujumbe uliosomeka: "Siwezi kusubiri kurudi uwanjani."

Solskjaer kikosi chake kimekuwa kikionekana kutokuwa imara kwenye safu ya kiungo kutokana na kukosekana kwa Pogba na kurudi kwake kutakuwa ahueni kubwa kwa kikosi hicho.

Hata hivyo, Pogba anatarajia kurudi uwanjani haraka zaidi tofauti na ilivyotarajiwa hapo awali.

# Ceballos aeleza sababu kuchagua kutua Arsenal

**LONDON,** England

DANI Ceballos anaamini ingekuwa hatari kutua Anfield kama angechagua kujiunga na Liverpool kuliko Arsenal.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania aliondoka Real Madrid na kujiunga na 'Washikabunduki' hao wa London kwa mkopo wa muda mrefu Julai mwaka jana, lakini tu baada ya kuona hangeweza kupata nafasi ya kukichezea kikosi cha Jurgen Klopp ambacho ni mabingwa wa Ulaya.

Ceballos alifikia uamuzi huo baada ya kuona kwamba hangefiti kucheza Liverpool, na akakubali mualiko wa kocha Unai Emery kutua pale London.

"Nilikuwa najisikia fahari kutakiwa na klabu kama Liverpool, lakini niliichagua Arsenal kwa sababu ya Unai Emery na namna gani alivyoweza kunishawishi," alisema Ceballos akiliambia gazeti la Marca.

"Klopp ni kocha mkubwa, lakini unatakiwa kuangalia falsafa ya timu inavyocheza. Kwangu mimi ningekuwa kwenye wakati mgumu zaidi kucheza pale kwa falsafa yao."






# *Salah aachiwa aamue hatima Olimpiki Misri*

**LIVERPOOL,** England

WAKALA wa Mohamed Salah amerudia kusema kwamba hakuna maamuzi yaliyofanyika hadi sasa kama nyota huyo wa Liverpool ataiwakilisha Misri kwenye michezo wa Olimpiki jijini Tokyo, Japan.

Kocha wa timu ya Taifa ya Misri ya umri chini ya miaka 23, Shawky Gharib alithibitisha mpango wake wa kutaka kumchagua Salah kuwa mmoja wa wachezaji watatu wenye umri mkubwa kushiriki kwenye michezo hiyo, ingawa alibainisha kutofanya mazungumzo na mchezaji mwenyewe.

Akizungumza mwezi uliopita, bosi wa 'klabu yake ya Liverpool, Jurgen Klopp alisema "haitakuwa sawa" kama Salah atasafiri kwenda Japan na bado jambo hilo halijafanyika.

Na wakala wa Salah, Ramy Abbas Issa alisema kupitia mitandao ya kijamii akizungumzia kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, angeweza kuchaguliwa kwenye kikosi hicho alisema: "Bado hakuna maamuzi yaliyofanyika."

Kama Salah atatakiwa kuiwakilisha Misri, Liverpool itakuwa bila ya mshambuliaji wake muhimu kwenye maandalizi ya msimu na pengine mwanzoni kwa msimu.

Mechi za michezo hiyo zimepangwa kufanyika Agosti 8, mwaka huu siku ambayo msimu mpya wa Ligi Kuu ya England utakapokuwa unaanza.

HABARI MICHEZO

# NEYMAR HATIHATI KUIVAA DORTMUND




**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR yupo shakani kuichezea Paris Saint-Germain kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano ya timu 16-bora dhidi ya Borussia Dortmund, kwa mujibu wa kocha mkuu, Thomas Tuchel.

PSG ishuka dimbani bila Neymar kwenye mchezo wa Jumatano wa ushindi wa 6-1 dhidi ya Dijon kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la Coupe de France kutokana na Mbrazil huyo kuumia mbavu.

Neymar alibakia jijini Paris wakati mshambuliaji huyo akiendelea kupona majeruhi yake, ambayo aliumia kwenye mchezo dhidi ya Montpellier Februari Mosi na pia alikosa mechi za ushindi za Ligi 1 dhidi ya Nantes na Lyon.

Baada ya kusafiri kwenda Amiens kwenye Ligue 1 Jumamosi, PSG itakwenda Dortmund kwa ajili ya mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya miamba hao wa Bundesliga.

Alipoulizwa kuhusu Neymar, Tuchel aliwaambia waandishi wa habari: "Siwezi kusema kwamba atakuwa fiti kwa asilimia 100 dhidi ya Borussia Dortmund.

"Tutajadiliana Ijumaa, kuangalia uwezekano wa nini kifanyike. Tunaweza tukahatarisha kuwa fiti kwake."

Tuchel aliongeza: "Hatuwezi kufanya maamuzi ya haraka, tunatakiwa kusubiri kuona ni lini atakuwa fiti kurudi uwanjani."

## Conte: Dabi Milan imetumaliza nguvu



**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte anahisi mchezo wa 'dabi' kati ya Inter Milan na AC Milan ulichukua nguvu nyingi zaidi wakati kikosi chake kikipoteza kwenye nusu fainali ya kwanza ya Kombe la Coppa Italia nyumbani kwa Napoli, juzi.

'Nerazzurri' hao walipigana kutoka nyuma na kupata ushindi wa 4-2 dhidi ya Milan Jumapili kwenye mchezo wa Ligi Ku ya Italia, Serie A.

Ilikuwa habari tofauti wakati huu, kwani Inter walishindwa kupata ushindi wakati wakipoteza kwa kufungwa 1-0, shukrani kwa bao la Fabian Ruiz la kipindi cha pili. Akizungumza na televisheni ya Rai baada ya mchezo huo, kocha Conte alisema: "Mchezo wa dabi ulichukua nguvu nyingi za wachezaji wetu.

"Nilifanya mabadiliko matano kutoka kwenye mchezo wa Jumapili, lakini Napoli waliwafunga Juventus, Lazio na Liverpool msimu huu, maana yake ni kwamba wana kiosi bora kabisa. "Kama nilivyosema, baada ya Juventus, Napoli wanakikosi kilichoimarika zaidi kwenye Serie A.

"Gennaro Gattuso alikiandaa vizuri kikosi chake kwa ajili ya mchezo huu. Tulikuwa na nafasi na ingekuwa vizuri tungepata hata sare.

"Wakati unapocheza dhidi ya timu inayozuia zaidi kama hivyo, unatakiwa kuondoa mpira haraka eneo lako kwa ajili ya kutengeneza nafasi."

## *Ziyech rasmi mali ya Chelsea*

**AMSTERDAM,** Uholanzi

KOCHA wa Ajax, Erik ten Hag amethibitisha kwamba, Hakim Ziyech atajiunga na Chelsea mwishoni mwa msimu huu, akibainisha kwamba alimtarajia mshambuliaji huyo nyota kuondoka "mwaka mmoja au miwili iliyopita".

Ripoti za Jumamosi zimebainisha kwamba mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, Ajax na miamba wa Ligi Kuu ya England, Chelsea wamefikia makubaliano ya uhamisho wa euro milioni 45 kwa Ziyech.

Ziyech alitokea benchi wakati wa mchezo wa Jumamosi wa ushindi wa 3-0 dhidi ya KNVB Beker pale Vitesse na Ten Hag alizungumzia hatua iliyofikiwa juu ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 raia wa Morocco.

"Ziyech kwenda Chelsea? Uhamisho ulikuwa unakuja, tulitarajia ungetokea tu," alisema Ten Hag akiiambia Fox Sports.

"Kwa uhakika nilitarajia hili kutoka mwaka mmoja au miwili iliyopita. Na mara zote tulikuwa tunasema: 'Wow, amebaki tena'.


"Tuna furaha kwamba tutakuwa naye hadi mwishoni mwa msimu huu."

Ziyech amehusika moja kwa moja kwenye mabao 166 tangu atue kule Eredivisie msimu wake wa kwanza 2012-13, akichangia mabao 79 na pasi za mwisho 87.

Tangu alipojiunga Ajax akitokea Twente mwaka 2016, Ziyech amefunga mabao 38 ya ligi na 48 kwenye mashindano yote.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MARTIAL AMCHAMBUA MOURINHO MAN UTD

Inaweza kuuma, lakini unataka tu kumuonyesha kwamba unapaswa kuwa uwanjani...

**MANCHESTER,** England

ANTHONY Martial amesimulia jinsi alivyotamani kumthibitishia Jose Mourinho kukosea baada ya kutomkubali kipindi cha msimu wa pili wa Mreno huyo katika kikosi cha Manchester United.

**Wasifu wa Martial kikazi hapo United umekuwa ukiandamwa na kiwango kushuka na kupanda na zaidi wakati Mourinho akiinoa timu hiyo.**

Baada ya kuwa na mwanzo mzuri wa msimu klabuni hapo, Martial alionekana atapiga hatua zaidi kama ilivyokuwa msimu wa 2016-17, akianza mechi 18 za Ligi Kuu ukilinganisha na 29 za mwaka wa hivi karibuni pia ufungaji wake wa mabao uliporomoka kutoka 11 hadi manne.

Tetesi kuhusu Martial kuondoka zilizagaa kabla ya msimu wa 2017-18 na alianza mechi tatu tu za Ligi Kuu kabla ya Novemba, lakini alirejea mwenyewe katika kikosi cha kwanza na kuanza mara kwa mara, akifunga mara tisa na kisha kutengeneza mabao mengine matano.

Mbinu za kuhamasisha za Mourinho zinajulikana vizuri, kama ambavyo amekuwa haogopi kuwakosoa wachezaji hadharani ili kupata majibu, na wakati zikionekana kufanya kazi kwa Martial, amesema angependa matibabu mbadala.

"Ni kweli kwamba ningependa kuambiwa ana kwa ana," Martial aliambia RMC Sport kama sehemu ya kumbukumbu yake kuhusu Mourinho.

"Palikuwa hakuna haja ya hili kuzungumzwa mbele ya kila mtu. Pengine, baada ya hilo, unataka kumthibitishia kukosea."Hakunichezesha wakati wa mechi za kwanza za msimu. Kila wakati niliingia, nilifunga, na kisha alizungumza na mimi, 'Unaona, sasa unaelewa nilichokuwa nakitaka.'

"Inaweza kuuma, lakini unataka tu kumuonyesha yeye kwamba unapaswa kuwa uwanjani."

Martial alianza msimu wa 2019-20 vizuri chini ya Ole Gunnar Solskjaer, lakini alihaha kurejesha kiwango baadaye baada ya kuhamishiwa katika majukumu ya mshambuliaji wa kati kutokana na kukosekana kwa Marcus Rashford.

## ZISIKUPITE

### SANCHO AVUTIA VIGOGO ULAYA

LIVERPOOL inataka kumsajili Jadon Sancho majira haya ya joto kutoka Borussia Dortmund, ambayo itahitaji takriban pauni milioni 100m kwa mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 19, na Manchester City, Manchester United, Chelsea, Real Madrid pamoja na Barcelona pia zinavutiwa naye. ***(Mail)***

### ZIYECH, SANCHO WATIKISA

MANCHESTER United ni klabu mpya inayopewa nafasi zaidi ya kuinasa saini ya Jadon Sancho na Chelsea ikikaribia kufanikisha mpango wa kumsajili kiungo mshambuliaji wa Ajax, Hakim Ziyech, 26. ***(Standard)***

### CHELSEA, UNITED KWA JUDE

CHELSEA na Manchester United zinajiandaa kulipa pauni milioni 35 kwa kiungo wa Birmingham, Jude Bellingham, 16, pamoja na nyongeza ya pauni milioni 15. ***(Sun)***

### MADRID, LIVER KWA BROZOVIC

LIVERPOOL itaingia vitani na Real Madrid kuwania saini ya kiungo wa Inter Milan, Marcelo Brozovic, 27, katika majira ya joto. ***(Star)***

### SARRI AMFUNGUKIA RAMSEY

KOCHA wa Juventus, Maurizio Sarri amekiri Aaron Ramsey, 29, hajakuta mambo rahisi wakati alipokumbwa na majeraha nchini Italia, kufuatia kuwapo kwa uvumi wa kurudi kwenye Ligi Kuu England na Arsenal, Manchester United, Liverpool na Chelsea zote zikihusishwa naye. ***(Mirror)***

### CORONA VYAMZUZUIA IGHALO

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Mnigeria Odion Ighalo, 30, amezuiwa kuhudhuria mazoezi ya klabu hiyo kwa kuhofia tahadhari ya virusi vya corona. ***(Mirror)***

### COUTINHO AFUNGUKA LIVER

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Philippe Coutinho, 27, ametupilia mbali kuwa na mhemko wa kurudi Liverpool na kudai yupo katika "safari nyingine". ***(Sun)***

### SAKA ATEGWA MAN UNITED

MANCHESTER United inafuatilia kwa karibu hali ya mkataba wa winga Bukayo Saka, 18, na Arsenal. ***(Mail)***

### ANCELOTTI ANOGEWA EVERTON

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti (60), tayari anatupia jicho uwezekano wa kuongeza mkataba hapo Goodison Park licha ya kusaini mkataba mrefu Desemba mwaka jana. ***(Mail)***

### MADRID RADA KWA KEAN

REAL Madrid imeanika uwezekano wa kumuwinda mshambuliaji wa Everton, Moise Kean, 19. ***(Teamtalk)***

### LIVER KUMFUATA WERNER

LIVERPOOL inapanga kwenda kumsajili mshambuliaji wa RB Leipzig, Timo Werner, 23, majira haya ya joto kwa ada ya takriban pauni milioni 46. ***(Bild)***

HABARI MICHEZO

## Mwenge walia njaa wakiiwinda Mlandege

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HUKU akipania alama tatu za Mlandege katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayopigwa Uwanja wa Amaan kesho, timu ya Mwenge fc imesema kufanya kwao vibaya kunatokana na uhaba wa fedha unaowasababishia kushindwa kusajili wachezaji wenye viwango vya juu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo yenye makazi yake Kisiwani Pemba na inayoshiriki Ligi Kuu ya Zanzibar, Bajaka Mussa Rajabu, alisema ili uwe na timu nzuri na yenye ushindani lazima usajili wachezaji wenye viwango na watakaoleta mafanikio kwa timu.

Alisema timu nyingi hususan zile za kisiwani Pemba, zinakabiliwa na changamoto ya fedha hivyo kusababisha kusajili wachezaji wa viwango vya kawaida jambo ambalo halileti ushindani.

Aidha, alisema licha ya timu hiyo kuwa katika mstari wa hatari wa kushuka daraja, anatarajia kuhakikisha anapambana kuepuka janga hilo.

Pia ameliomba Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) kuendelea na mchakato wake wa kutafuta wadhamini wa Ligi Kuu ya Zanzibar ili kuzinusuru klabu na ukata wa fedha wanaokumbana nao kwa sasa.

## Kocha KMC alia na washambuliaji

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa timu ya KMC FC unalia na safu yao ya ushambuliaji ambayo imeendelea kudhihirisha ubutu wake katika michezo yake ya hivi karibuni.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Haruna Hererimana alikiri kuwapo na upungufu katika safu hiyo ambayo imekuwa ikimuumiza kichwa kila uchao.



"Safu ya ushambuliaji ina upungufu, nina kazi ya ziada kuirekebisha mpaka ikae sawa," alisema Hererimana.

Kocha huyo alisema atakaa na wachezaji wake azungumze nao ili wajue nini wanapaswa kukifanya huku akiwataka mashabiki wao wasikate tamaa na matokeo yaliyopita bali wagange yaliyopo mbele.

"Lengo ni kuendelea kubakia Ligi Kuu, tutapambana tutoke na pointi tatu kwenye kila mchezo," alisema kocha huyo wakati huu akikiandaa kikosi chake kukaribisha Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Uhuru leo.

# TWIGA STARS YAZITAKA 3 ZA MAURITANIA LEO

**Na Somoe Ng'itu,** TUNISIA

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), inatarajia kuvaana na Mauritania katika mechi ya kwanza ya kuwania ubingwa wa UNAF itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Kram ulioko jijini Tunis nchini hapa.

**Mechi hiyo ya kwanza ya mashindano hayo yanayoshirikisha nchi tano imepangwa kuchezwa kuanzia saa 11:00 kwa saa za hapa sawa na saa 7: 00 mchana kwa saa za Afrika Mashariki.**

Akizungumza na Nipashe jijini hapa, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime alisema wachezaji wake wote wako salama na wako tayari kuanza kuwania ubingwa wa michuano hiyo.

Shime alisema amewaandaa wachezaji wake kupambana na kuwa watulivu katika mchezo huo ili kuanza vema michuano hiyo na kufikia malengo ya kurejea na kombe.

Alisema anaamini kasi waliyokuwa nayo katika mashindano yaliyopita wataiendeleza na kulitangaza vema jina la Tanzania.

"Kiufundi tuko vizuri na tunaamini tutafanya vema katika mashindano haya, sijui vizuri wapinzani wetu Mauritania zaidi ya jina lao, lakini kimpira baada ya kuwaona uwanjani kwa dakika 10 nitajua mbinu zaidi za kuwamiliki," alisema Shime.

Nahodha Msaidizi wa Twiga Stars, Amina Ally, aliliambia gazeti hili kikosi chao kiko imara na wamekuja Tunisia kwa kazi moja ya kusaka ushindi katika kila mechi watakayocheza.

Amina alisema wanaamini wana uwezo wa kuibuka mabingwa na kulinda heshima waliyopewa ya kualikuwa kwenye michuano hii.

"Kama ambavyo wametuamini, sisi pia tutapambana kuhakikisha tunaanza vizuri na kujiweka katika nafasi nzuri, ukishinda mechi ya kwanza unajiongezea nguvu kuelekea mechi inayofuata, kila mechi kwetu ni sawa na fainali," Amina alisema.

Mechi nyingine ya mashindano hayo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya wenyeji Tunisia dhidi ya Morocco ambayo itaanza saa 10:15 jioni kwa saa za Tanzania.



Winga wa Azam FC, Bruce Kangwa (kulia) katika mshikemshike wa kuwania mpira na mchezaji wa Polisi Tanzania, Mohammed Kassim, kwenye mchezo wa Ligi Kuu uliopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam Jumanne wiki hii. Azam ilishinda 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Mgunda aelekeza hesabu kwa Azam*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union ya Tanga, Juma Mgunda, amesema mikakati yake kwa sasa ni kupambana na Azam FC kuhakikisha katika mechi yao ya Jumamosi anaondoka na pointi tatu ili kuendelea kujiweka katika mazingira mazuri ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Coastal tayari ipo jijini Dar es Salaam kwa ajili ya mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Uhuru Jumamosi, wakati huu ikiwa nafasi ya tano na alama zake 35 kwenye msimamo wa ligi hiyo ikizidiwa pointi tisa na Azam FC iliyopo nafasi ya pili baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 21 hadi sasa.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mgunda alisema baada ya kutoka suluhu ya bila kufunga dhidi ya KMC, sasa wanajipanga vizuri kwa mchezo wao ujao dhidi ya Azam ili kupata matokeo mazuri.

Alisema upungufu walioubaini zaidi ni katika safu yake ya ushambuliaji kutokuwa makini na utulivu wanapofika ndani ya 18 hali ambayo imewasababishia kukosa pointi tatu katika mchezo wao uliopita.

"Kwa sasa tunasahau matokeo ya KMC na kuanza mikakati ya kupambana na Azam, natumia siku mbili hizi kufanyia kazi upungufu huo, usijirudie katika mchezo unaofuata ili kupata pointi," alisema.

Alisema hawako katika nafasi mbaya ila anahitaji kupata pointi muhimu katika michezo yao ya ugenini na nyumbani ili kupanda hadi katika nafasi nne za juu ya msimamo wa ligi hiyo.

# Michezo

Ijumaa Februari 14, 2020

Nipashe




Martial amchambua Mourinho Man U UKURASA 30

GARI LIMEWAKA...



Katikati ni beki wa Simba, Muivory Coast Pascal Wawa na pembeni ni Wabrazil, beki Tairone Santos (kulia) na kiungo Gerson Fraga wakati wa mazoezi kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro kabla ya jana kutua Iringa tayari kwa mechi yao ya Ligi Kuu dhidi ya Lipuli FC itakayopigwa kesho katika Dimba la Samora. **PICHA: SIMBA**

## Kagere: Sababu kutofunga ni hii

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa Simba, Meddie Kagere, amesema kukamiwa na mabeki wa timu pinzani ni sababu inayomfanya kushindwa kucheka na nyavu kama ambavyo alivyokuwa akifanya awali.

Kagere anayeongoza katika orodha ya wafungaji Ligi Kuu akiwa na mabao 12, hajaziona nyavu kwenye mechi tatu zilizopita tangu alipofunga dhidi ya Namungo FC.

Akizungumza na Nipashe jana, Kagere alisema kitendo cha mabeki wa timu pinzani kuonekana kama wanapewa maagizo maalumu ya kumkaba kinawapa nafasi wachezaji wenzake kufunga hali ambayo kocha imemfanya Kocha Mkuu, Mbelgiji Sven Vandenbroeck kumtaka kila mchezaji anayepata nafasi kuhakikisha anafunga.

Alisema kukamiwa kwake kunawapa nafasi wachezaji wengine ndani ya timu hiyo kufunga na kupata ushindi hali inayowaongezea pointi ambazo zitawasaidia katika kufikia malengo yao ya kutwaa ubingwa.

"Hakuna sababu nyingine ambayo imenifanya kushindwa kufunga kwa muda mrefu zaidi ya kukamiwa sana, hivyo nikipata nafasi ya kufunga nitaitumia vema au kutengeneza pasi kwa wenzangu kufunga," alisema.

Kagere alisema wanahitaji kupata matokeo mazuri katika kila mechi hivyo asipofunga yeye hupambana kutengeneza nafasi na wengine kuweza kufunga.

"Ni kumuomba Mungu katika kila ninachokifanya, juhudi ya kufanya mazoezi na kufanyia kazi yale ninayofundishwa kikubwa tunachohitaji ni matokeo, mengine baadaye," alisema.

# Eymael agawa kazi Nchimbi, Molinga

**Na Saada Akida**

### ●●● Ni kutokana na kubaini ubora wake wa upishi na kumlisha mwenzake huku...

KOCHA Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, amekiri kugawa majukumu mapya katika safu yake ya ushambuliaji kwa kumbadili Ditram Nchimbi kuwa mpishi maalumu wa David Molinga.

**Nchimbi ni mshambuliaji asilia (namba tisa), lakini kwa sasa amebadilishwa na kupewa jukumu la winga wa kulia, lengo likiwa ni kuhakikisha anapiga krosi za uhakika zitakazotua ama mguuni, kifuani au kichwani kwa Molinga.**

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, kocha huyo alisema Nchimbi ana kila sifa ya kucheza kama kiungo mshambuliaji akitokea wingi wa kulia (namba saba) na hiyo ni kutokana na nguvu na kasi aliyokuwa nayo katika kulazimisha mabeki wa timu pinzani.

Alisema amefanya mabadiliko hayo baada ya kuridhishwa na uwezo wa nyota huyo ambaye ametengeneza muunganiko mzuri na Molinga ndani ya kikosi cha timu yake.

"Nilijaribu kumpanga namba tisa, ni mzuri lakini kwa sasa Nchimbi ataendelea kucheza namba saba ambayo anatimiza majukumu yake ipasavyo na lengo ni kumtengenezea mabao Molinga anayetegemea krosi kutoka kwake," alisema Eymael.

Aliongeza kuwa amemuangalia Nchimbi katika michezo ya hivi karibuni ya ligi, akiwa na mpira pembeni mara nyingi anaangalia eneo la katikati ambalo yupo Molinga ambaye ni hodari wa kupiga mipira ya vichwa na kufunga kwa miguu yote miwili.

Kocha huyo alisema sababu hiyo imemlazimu kumbadilishia majukumu Nchimbi akiamini atasaidia katika malengo yake ya kuisuka safu yake ya ushambuliaji kuwa imara zaidi.

Katika mechi za hivi karibuni, Nchimbi na Molinga wamekuwa gumzo kwa mashabiki wa timu hiyo kutokana na kuelewana vizuri huku katika winga ya kushoto, Bernard Morrison naye akiwa msumbufu kwa mabeki.

Kwenye mechi mbili za Ligi Kuu zilizopita dhidi ya Mtibwa Sugar na Ruvu Shooting, zote Nchimbi alimtengenezea Molinga bao moja moja.

Hata hivyo, Nchimbi mapema wiki hii alimwambia mwandishi wetu kuwa lengo lake ni kuona mchezaji wa timu hiyo anaibuka na Kiatu cha Dhahabu kwa kuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu msimu huu.

"Kusema nafukuzia ufungaji bora si rahisi, lakini ukiangalia wapo ambao wana mabao mengi na wenye nafasi hiyo zaidi yangu, ukweli mimi nitafurahi nikiona nakuwa sehemu ya mafanikio ya mchezaji wa timu yangu akipata nafasi hiyo," alisema Nchimbi.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >